Uzingatiaji wa Matibabu na Uponyaji wa Kiimani katika Muktadha wa VVU na UKIMWI Barani Afrika

Mwongozo wa Mafunzo kwa Viongozi wa Dini

World Council of Churches

Uzingatiaji wa Matibabu na Uponyaji wa Kiimani katika Muktadha wa VVU na UKIMWI Barani Afrika

Mwongozo wa Mafunzo kwa Viongozi wa Dini

World Council of Churches

UZINGATIAJI WA MATIBABU NA UPONYAJI WA KIIMANI KATIKA MUKTADHA WA VVU NA UKIMWI BARANI AFRIKA
Mwongozo wa Mafunzo kwa Viongozi wa Dini

Umehaririwa na Masiiwa Gunda, Nyambura J. Njoroge, Ezra Chitando, Pauline Wanjiru Njiru

Hakimiliki © WCC Publications. Mwongozo huu unaweza kunakiliwa kwa lugha ya Kiswahili kwa kukiri kikamilifu wa chanzo cha taarifa. Hairuhusiwi kuiga au kutafsiri sehemu yoyote ya chapisho hili bila idhini ya maandishi kutoka kwa mchapishaji. Tuandikie kupitia: publications@wcc-coe.org

Tunapenda kutambua na kukiri ufadhili wa kifedha uliotolewa na Mradi wa Mashirika ya Kidini wa PEPFAR-UNAIDS kwa ajili ya utayarishaji wa chapisho hili. Hata hivyo, hii haimaanishi kwamba maudhui na mawazo yote yaliyomo katika chapisho hili ni lazima yawe yanawakilisha mtazamo au maoni ya mashirika ya PEPFAR au UNAIDS na wala hayahusishi uwajibikaji wa moja kwa moja wa mashirika ya PEPFAR au UNAIDS.

WCC Publications ni programu ya uchapishaji vitabu ya Baraza la Makanisa Duniani. Likiwa limeundwa mwaka 1948, WCC ni shirika linalolenga kukuza umoja wa Kikristo katika imani, ushuhuda na huduma ili kuwa na ulimwengu wenye haki na amani. Ukiwa ni ushirika wa kidunia, WCC linayaunganisha makanisa 350 ya Kiprotestanti, ya Kiothodoksi, ya Kianglikana, na makanisa mengineyo yanayowakilisha zaidi ya wakristo 550 milioni katika nchi 110 na pia hufanya kazi kwa kushirikiana na kanisa Katoliki.

Maoni yaliyoelezwa katika machapisho ya WCC ni yale ya waandishi.

Isipokuwa kama itakuwa imeelezwa tofauti, vifungu vya maandiko katika mwongozo wa Kiswahili vimetolewa katika toleo la Biblia la Union Version

Ubunifu wa Kitabu na Mpangilio wa Chapisho: Beth Oberholtzer
Translated by Mpoki John Mwaikokesya = Imetafsiriwa na Mpoki John Mwaikokesya
ISBN: 978-2-8254-1716-4

Baraza la Makanisa Duniani
150 route de Ferney, P.O. Box 2100
1211 Geneva 2, Switzerland

www.oikoumene.org

Yaliyomo

Vifupisho iii

Dibaji vi

Utangulizi na Shukrani vii

SEHEMU YA I: Utangulizi wa Mwongozo 1

SOMO LA 1 – Utangulizi na Kusudi la Mwongozo Huu 1

SOMO LA 2 – Usuli: Uponyaji wa Kimani Katika Muktadha wa VVU na UKIMWI Katika Nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara 3

SOMO LA 3 – Namna ya Kutumia Mwongozo Huu 8

SOMO LA 4 – Kuanza Kutumia Mwongozo 12

SEHEMU YA 2: Kuuchambua Uponyaji Mkamilifu katika Muktadha wa Madai ya Uponyaji wa VVU kwa Imani Pekee 19

SOMO LA 5 – Masimulizi na Shuhuda: Matokeo ya Uponyaji kwa Imani Katika Maisha Yangu 19

SOMO LA 6 – Kuelewa Uponyaji kwa Imani na Tiba kwa Imani 29

SOMO LA 7 – Dawa za Kupambana na Virusi ni Muujiza wa Mungu 34

SOMO LA 8 – Je, ni Nani Mwenye Uhitaji wa Uponyaji? Teolojia ya Kufuatana nao 40

SOMO LA 9 – Watoto, Vijana na Wenye Umri wa Kati, na Uponyaji wa Kiimani Katika Muktadha wa VVU 47

SOMO LA 10 – Kuitazama Upya Maana ya Uponyaji kwa Jamii za Kiimani za Kimageuzi 52

SOMO LA 11 – Mikakati ya Uponyaji Mkamilifu – Kuchagua Mbinu ya Uponyaji Inayotumia Njia za Kibiolojia, Kisaikolojia, Kijamii na Kiroho 57

SEHEMU YA 3: Mbinu na Mikakati ya Kufanikisha Uponyaji Mkamilifu Katika Muktadha wa VVU na UKIMWI 64

SOMO LA 12 – Kutambua Ubia na Ushirikiano 64

SOMO LA 13 – Utetezi na Mawasiliano 71

SOMO LA 14 – Uongozi wa Kimageuzi Katika Kuleta Uponyaji Mkamilifu: Kutekeleza Utetezi 75

Viambatisho 79

Kiambatisho cha 1 – Kuwabainisha Wadau na Washirika wa kufanya nao kazi ili Kufanikisha Uponyaji Mkamilifu katika Muktadha wa Madai ya Uponyaji wa Imani Pekee 79

Kiambatisho cha 2 – Je, Teolojia ya Kufuatana Nao ni Nini? Tafakari Fupi 83

Kiambatisho cha 3 – Ukurasa Kuhusiana na Ukweli kuhusu Wenza Wenye Hali Mchanganyiko 88

Kiambatisho cha 4 – Ukurasa Unaoelezea Ukweli kuhusu Kifua Kikuu na VVU 92

Kiambatisho cha 5 – Tiba ya Dawa za Kupambana na Virusi (ART) 93

Kiambatisho cha 6 – Ratiba ya Mafunzo Inayopendekezwa kwa Wawezeshaji 95

Kiambatisho cha 7 – Ratiba ya Mafunzo Inayopendekezwa kwa Viongozi wa Dini 96

Kiambaticho cha 8 – Fomu za Tathmini ya Kabla ya Kuanza Mafunzo na Tathmini ya Baada ya Kumaliza Mafunzo 97

Vifupisho

ABC	abstain, be faithful, use a condom (jiepushe, kuwa mwaminifu, tumia kondomu)
AIDS	acquired immunodeficiency syndrome (upungufu wa kinga mwilini)
ANERELA+	African Network of Religious Leaders Living with and Personally Affected by HIV and AIDS (Mtandao wa Viongozi wa Dini wa Kiafrika Wanaoishi na Kuathiriwa na VVU na UKIMWI)
ARASA	AIDS Rights Alliance for Southern Africa (Muungano wa haki za Wenye UKIMWI Kusini mwa Afrika)
ART	Antiretroviral Therapy (Matibabu ya Kupambana na Virusi)
AWET	Apostolic Women Empowerment Trust (Mfuko wa Uwezeshaji wa Wanawake Waliopo katika Utume)
CHAZ	Churches Health Association of Zambia (Umoja wa Afya Makanisani Nchini Zambia)
CMC	Christian Medical Commission (Tume ya Kidaktari ya Kikristo)
EPN	Ecumenical Pharmaceutical Network (Mtandao wa Kiumini wa Wafamasia)
FBOs	faith-based organizations (Mashirika ya Kidini)
GBV	gender-based violence (Ukatili wa Kijinsia)
HIV	human immunodeficiency virus (Virusi vya UKIMWI)
INERELA+	International Network of Religious Leaders Living with or Personally Affected by HIV and AIDS (Mtandao wa Kimataifa wa Viongozi wa Dini Wanaoishi au Kuathiriwa na VVU na UKIMWI)
IRCU	Inter-Religious Council of Uganda (Baraza la Watu Toka Dini Tofauti Nchini Uganda)
NACC	National AIDS Control Council (Baraza la Taifa la Kuzuia UKIMWI)

NEPWHAN	Network of People Living with HIV/AIDS in Nigeria (Mtandao wa Watu Wanaoishi na VVU/UKIMWI Nchini Nigeria)
NINERELA+	Nigeria Network of Religious Leaders living with or personally affected by HIV and AIDS (Mtandao wa Viongozi wa Dini Wanaoishi au Kuathiriwa na VVU na UKIMWI nchini Nigeria)
PEPFAR	President's Emergency Plan for AIDS Relief (Mpango wa Dharura wa Rais Kusaidia Masuala ya UKIMWI)
PLWHIV	people living with HIV (Watu Wanaoishi na VVU)
SAVE	safer practice, access to treatment, voluntary testing, and counselling, empowerment (vitendo salama, upatikanaji wa matibabu, kupima kwa hiari, na ushauri nasaha, uwezeshaji)
SRHR	Sexual and Reproductive Health and Rights (Haki na Afya za Kingono na Uzazi)
SSDDIM	Stigma, Shame, Denial, Discrimination, Inaction and Misaction (Unyanyapaa, Aibu, Kukataliwa, Ubaguzi, Kutochukua hatua na Kutofanya lolote)
UAC	Uganda AIDS Council (Baraza la UKIMWI nchini Uganda)
UCMB	Uganda Catholic Medical Bureau (Shirika la Tiba la Kanisa Kikatoliki Nchini Uganda)
UKIMWI	Upungufu wa Kinga Mwilini
UNAIDS	Joint United Nations Programme on HIV/AIDS (Programu ya Pamoja ya Shirika la Umoja wa Mataifa Kuzuia VVU na UKIMWI)
UNERELA+	Uganda Network of Religious Leaders Living with or Personally Affected by HIV and AIDS (Mtandao wa Viongozi wa Dini Wanaoishi au Kuathiriwa na VVU na UKIMWI nchini Uganda)
UPMB	Uganda Protestant Medical Bureau (Shirika la Tiba la Kiprotestanti Nchini Uganda)
VVU	Virusi vya UKIMWI
WCC	World Council of Churches (Baraza la Makanisa Duniani)
WCC- EHAIA	World Council of Churches – Ecumenical HIV and AIDS Initiatives and Advocacy (Baraza la Makanisa Duniani-, Mradi wa Kiumini wa Utetezi na Kushughulikia VVU na UKIMWI)

WFP	World Food Programme (Programu ya Chakula Duniani)
WHO	World Health Organization (Shirika la Afya Duniani)
YWCA	Young Women's Christian Association (Jumuiya ya Vijana wa Kike wa Kikristo)
ZANERELA+	Zambia Network of Religious Leaders Living with or Personally Affected by HIV and (Mtandao wa Viongozi wa Dini Wanaoishi au Kuathiriwa na VVU na UKIMWI nchini Zambia)
ZAOGA-FIF	Zimbabwe Assemblies of God Africa–Forward in Faith (Kusanyiko la Mungu la Afrika Nchini Zimbabwe – Mbele Daima kwa Imani)

Dibaji

Mwongozo huu unalenga kukosoa madai ya uongo kwamba tiba ya kupambana na virusi na uponyaji wa kiimani ni pande mbili zisizokutana. Lengo la Mwongozo huu ni kuwahamasisha viongozi wa dini ili waione tiba ya kupambana na virusi kuwa ni sehemu muhimu ya mpango wa Mungu wa uponyaji. Aidha, Mwongozo huu unalenga kuwahimiza viongozi wa dini kushiriki kikamilifu katika kuhamasisha upimaji wa VVU, matumizi ya dawa na uzingatiaji wa matibabu katika muktadha wa VVU na UKIMWI.

Baraza la Makanisa Duniani (The World Council of Churches, WCC) linawashukuru wale wote ambao wamejitokeza na kueleza namna ambavyo jumuiya za kiimani zinavyoweza kuongeza ushiriki wao katika kuwasaidia viongozi wa dini kuwa na mtazamo mpana wa kiteolojia kuhusiana na suala la tiba ya kupambana na virusi na uponyaji kwa njia ya imani na kuwasaidia waweze kufanya kazi kwa karibu zaidi na watu wanaoishi na VVU pamoja na wale wanaowahudumia.

Tangu mwanzoni mwa miaka ya 1980, WCC imekuwa ikishughulika na suala la kukabiliana na changamoto kubwa za VVU na UKIMWI kwa kupitia makanisa yake wanachama na wabia wengine. Mwongozo huu ni moja ya hatua muhimu katika jitihada zinazofanywa na makanisa kushughulikia matatizo yanayowakabili watu wanaotaka kutoa matibabu yenye ufanisi kwa watu wanaoishi na VVU na UKIMWI.

WCC inawiwa shukrani za dhati kwa Mradi wa Mashirika ya Kidini wa PEPFAR-UNAIDS, kwa msaada wao wa kifedha walioutoa na kwa namna walivyolipa uzito suala la mchango wa jumuiya za kidini katika kukabiliana na VVU duniani kwa namna tofauti tofauti. Baraza linathamini ubia na ushirikiano ambao unaongeza thamani katika safari ya kupata haki na amani na hasa katika kujenga jamii ya waamini wenye upendo na wanaoshiriki katika kukabiliana na VVU.

Afya, uponyaji, na uzima ni zawadi ambayo sisi kama watu wa imani tunaweza kuwapa wengine na hata kuzitumia sisi wenyewe pale ambapo tunakuwa na utayari wa kujifunza kila mmoja kutoka kwa mwenzake. Kwa namna hiyo, mwongozo huu hutusaidia kutuwezesha kupata stadi za maisha ambazo zitasaidia jamii zetu kuwa zenye afya na jumuishi kwa wote.

Mch. Dr Olav Fykse Tveit
Katibu Mkuu WCC

Utangulizi na Shukrani

Mwongozo huu umetokana na kugundua uwepo wa madai ya uponyaji wa kiimani katika muktadha wa VVU na UKIMWI katika nchi za Afrika kusini mwa Jangwa la Sahara yenye kudhoofisha uzingatiaji wa tiba ya kupambana na virusi. Mwongozo unatambua kwamba viongozi wa dini wamewekwa kimkakati ili kuhamasisha uzingatiaji (yaani kutumia dawa kikamilifu kama ilivyoelekezwa na daktari) wa tiba ya kupambana na virusi na kupinga unyanyapaa na ubaguzi.

Mwongozo huu unajumuisha masomo yaliyoandaliwa kwa kuzingatia uhalisia, na urahisi wa kuutumia kwa wasomaji wa aina mbalimbali kutoka katika jumuiya za kiimani, na wanaotoka kwenye taasisi za kiteolojia na wale wenye kutoa elimu ya teolojia kupitia huduma za kijamii. Ni nyaraka hai ambayo inaweza kutumika katika miktadhatofautitofauti. Mwongozo umetokana na mfululizo wa mashauriano yaliyofanyika katika nchi za Kenya, Zambia na Uganda, na kuwezeshwa na Mradi na Utetezi wa Ekumeni wa WCC wa VVU na UKIMWI (WCC-EHAIA) kwa ushirikiano na jumuiya mbalimbali za kiimani, Mabaraza ya kitaifa ya UKIMWI, ushirikiano toka Programu ya UKIMWI ya Umoja wa Mataifa (UNAIDS) na Mpango wa Dahrura wa Rais wa Marekani wa Misaada katika Masuala ya UKIMWI (PEPFAR). Pia tulipokea maoni mengi sana ya thamani na ushauri kuhusu namna ya kuboresha Mwongozo huu, wakati wa warsha ya mafunzo ya majaribio kule Zambia kwa kushirikiana na Shirika la UNAIDS la Zambia pamoja na Baraza la UKIMWI la Taifa (NAC) ambayo ilijumuisha wataalamu wa masuala ya uponyaji wa kiimani katika muktadha wa VVU.

Kupitia ushirikiano na Chuo Kikuu cha Mtakatifu Paulo (SPU), kilichopo Limuru, Kenya, WCC-EHAIA imefanya kazi na watu mbalimbali kama vile watu kutoka jumuiya ya wanateolojia, walimu wa teolojia na viongozi wa dini wanaoishi na VVU ili kupata maoni yao. Aidha, Idara ya Teolojia katika Chuo Kikuu cha SPU wameanza kutumia Mwongozo huu katika mfululizo wa semina za wanafunzi wao wa somo la Teolojia wanaotoka katika nchi saba za kiafrika na wanaotoka katika madhehebu tofautitofauti. Tumefurahi pia kuona kwamba Chama Elimu ya Teolojia Afrika (All Africa Theological Education by Extension Association, AATEEA) kimepokea vizuri sana Mwongozo huu na wameuthibitisha kuwa chapisho lao kuu litakalotumika katika moduli zao za VVU na UKIMWI huku wanachama wakiendelea kushughulikia changamoto za VVU na UKIMWI katika jamii zao.

Tunakualika uutumie Mwongozo huu katika jumuiya yako ya kiimani na kutushirikisha uzoefu wako na kutuma maoni yako kwa ehaia@wcc-coe.org.

Prof Dr Isabel Apawo Phiri
Naibu Katibu Mkuu wa WCC,
Ushuhudiaji na Diakonia

SEHEMU YA I

Utangulizi wa Mwongozo

SOMO LA 1

Utangulizi na Kusudi la Mwongozo Huu

"Je! Hapana zeri katika Gileadi? Huko hakuna tabibu? Mbona, basi, haijarejea afya ya binti ya watu wangu?" (Yer 8:22).

Mwongozo huu umeandaliwa ili kuwasaidia viongozi wa dini kukuza ufahamu, ujuzi na uelewa wao kuhusiana na dawa za kupambana na virusi katika muktadha wa wa VVU na UKIMWI. Umetokana na mpango wa pamoja za Baraza la Makanisa Duniani, Mpango wa Mradi na Utetezi wa Ekumeni wa WCC wa kushughulika na VVU na UKIMWI (WCC–EHAIA), Programu ya Umoja wa Mataifa ya Kushughulikia VVU/UKIMWI (UNAIDS) na Mpango wa Dharura wa Rais Kusaidia Masuala ya UKIMWI (PEPFAR). Mpango huu unalenga katika kutaka kuimarisha mchango mkubwa unaotolewa na viongozi wa dini katika kusaidia uzingatiaji wa dawa za kupambana na virusi katika uponyaji wa VVU barani Afrika na kupinga njia hatarishi katika uponyaji wa kiimani. Njia hizo hatarishi za uponyaji wa kiimani husababisha baadhi ya watu wanaoishi na VVU kushawishika kukataa kuanza au kuendelea na matumizi ya dawa za kupambana na virusi (ART).

Mwongozo huu pia unalenga kuwahamasisha viongozi wa dini kuwa mstari wa mbele katika kutekeleza jukumu la kuhamasisha uzingatiaji wa matibabu ili kukabiliana na tatizo la VVU na UKIMWI. Mwongozo huu umekuja kutokana na kutambua yafuatayo:

- Viongozi wengi wa dini wameshiriki na wamekuwa mstari wa mbele katika kukabiliana na unyanyapaa na ubaguzi dhidi ya watu wenye VVU na UKIMWI
- Katika kushugulikia tatizo, baadhi ya viongozi wa dini wamesababisha wahanga kupata uchungu, maumivu na hata vifo kutokana na kuwakataza watu wanaoishi na VVU kutumia dawa za kupambana na virusi kutokana na imani kwamba maombi pekee au uponyaji wa kimiujiza pekee ndivyo vinavyokubalika

- Baadhi ya watu wanaoishi na VVU wamepuuza matibabu yao kutokana na mafundisho na matamko potofu ya baadhi ya viongozi wa dini
- viongozi wengi wa dini hawajapewa tahadhari ya kutosha kuhusu mahitaji maalum ya vijana wanaoishi na VVU na changamoto wanazokumbana nazo zinazohusiana na matibabu
- Viongozi wa dini wako katika nafasi nzuri zaidi ya kushirikiana na wadau wengine katika kuendelea kuimarisha afya na ustawi wa watu wanaoishi na VVU.

Mwongozo huu una makusudi yafuatayo:

- Kuwahamasisha viongozi wa dini kushiriki kikamilifu katika kuhamasishaa upimaji wa VVU, matumizi ya dawa na uzingatiaji wake kwa watu wanaoishi na VVU
- Kuwahamasisha viongozi wa dini kutambua namna ambavyo uponyaji wa kiimani na dawa za kuokoa maisha vinavyokamilishana.

Kwa Nini Mwongozo Huu ni wa Kipekee?

Katika miaka ya karibuni machapisho mengi yamekuwa yakiandikwa kuhusu VVU na UKIMWI kwa ujumla, na kwa umahususi katika eneo la uongozi wa dini naVVU na UKIMWI. Hata hivyo pamoja na uwepo wa machapisho hayo, ni machapisho machache ambayo yanashughulikia suala mahsusi la uzingatiaji wa matibabu.[1] Mwongozo huu unalenga kukidhi pengo na uhitaji huo kwa kuanzisha mjadala uliojikita kwenye suala la matibabu ya VVU katika muktadha wa uponyaji wa kiimani. Mwongozo unatoa tafakari ya kiteolojia kuhusiana na dawa za kuokoa maisha na kuwasaidia viongozi wa dini waweze kufanya ubia wenye manufaa na watu binafsi na mashirika mengine kwa ajili ya kuwasaidia watu wanaoishi na VVU.

Kwa hiyo lengo kuu la mwongozo huu ni kuwawezesha viongozi wa dini kupanua (au kukuza) mitazamo yao ya kiteolojia kuhusiana na dawa za kupambana na virusi. Mwongozo unalenga katika kukosoa madai ya uongo yaliyopo yanayoweka dawa za kupamba na virusi na uponyaji wa kiimani katika pande mbili zisizokutana. Mwongozo unajaribu kuwahamasisha viongozi wa dini kuona kuwa matumizi ya dawa za kupambana na virusi ni sehemu muhimu ya mpango wa uponyaji wa Mungu. Aidha pia mwongozo unawataka viongozi wa dini kushiriki kikamilifu katika kuhamasiha upimaji wa VVU, matumizi ya dawa na uzingatiaji wake katika muktadha wa VVU na UKIMWI.

---

1. Moja miongoni mwa machapisho bora kabisa ni lile llinaloitwa Ecumenical Pharmaceutical Network (EPN), *HIV and AIDS Treatment Literacy Guide for Church Leaders: Bridging the Gap* (Nairobi: Ecumenical Pharmaceutical Network, 2009).

SOMO LA 2

Usuli: Uponyaji wa Kimani Katika Muktadha wa VVU na UKIMWI Katika Nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara

"Watu wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa . . ." (Hos. 4:6)

Kutolewa kwa mwongozo huu kumetokana na kutambua kwamba ongezeko la madai ya uponyaji wa kiimani katika muktadha wa VVU na UKIMWI katika nchi za Afrika kusini mwa Jangwa la Sahara kunadhoofisha uzingatiwaji wa dawa za kupambana na virusi. Mwongozo huu unatambua kwamba viongozi wa dini wana nafasi nzuri zaidi kimkakati ya kuhamasisha uzingatiaji wa dawa za kupambana na virusi (kuzingatia kikamilifu maelekezo ya matibabu kama yanavyoshauriwa na daktari) na kupinga unyanyapaa na ubaguzi. Mwongozo huu pia umetokana na kugundua mambo yafuatayo:

- Ni muhimu sana kwa viongozi wa dini kutambua au kuelewa mambo mbalimbali yanayohususiana na uzingatiaji wa matibabu (yaani watu kuzingatia dozi na muda sahihi wa matumizi ya dawa zao) katika muktadha wa VVU na UKIMWI. Viongozi wa dini wana mchango mkubwa katika kutoa ushauri nasaha, kutoa miongozo na kufanya uhamasishaji
- Ingawa viongozi wa dini wameendelea kutoa uongozi muhimu katika kushugulikia tatizo la VVU na UKIMWI, suala la kutoa madai ya kutumia wa uponyaji wa kiimani pekee limerejesha dhana yenye kuonesha kwamba viongozi wa dini ni "sehemu ya tatizo" na si sehemu ya suluhisho
- Kutokana na ukweli kwamba watu wengi wanaoishi na VVU wamegundua kuwa dini ni kimbilio, ni muhimu viongozi wa dini wakawa na mafundisho yenye uzima yanayohamasisha uzingatiaji wa matibabu katika muktadha wa VVU na UKIMWI.

Uzingatiaji ni jambo muhimu katika kuzifanya dawa ulizoandikiwa zifanye kazi ipasavyo. Suala la kuzingatia matibabu ni muhimu na linahusu magonjwa yote kama vile ilivyo kwa tatatizo la VVU na UKIMWI. Hata hivyo swali la msingi linabaki ni kuwa: ¿Je, ni nini maana ya kuzingatia? Kwa lugha rahisi, inamaanisha ni kuendelea kutumia dawa katika muda wako wote wa maisha uliobaki.

Kuzingatia Kunaweza kutafsiriwa kama kiwango ambacho tabia ya mgonjwa inakuwa inaendana na maelekezo ya wahudumu wa afya kama yalivyoamuliwa kwa pamoja kati ya mgonjwa na mhudumu wa afya. Kuzingatia matibabu ni pamoja na kutumia dawa kwa wakati sahihi na kwa kiwango sahihi (WHO).

Kwa upande wa dawa ya kupambana na virusi (ART), kiwango cha uzingatiaji cha 95% ya matibabu hayo ni muhimu ili kupata manufaa na faida kamili ambazo ni pamoja na suluhisho la kiwango cha juu na la kudumu la kuzuia virusi kuzaliana, kupunguza uharibifu wa seli za CD4, kuzuia virusi kuzoea dawa, uimarishaji wa kinga, kupunguza kuendelea kusambaa kwa ugonjwa na kupunguza kiwango cha maambukizi. Hivyo basi, ni muhimu kwa viongozi wa kiimani, na watu wanaofanya kazi na kuishi na watu wenye VVU (wadau) wasaidiane katika kukuza kiwango cha uzingatiaji wa matibabu katika muktadha wa VVU na UKIMWI.

Ingawa mambo mengi huathiri uzingatiaji wa matibabu ya VVU (mambo yanayohusiana na mgonjwa mwenyewe kama vile kujikubali, kutoa taarifa, na msaada toka kwa familia yake; upatikanaji wa vituo vya afya, usaidizi kutoka kwenye jamii, nk); madai ya kutumia uponyaji wa kiimani au kimiujuza pekee kwa wagonjwa wa VVU na UKIMWI ni limeonekana kuwa ni tatizo kubwa linalosababishwa na viongozi wa dini. Katika maeneo mengi, watu kadhaa wanaoishi na VVU ama wameacha au kupuuzia matumizi ya dawa kwa kuwa tu walielezwa na viongozi wa dini kwamba walikuwa tayari wameponywa kimiujiza, na kwamba tatizo la VVU halipo tena katika mfumo wao wa kinga. Wanaambiwa waachane na matumizi ya dawa na kwamba kama hawataachana na dawa basi hiyo ni sawa na kwamba hawana imani.

Miongoni mwa mikanganyiko inayohusiana na kuwataka watu wafuate uponyaji wa VVU na UKIMWI kwa imani pekee ni pamoja na ifuatayo:

- Vifo visivyo vya lazima na vya mapema vitokanavyo na UKIMWI baada ya baadhi ya watu wanaoishi na VVU kuacha matibabu yao
- Kusababisha virusi kutosikia dawa baada ya baadhi ya watu wanaoishi na VVU kuacha matibabu
- Madai ya kutumia uponyaji wa kimiujiza pekee kwa wagonjwa wa VVU na UKIMWI katika vituo vya runinga vya serikali na vile vya binafsi, yamesababisha watu wengi wakimbilie kutafuata huduma za watu wanaotoa huduma hizo
- Ushindani miongoni mwa viongozi wa dini kunakopelekea kuwepo na, matangazo mengi na madai makubwa kuwa wanaponya VVU na UKIMWI (Hali hiyo imesababisha viongozi hao kuwashawishi watu waache matibabu ya VVU na UKIMWI)
- Kukosekana kwa uthibitisho wa uponyaji wa VVU na UKIMWI kwa njia ya imani kutoka kwa wataalamu wa dawa waliobobea (Suala hili limesababisha machakato mzima pamoja na kanisa kuwa katika mtazamo na sifa mbaya).

Madhumuni ya zoezi: Mwishoni mwa zoezi hili washiriki watakuwa wameongeza kiwango chao cha uelewa wa changamoto zitokanazo na madai ya uponyaji wa VVU na UKIMWI kwa nji ya imani pekee.

Njia za kufundishia: vikundi vidogo vidogo, majadala wa wote

Vifaa vya kufundishia: bangokitita, kalamu za maka (maka peni)

Muda: dakika 30

Mwezeshaji awagawe washiriki katika vikundi vidogo vidogo vya washiriki wasiozidi sita na atoe nafasi kwa vikundi hivyo kutafakari matokeo au madhara ya madai ya baadhi ya viongozi wa dini kudai kuwa wana uwezo wa kuponya VVU na UKIMWI kwa imani pekee.

1. Katika kusikiliza kwako vyombo vya habari mbalimbali (maongezi ya mdomo, redio, runinga, ujumbe wa simu, mabango, matangazo, nk.), je, ni madai gani makubwa yanayotolewa kuhusu kile kinachoitwa uponyaji wa VVU na UKIMWI kimiujiza?
2. Je, hao baadhi ya viongozi wa dini ni akina nani (waganga wa kienyeji, Wakristo, Waislam, na wengineo) wanaodai kuwa wana uwezo wa kuponya VVU na UKIMWI kwa imani?
3. Je, ni matokeo gani mabaya yanayotokana na madai ya wale wanaojiita waponyaji wa kimiujiza wa VVU na UKIMWI kwa familia yako, kwa jamii zetu na taifa kwa ujumla?
4. Jadili nafasi na jukumu la viongozi wa dini katika kukuza uzingatiaji wa dawa za kupambana na virusi katika muktadha wa VVU na UKIMWI.
5. Je, kuna watu unaowafahamu wanaodai kuwa wamepona kutokana na kuombewa? Je kuna watu waliokufa baada ya kuacha kutumia dawa za kupambana na virusi kwa sababu ya kushawishiwa na wanaoponya kwa imani? (washirikishe wengine simulizi na shuhuda hizo).

Wapo Kimkakati: Viongozi wa Dini na Uhamasishaji wa Uzingatiaji wa Matibabu, katika Muktadha wa VVU na UKIMWI

Mwongozo huu umetokana na kutambua kwamba ingawa baadhi ya viongozi wamelalamikia na kuonesha kukerwa kuhusu madai yanayohusiana na kile kinachoitwa uponyaji wa kimiujiza wa VVU na UKIMWI, viongozi wa dini bado wameonekana kuwa katika nafasi muhimu ya kuweza kuwashawishi na kuwaongoza wafuasi wao ili wazingatie tiba wanazopewa. Upo ushahidi unaoonesha kwamba viongozi wa dini wamekuwa wakitekeleza jukumu kubwa katika kushughulikia masuala ya VVU na UKIMWI.

Je, kiongozi wa dini ni nani?

Viongozi wa dini ni watu wanaoongoza dini katika ngazi mbalimbali kama vile katika jamii, katika taifa au ngazi ya kimataifa ambao wana jukumu la msingi katika jamii zao za kiimani, hasa wale walio kwenye mamlaka ya uongozi, na waliokabidhiwa rasmi kuwakilisha jamii au makundi hayo ya kiimani.[2]

Viongozi wa dini wana majukumu makubwa yaliyoorodheshwa hapa chini katika kuhamasiha uzingatiaji wa tiba katika muktadha wa VVU na UKIMWI:

- Kuinua viwango vyao vya ushawishi kama watu wanaoheshimika sana katika jamii kwa kuwasilisha ujumbe chanya kuhusu dawa za kupambana na virusi. Kwa mfano kueleza mtazamo kwamba dawa ya kupambana na virusi ni sehemu ya mpango wa Mungu katika kukabiliana na VVU na UKIMWI
- Kuchangia katika kuongeza ufahamu kuhusu madhara yanayotokana na kuacha au kukiuka ushauri wa daktari
- Kufahamu mambo ambayo yanaweza kuhamasisha uzingatiaji wa matibabu, kama vile uelewa na imani, na elimu kuhusu VVU na UKIMWI na uwepo wa wanamtandao wanaosaidiana (Ni lazima watilie mkazo mambo hayo.)
- Kutumia uwepo wa dini kama mahali panapoweza kukuza ufahamu kuhusu matokeo chanya ya matumizi ya dawa za kupambana na virusi, madhara yake, pamoja na mikakati ya kukabiliana na madhara hayo
- Kutangaza ujumbe chanya ambao haunyanyapai matumizi ya dawa za hospitalini na wala hautengenezi mipaka ya kubuni kati ya uponyaji wa kiimani na uponyaji wa hospitalini
- Matumizi ya vyombo vya habari katika kukosoa ujumbe potofu wenye madai ya kuponya VVU na UKIMWI kwa imani pekee
- Kutumia vyombo vya habari, matumizi ya njia zenye kuonesha ubunifu kama vile ujumbe mfupi wa simu (SMS) ili kuhamasisha uzingatiaji wa matumizi ya dawa za kupambana na virusi
- Kwa viongozi wa dini wanaoishi na VVU, kuhamasisha usaidizi kwa waumini wao pamoja na wanajamii wengine ambao wanaishi vizuri. (Viongozi hao wapo katika nafasi nzuri na wana jukumu kubwa katika kuukabili unyanyapaa na ubaguzi.)
- Kuelewa na kukuza ufahamu kuhusu mambo mbalimbali yanayosababisha uwepo wa vikwazo katika uzingatiaji wa matibabu, ambavyo ni pamoja na unyanyapaa na ubaguzi, kushindwa kujieleza, uhaba wa chakula, dini (uponyaji wa kiimani), madhara yatokanayo na matumizi ya dawa, kutokuwa na taarifa sahihi, upungufu wa dawa, na kutotosheleza kwa wataalamu
- Kushirikiana na kuunda mitandao na wadau stahiki kama vile wataalamu wa

2. Shirika la UNAIDS, *Kwa Mashirikiano na Mashirika ya Kidini, Mfumo wa Kimkakati wa UNAIDS* (Geneva: UNAIDS, 2010), 7.

afya, viongozi wa kijamii, wanaharakati (ikijumuisha makahaba) na wengineo ili kuhamasisha uzingatiaji wa matibabu.

> "Inatisha kuona kwamba katika miaka miwili hadi minne iliyopita, tumeshuhudia ongezeko kubwa la watu wanaoishi na VVU wanaoacha matumizi ya dawa na kushawishiwa na waponyaji wa kiimani; ambao ni pamoja na wachungaji na manabii, "n'angas" (waganga wa kienyeji), na wengine wengi. Hebu tutumie uwanja huu ili kujichunguza ili kujua ni nini kinachoendelea katika jamii zetu, kwa malengo ya kuja na msimamo na ujumbe wa pamoja. Hivyo ni muhimu kuelewa na kusisitiza jukumu la dini na kanisa katika vita dhidi ya VVU, ikiwa ni pamoja na unyanyapaa na ubaguzi unaohusiana na VVU." (Tamko la viongozi wa dini wa Kadoma, Zimbabwe, wakati wa warsha iliyoitwa walete pamoja viongozi wa dini na watu wanaoishi na VVU)

Kwa hiyo mwongozo huu, unalenga kuwahamasisha viongozi wa dini ili wasaidie katika kuwahamasisha watu kupima VVU, kutumia dawa na kuzingatia matibabu katika muktadha wa VVU na UKIMWI. Mwongozo huu pia unatambua kuwa viongozi wa dini wanaweza kukosoa na kupinga imani zenye madhara na zinazosababisha baadhi ya watu wanaoishi na VVU waache kutumia dawa za kupambana na virusi. Unawahamasisha pia viongozi wa dini kuwa wabunifu kiteolojia, kiuchungaji na kivitendo ili kuhakikisha kuwa wale wote waonahitaji kupata dawa za kupambana na virusi wanasisitizwa na kusaidiwa kufanikisha mahitaji hayo.

Kwa kutambua kwamba mara nyingi viongozi wa dini wanafanya kazi ndani ya sekta yao, mwongozo unalenga kuwapa viongozi wa dini ujuzi kuhusu namna ya kuanzisha na kukuza ushirikiano na ubia na wadau wengine wanaofaa ili kukabiliana na suala la madai ya uponyaji wa VVU na UKIMWI kwa imani pekee.

Hivyo basi, kwa ujumla, mwongozo huu unakusudia kuwajengea uwezo viongozi wa dini katika kushughulikia changamoto ya uwepo wa madai ya uponyaji wa VVU na UKIMWI kwa imani pekee. Mwongozo huu ni juhudi za kutaka kuwapa viongozi wa dini ufahamu na mbinu ili waweze kukabiliana na changamoto hii kwa ufanisi zaidi na kutengeneza mikakati ya ufumbuzi wa kiubunifu zaidi na wa kudumu.

SOMO LA 3

Namna ya Kutumia Mwongozo Huu

"Naye Isaya akasema, twaeni mkate wa tini. Wakautwaa, wakauweka juu ya jipu, naye akapona" (2 Wafalme 20:7)

Mwongozo huu una sehemu tatu zenye jumla ya masomo 14 (Sehemu ya kwanza ina masomo manne yanayotoa utangulizi wa jumla wa mwongozo, kwa wawezeshaji na kwa washiriki kuhusiana na masuala yatakayojadiliwa katika mwongozo wote; Sehemu ya pili ina masomo saba ambayo yanaelezea hali na mazingira ambayo watu wanaoishi na VVU wanaipitia na vile wanavyopaswa kuzingatia matibabu na uponyaji wa kiroho. Sehemu ya tatu ina masomo matatu ambayo yanahitimisha mwongozo yakihamasisha roho ya kufanya kazi kwa ushirikiano miongoni mwa taasisi mbalimbali ili kushughulikia kwa huruma mahitaji ya watu wenye VVU na UKIMWI katika jamii zetu. Sehemu, hiyo pia inawahamasisha wadau wengine waliopo kwenye kada ya uuguzi pamoja na waliopo kwenye taasisi za dini kuwa wabia wa kweli wakishiriki kikamilifu kwa kuwa na mkakati wa pamoja wa kusaidia uponyaji mkamilifu na kurefusha maisha. Aidha, masomo hayayanajadili suala la uhamasishaji na mawasiliano kuchukuliwa kwa uzito unaostahili na viongozi wote wa dini pamoja na viongozi wengine waliopo kwenye jamii za watu wanaoishi na VVU, na hivyo kuonesha uongozi mbadala wa kimageuzi wenye kuleta uponyaji mkamilifu. Masomo katika mwongozo huu yameandaliwa ili kuwasaidia wawezeshaji waweze kuaandaa shughuli mbalimbali za kujifunzia. Kufanya maandalizi ni hatua muhimu katika kuhakikisha mafunzo katika hatua mbalimbali yanafanikiwa. Hivyo basi ni muhimu sana kwa wawezeshaji kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu malengo na maudhui ya kila somo, mbinu zake za kufundishia, zana na vifaa vitakavyohitajika katika ufundishaji, rejea au vitabu vingine vitakavyohitajika ili kusaidia uendeshaji wa majadala, na pia kuelewa ujumbe muhimu utakaotiliwa mkazo zaidi kwa kila somo.

Kila sehemu kuu ya mwongozo huu imegawanyika katika vipengele vifuatavyo:

Matokeo

Sehemu hii inaeleza mambo gani yanayotegemewa kufanikishwa katika somo husika, hii inaweza kujumuisha mabadiliko katika uelewa, mtazamo au fikra, au ujuzi fulani. Kufahamu au kukumbuka dhumuni au kusudi la somo ni suala la muhimu kwa mwezeshaji, kwa sababu itamsaidia kuweka mkazo zaidi kwenye lengo kuu halisi la kujifunza. Kwa maneno mengine, kuwa na malengo haya itatusaidia kuachana na tabia iliyozoeleka ya watu kuzungumzia na kuja-

dili mambo yasiyohusiana na mada au ambayo si ya msingi au ya kipaumbele kujadiliwa.

Njia za kufundishia

Njia za kufundishia ni vitendo au mtindo ambao tunaamua kuutumia kuwasilisha mafunzo ili kufikia malengo tuliyokusudia kwa somo au mada husika. Zipo njia mbalimbali za kufundishia ambazo mwezeshaji anaweza kuchagua kuendesha mafunzo haya kutegemeana na makusudi au malengo tunayotaka kufanikisha, kama vile, banguabongo, majadiliano ya vikundi, majadiliano ya pamoja, uchunguzi kifani, igizo dhima, na maonesho.

Njia ya banguabongo

Katika njia hii mwezeshaji huandaa maswali yanayolenga kuwahamasisha washiriki kujadili mawazo, dhana, na ufumbuzi kuhusu mada husika.

Majadiliano au kazi za vikundi

Aina hii ya majadiliano hufanyika katika vikundi vidogovidogo vinavyojumuisha kati ya watu wanne au sita. Njia hii hujumuisha mwezeshaji kutoa maswali yatakayojadiliwa na washiriki katika vikundi vidogovidogo. Baada ya kumaliza kazi katika vikundi, muhtsari wa mambo yaliyojadiliwa huwasilishwa mbele ya kundi zima (yaani washiriki wote) na mmojawapo wa wajumbe kutoka katika kila kundi. Baada ya makundi yote kuwasilisha mbele ya kundi zima, mwezeshaji huhitimisha kwa, ama kufanya marekebisho muhimu au kufanya majumuisho ya mtazamo unaopaswa kufuatwa na washiriki wote.

Njia ya Uchunguzi Kifani

Uchunguzi kifani ni njia mojawapo ambayo husaidia kutoa taarifa au masimulizi ya kina ya watu (shuhuda zao), makundi, au hali fulani. Njia hii hutumika iwapo unaona kuna haja ya kuwaita washiriki ili waelewe tatizo fulani au kuchanganua tatizo pamoja na kusaidia katika kutafuta majibu yake. Katika njia hii mwezeshaji huanza kwa kutoa maswali yatakayowaongoza washiriki katika kufanya majadiliano ya suala husika.

Igizo dhima

Katika njia hii, washiriki hufikia uelewa wa tatizo fulani kwa wao wenyewe kujivika uhusika fulani katika nafasi ya mtu mwingine ambaye anakabiliwa na changamoto. Kwa kutumia njia hii, washiriki huchukua uhusika wa mtu mwingine na kuigiza mbele ya washiriki. Kupitia igizo dhima hali halisi na hisia ambazo watu hukumbana nazo huwasilishwa kwa washiriki kama zilivyo na kama vile mhusika anavyoona au kuhisi (kwa pande zote mbili, mwigizaji na watazamaji).

Uwasilishaji kwa kuhusisha washiriki

Katika njia hii, ambayo ndiyo hutumika mara kwa mara katika mafunzo, mwezeshaji huwasilisha mawazo au taarifa zilizopangiliwa au kufanya uwasilishaji kwa njia mbalimbali kama vile kompyuta (au vifaa vingine vya kuwasilishia kama vile bango kitita na ubao wa kalamu za maka). Ni muhimu sana kwamba mara zote uwasilishaji ufanyike kwa kuzingatia ushirikishwaji wa washiriki ili kuzuia mawasiliano ya upande mmoja, vinginevyo uwasilishaji utawafanya washiriki wachoke au kukerwa.

Kuna mambo kadhaa ambayo yanapaswa kukumbukwa na mwezeshaji katika kuhakikisha kuwa uwasilishaji wa mada unakuwa shirikishi:

- Ongea kwa sauti kubwa kiasi, yenye ufasaha na lafudhi nzuri (kushuka na kupanda kwa sauti) yenye kuendana na ujumbe unaotolewa. Hii itahuisha uwasilishaji.
- Tumia lugha nyepesi ambayo itaeleweka kiurahisi kwa washiriki.
- Hakikisha unawatazama washiriki. Kutazamana na washiriki kunaweza kuhamasisha ushiriki mzuri wa washiriki. Kinyume chake, iwapo utashindwa kutazamana na washiriki inaweza kusababisha wajisikie kuwa wametengwa na kuachwa.
- Uliza maswali ili kuongeza ushiriki na kuhamasisha majadiliano.
- Jizuie kuwasilisha mada kwa kusoma neno kwa neno kwa kuwa hata washiriki wanao uwezo wa kufanya hivyo. Vile vile, usisome notisi zote zilizoandikwa kwenye "andalio lako la somo". Maandalio yako ya somo yapo tu kwa ajili ya kukusaidia kukumbuka vidokezo muhimu na mtiririko wa majadiliano au hoja zinazopaswa kuongelewa.
- Epuka kusimama mahali pamoja muda mrefu. Wazungukie washiriki na tembea kutoka sehemu moja kwenda nyingine, epuka kusimama mahali pamoja kwa muda mrefu. Wasogelee washiriki ambao wanauliza maswali au wale ambao wanaonekana kutofuatilia somo au kupoteza usikivu. Waulize maswali ili kuwashirikisha katika majadiliano.
- Tumia picha na michoro katika mada unazowasilisha, lakini usizidishe sana matumizi yake; mchoro au picha moja kwa kila slaidi unatosha.
- Wape washiriki taarifa nyingine za kina katika notisi za kujisomea au vitini.
- Jitambue wewe mwenyewe, kuwa mtulivu na unayeingilika kiurahisi ili washiriki wajisikie kwamba wapo huru kuja kuongea na wewe au kukuuliza maswali.

Zana na vifaa

Sehemu hii inaonesha vifaa na zana zinazohitajika kwa ajili ya kufanya uwezeshaji wa masomo yote, vifaa unavyovichagua pia vina uhusiano sana na njia za kufundishia utakazochagua. Mwongozo huu umeandaliwa katika namna ambayo utaweza kutumiwa na viongozi wa dini kutoka katika jamii na makundi tofauti tofuti, kwa kuzingatia hilo, tunapendekeza matumizi ya vifaa vinavyopatikana kwa urahisi, yaani, bangokitita, karatasi, kalamu za maka na kalamu za kawaida. Pamoja na hayo, yapo mazingira mengine, mwezeshaji anaweza kutumia vifaa bora zaidi vya kufundishia vikiwemo projekta-akisi na kompyuta vinavyoweza kuonesha picha au kusikilizwa. Kama utaamua kutumia zana hizo utalazimika kuwa na komputa mpakato, projekta-akisi ya LCD na ubao wa komputer akisi ya kuoneshea, spika, runinga na deki yake, pamoja na vipande vya sinema fupifupi au muziki.

Mchakato

Huu ni mfululizo wa hatua mbalimbali ambazo wawezeshaji wanapaswa kuzifuata ili kuwaongoza washiriki kwa kuzingatia njia ya kufundishia uliyoichagua ili kufikia malengo ya somo husika. Mfululizo huo wa hatua umendaliwa ili kurahisisha upangaji wa masomo katika mtiririko kwa mwezeshaji, na kuhakikisha hakuna kipengele kitakachorukwa. Kwa wale wawezeshaji ambao ni wapya katika kazi hii, maelezo ya hatua mbalimbali katika kila somo yatasaidia kutoa picha ya mambo yanayopaswa kufanywa katika kila somo.

Ujumbe Muhimu

Kipengele hiki kinafanya marudio na kukazia ujumbe muhimu unaopaswa kusisitizwa au kuzingatiwa wakati wa kufundisha, kutoka katika kila mada inayowasilishwa ili washiriki “waende nazo nyumbani.”

Dondoo kwa Mwezeshaji: Mwongozo huu unajumuisha mazoezi mengi na vitendo au kazi mbalimbali, lakini mazoezi na vitendo hivyo vinatoa mwongozo wa jumla tu. Ni vema mwezeshaji akawa na uelewa wa kutosha kuhusu aina ya washiriki atakaowafundisha ili aamue idadi inayofaa ya mazoezi atakayotoa wakati wa mafunzo yatakayoendana na washiriki. Hata hivyo, tunapendekeza sana kwamba masomo yote yafundishwe katika warsha ya mafunzo. Wawezeshaji wanashauriwa kuwa wabunifu na wawe tayari kubadilika kulingana na hali halisi na aina ya wanafunzi walionao ili kuamua aina na idadi ya mazoezi pamoja na muda utakaohitajika kwa kila zoezi pasipo kuathiri ubora wa mafunzo.

SOMO LA 4

Kuanza Kutumia Mwongozo

"Naye atasema, Tutieni, tutieni, Itengenezeni njia, Kiondoeni kila kikwazacho Katika njia ya watu wangu." (Isa 57:14)

Madhumuni ya somo

Mwisho somo hili washiriki wataweza:

- kufahamiana
- kuelewa madhumuni ya warsha hii ya mafunzo
- kutengeneza kanuni za ushirikishwaji zitakazoongoza na kuyafanya mafunzo haya kuwa ya mafanikio.

Usuli

- Yafanye mafunzo haya yawe shirikishi tangu pale unapoanza. Iwapo utawashirikisha walengwa na kuwasaidia wajione kuwa wanayamiliki mafunzo, basi si tu kwamba watapata nafasi ya kusikiliza bali pia wao wenyewe watasikilizwa.
- Uwezeshaji ni jukumu zito, kwa hiyo jiandae vizuri. Hakikisha kuwa una ufahamu wa kutosha na uwe na taarifa mbalimbali kabla hujakutana na kundi unalotaka kulifundisha.
- Wawezeshaji wanaweza kuutofautisha muda uliopendekezwa kwa kila zoezi kutegemeana na mazingira na aina ya washiriki. Mambo yanayoshauriwa katika mwongozo huu ni maelekezo ya jumla tu na yanaweza kubadilika.
- Vitendo vifuatavyo vinaweza kumsaidia mwezeshaji kuamua namna ambavyo darasa lake la mafunzo litakavyokuwa.

1. Utambulisho wa washiriki
2. Sherehe ya ufunguzi
3. Matarajio ya washiriki
4. Madhumuni ya mafunzo
5. Kanuni za ushirikishwaji

Utambulisho kwa washiriki na Utangulizi wa Warsha

Ni muhimu sana kwamba washiriki wafahamiane vizuri ili waanze kushirikiana wakati wote wa mafunzo na hata baadaye. Katika mafunzo shirikishi, ni lazima washiriki wahamasishwe kutoendekeza ubinafsi, kupunguza hali ya kujilinda kupita kiasi, na kuwa tayari kufanya kazi na watu wengine kama ilivyo katika timu ya mpira. Somo hili la kwanza linahusika na mambo kama vile utambulisho binafsi, nasaha za ufunguzi, matarajio ya washiriki, madhumuni ya mafunzo na taratibu za wanafunzi kufanya kazi pamoja, ili kuandaa mazingira mazuri ya wao kushiriki katika masomo kwa uhuru kamili, kwa uhakika na wakiwa na ari. Mwezeshaji anaweza akachagua njia yoyote ile ya utambulisho binafsi, ili kulifanya zoezi zima liwe shirikishi na lenye kuwavutia washiriki. Kufanya hivyo ni muhimu hasa kwa masomo haya yanayohusu suala "zito" kuhusu VVU na UKIMWI.

Kusaidia Ufanyaji Mazoezi Yatakayotolewa kwa Washiriki

Zoezi la 1: Utambulisho kwa Washiriki

Madhumuni ya zoezi: Hadi mwisho wa zoezi hili, washiriki watakuwa wamewajua angalau washiriki wenzao watano

Njia za kufundishia: Utambulisho katika vikundi vya watu wawili wawili au utambulisho wa kundi zima

Vifaa vya kufundishia: bango kitita, vipande vidogovidogo vya karatasi na kalamu

Muda: dakika 30

Kwa kuwa mafunzo haya yatakuwa shirikishi, ni vizuri kuwaandaa washiriki ili waijaribu na kuelewa mapema maana ya njia shirikishi katika warsha ya mafunzo shirikishi, kwa kuwafanya wao wawe washiriki wakuu katika sehemu hii ya utambulisho. Kuna namna mbili za kufanikisha jambo hili:

- Unaweza ukawagawa washiriki katika vikundi vidogo vya watu wawiliwawili ili waulizane na kila mtu amtambulishe mwenzake kwa zamu wakati mwingine akiwa anasikiliza. Washiriki watahitaji kuwa na vipande vya karatasi na kalamu watakazozitumia kuandika taarifa muhimu za kila mmoja, ambazo watazitumia wakati wa kutoa utambulisho wa wenzao mbele ya kundi zima. Zoezi hili litasaidia kumfanya kila mshiriki kuwa na ufahamu mzuri na wa karibu wa angalau mmojawapo wa washiriki, na hivyo kujenga moyo wa kufanya kazi pamoja kama timu na moyo wa umoja na kushirikiana miongoni mwao. Unaweza pia kuamua kutumia njia ya "taksi." Katika njia hii mwezeshaji huita "taksi" na kila mshiriki hupanda kwenye taksi hiyo pamoja na washiriki wengine wawili, na wakati huo watatakiwa kutambulishana. Baada ya kushuka kwenye taksi washiriki watapeana zamu ya kutambulishan mbele ya kundi zima.

- Njia nyingine ni ya kuwataka washiriki kutoa utambulisho binafsi mbele ya kundi zima, kwa kufuata utaratibu utakaoamuliwa. Iwapo njia hii ya utambulisho itachaguliwa, itabidi mwezeshaji aanze kwa kuwaomba washiriki wapendekeze mambo ambayo yatapaswa kuongelewa wakati wa utambulisho huo ambayo itabidi yaandikwe kwenye bango kitita ili kila mtu ayaone. Baada ya hapo washiriki watafuata mwongozo uliopo kwenye bangokitita wakati wakijitambulisha. Angalia mfano huu hapa chini.

Utambulisho shirikishi ni ule ambao washiriki wanaongea na kushirikiana ili kusaidia kukuza hali ya kufanya kazi pamoja na kujenga timu moja ya wanamafunzo.

Mfano wa Vichwa vya Habari Katika Utambulisho Binafsi

Jina Kamili
Jina unalopendelea kutumia wakati wa mafunzo
Taasisi unayotokea
Cheo au nafasi yako kwenye taasisi

Zoezi la 2: Sherehe ya Ufunguzi

Madhumuni ya zoezi: Kufikia mwisho wa zoezi hili, washiriki wawe wameelewa mazingira na sababu za uwepo wa mafunzo haya

Njia za kufundishia: mhadhara kwa washiriki, maswali na majibu

Muda: dakika 25

Ingawa ni muhimu kuwafanya washiriki wajisikie vizuri wakati wakiwa kwenye mafunzo kwa kuwafanya wawe huru kupitia majadiliano na maongezi kati yao na mwezeshaji, na kuondoa mazingira ya urasimu, ni muhimu pia kuwafanya washiriki wayaone mafunzo haya kuwa si jambo la mzaha. Ili kuonesha uzito wa mafunzo haya na kuonesha kuwa si ya mzaha, siku ya ufunguzi wa mafunzo, washiriki wahutubiwe na viongozi wa taasisi zinazosimamia mafunzo haya au washirika wao pamoja na wabia wengine (mfano watu kutoka WCC, Shirika la UKIMWI Duniani (UNAIDS); Waziri toka serikalini katika nchi ambapo warsha inafanyikia) wakielezea hali ya sasa ya VVU na UKIMWI nchini na juhudi ambazo zinafanyika kukabiliana na tatizo. Uzito na umuhimu wa mafunzo haya utategemea pia mhusika atakayefanya ufunguzi; hivyo basi kuna haja ya kutafuta maafisa wa ngazi za juu kuungana na washiriki na kutoa hotuba, wakisistiza jukumu kubwa la jumuiya za kidini na viongozi wa dini katika kusaidia juhudi za serikali katika kukabiliana na VVU.

Si lazima kwamba wageni waalikwa wakae siku nzima pamoja na washiriki, kwa sababu hicho kinaweza kuwa ni kikwazo kwa washiriki kukosa uhuru wa kutoa mawazo na kushiriki kikamilifu katika majadiliano. Kwa hiyo njia nzuri

yaweza kuwa ni kwa viongozi kuja kutoa hotuba na mara tu baada ya hotuba waruhusiwe kuondoka wasiwepo kwenye mafunzo na pengine wanaweza kutembelea tena mwishoni.

Zoezi la 3: Matarajio ya Washiriki

Madhumuni ya zoezi: Kupima na kujua mambo ambayo washiriki wanayatarajia kuyapata kutokana ushiriki wao katika mafunzo haya

Njia za kufundishia: majadiliano ya pamoja, fomu ya tathmini ya awali

Vifaa vya kufundishia: vipande vidogo vidogo vya karatasi, bangokitita, fomu ya tathmini ya awali, kalamu za kawaida, kalamu za maka

Muda: dakika 30

Mara nyingi wawezeshaji huwa wanafanya kosa kwa kudhani kwamba wanaelewa mambo na matarajio ambayo washiriki wanayapendelea au kuwa nayo. Hali hii inapotokea, washiriki wanaweza kujitoa kabisa katika mafunzo kwa sababu ya kukosa sauti na maamuzi kuhusiana na mafunzo haya. Hata hivyo hii haimaanishi kwamba wawezeshaji waje pasipo kufanya maandalizi. Tofauti na hilo, hii inamaanisha kwamba wawezeshaji wanatakiwa watengeneze mazingira yatakayoruhusu washiriki kuchangia katika kupanga na kutekeleza mafunzo kwa kueleza matarajio, mashaka au hofu walizonazo mwanzoni mwa mafunzo. Baada ya hapo mwezeshaji anaweza kuoanisha majibu au matokeo yatakayopatikana na madhumuni ya mafunzo na kufanya marekebisho au maboresho katika mafunzo au njia za ufundishaji ili kikukidhi matarajio halisi na kuondoa hofu za washiriki. Ni muhimu pia kwa mwezeshaji kuwa na uhakika na kuwa mkweli kuhusu matarajio ya washiriki ambayo hayataweza kutimizwa au ambayo yako nje ya lengo kuu. Mwezeshaji anaweza kufanikisha hili pia kwa kutumia njia ya majadiliano ya pamoja au kutumia fomu ya tathmini ya mahitaji ya awali (angalia mfano hapo chini), ambayo washiriki huchukua wakati wanajisajili, kuijaza na kuiwasilisha.

Ili kufanikisha kusudi hili, mwezeshaji anaweza kujaribu mbinu moja au zaidi kati ya hizi zifuatazo:

- Kusoma majibu yaliyopo kwenye fomu za tathmini ya awali, kuchukua mawazo makuu ya pamoja na kuyaandika kwenye bangokitita
- Pale ambapo hakuna fomu za tathmini ya awali, waombe washiriki waandike matarajio na hofu zao kuhusiana na mafunzo (kila mtu aandike peke yake), kisha soma kwa sauti hayo waliyoyaandika mbele ya kundi zima (angalia mfano hapo chini).
- Iwapo mwezeshaji ataamua kutumia njia ya mazungumzo, itabidi awaombe washiriki waelezane matarajio yao kila mmoja kwa kuuliza swali hili, “je unatarajia kupata nini kutokana na mafunzo haya?”

Ni lazima mwezeshaji ahakikishe kuwa mawazo makuu na yale yanayotofautiana yanaandikwa kwenye bangokitita ili washiriki wayaone. Matarajio,

hofu na matumaini haya ni lazima yaendelee kuonekana kwa washiriki muda wote wa mafunzo, kama itawezekana, mwezeshaji, awaeleze washiriki kuwa ni wakati gani katika mtiririko wa mafunzo matarajio yao yatakuwa yanatimizwa.

Fomu ya Tathmini ya Awali

Fomu hii ijazwe na kila mshiriki peke yake pasipo mwingine kujua kilichojazwa na mwenzake

1. Unaelewa nini kuhusu uhusiano uliopo kati ya imani na uponyaji? (acha nafasi kwa ajili ya kuandika majibu)
2. Je, unadhani kuna uwezekano wa mtu anayeishi na VVU na UKIMWI kupona? Fafanua kwa ufupi. (acha nafasi kwa ajili ya kuandika majibu)
3. Je, nini mategemeo yako kwa kuja na kuhudhuria mafunzo haya? (acha nafasi kwa ajili ya kuandika majibu)
4. Je, ni nini hofu uliyonayo kuhusiana na mafunzo haya? (acha nafasi kwa ajili ya kuandika majibu)

Mifano ya Matarajio ya Washiriki

- Kufahamu uhusiano uliopo kati ya uponyaji, tiba, na matibabu
- Kupata mbinu za namna ya kufanya kazi na watu wanaoishi na VVU katika muktadha wa madai ya uponyaji kwa imani
- Kujifunza na kutafakari njia mbalimbali za namna uponyaji unavyotafsiriwa, hasa kutokana na uzoefu kutoka kwa watu wanaoishi na VVU

Mifano ya Hofu

- Kwamba baadhi ya washiriki hawataweza kutoa maoni yao kwa kuogopa kuwa wataitwa wadhaifu wa imani
- Kwamba tunaweza kushindwa kujenga uelewa utakao wahamasisha watu wote kuanza kuzingatia matibabu yao
- Kwamba muda ambao umepangwa kwa ajili ya mafunzo haya utakuwa mfupi iwapo kutakuwa na ushirikishwaji na majadiliano

Zoezi la 4: Madhumuni ya Mafunzo

Madhumuni ya zoezi: Kuwafanya washiriki waelewe na kutambua lengo kuu la mafunzo kwa kuwaruhusu waweze kufananisha malengo ambayo mwezeshaji aliyakusudia na matarajio ambayo wao walikuwa nayo kutoka katika zoezi lililopita.

Njia za kufundishia: majadiliano ya kundi zima

Vifaa vya Kufundishia: bangokitita, kalamu za maka

Muda: dakika 15

Ni lazima mwezeshaji aje na malengo au madhumuni ya mafunzo ambayo ameyatafakari kwa kina. Madhumuni hayo ni lazima yawekwe wazi kwa washiriki wote, ama kwa kuoneshwa ukutani kwa kutumia projekta au kwa kuandika kwenye bangokitita (angalia mfano hapo chini). Mwezeshaji atatakiwa kuwapitisha washiriki katika malengo na madhumuni ili kukuza uelewa miongoni mwao. Katika hatua hii ni muhimu pia kwa mwezeshaji kuwasaidia washiriki kutambua anachokikusudia kwa kutaja malengo hayo; hata hivyo mwezeshaji asiwalazimishe washiriki kukubaliana na malengo yake.

Baada ya uwasilishaji wa malengo na madhumuni, mwezeshaji awasaidie washiriki kufananisha malengo waliyokuwa nayo kabla na yale yaliyowasilishwa na aoneshe namna malengo hayo yanavyooana au kutofautiana. Ni muhimu kukumbuka kwamba pale ambapo washiriki watakuwa na matarajio makubwa zaidi kuliko malengo ya mafunzo, mwezeshaji anaweza kuyashughulikia matarajio hayo ama kwa kurekebisha programu nzima au shughuli za mafunzo, au kuwaonesha washiriki kwa nini itakuwa vigumu kuyatimiza matarajio yao katika muda wa mafunzo haya.

Madhumuni ya Mafunzo

1. Kuwasaidia washiriki kupata maarifa na taarifa za kutosha na zenye ushahidi kuhusiana na hatari ya madai ya uponyaji wa kiimani yanayofanywa na baadhi ya viongozi wa dini
2. Kuwasaidia washiriki kuwa na uelewa mbadala kuhusiana na uponyaji wa kiimani katika muktadha wa VVU na UKIMWI
3. Kuwasaidia washiriki kupata mbinu kuhusu uelewa mbadala na sahihi kama msingi wa kuwafanya watu wanaoishi na VVU wazingatie tiba

Wawezeshaji pia wajadili kuhusu muda wa kuanza na muda wa kumaliza mafunzo pamoja na muda wa chakula ili kuwafanya washiriki waone kuwa mpango mzima wa mafunzo unamilikiwa na wao wenyewe. Jambo hili la kuwashirikisha ratiba ni muhimu zaidi kwa washiriki wanaotokea majumbani mwao tofauti na wale wanaokaa hapo hapo.

Zoezi la 5: Kanuni za Mafunzo

Madhumuni ya zoezi: Kufikia mwishoni mwa zoezi hili, washiriki watakuwa wametunga kanuni kadhaa za mafunzo au kanuni za maadili zitakazowaongoza namna watakavyoshiriki mafunzo katika muda wote wa mafunzo haya.

Njia za kufundishia: vikundi vidogo vidogo, majadiliano ya pamoja

Vifaa vya kufundishia: bangokitita, kalamu za maka

Muda: dakika 30

Kunapokuwa na washiriki wengi katika programu ya mafunzo, kuna mienendo mingi ambayo inaweza kujitokeza. Iwapo mienendo hiyo haitasimamiwa vizuri, inaweza kuingilia na kuharibu kazi nzuri na juhudi zilizofanywa katika kuandaa mafunzo haya. Moja kati ya mienendo hiyo ni pamoja ifuatayo: kila mshiriki ni mtu binafsi na ana matarajio na tabia yake ambayo ni tofauti na wengine; kwa pamoja washiriki huunda kundi linalojumuisha makundi rika yenye baadhi ya tabia zinazolingana; washiriki humwangalia mwezeshaji kama kiongozi na mwenye maamuzi ya mwisho. Mahusiano haya miongoni mwa mtu mmoja mmoja, kundi au makundi na kiongozi yanahitaji kusimamiwa vizuri ili kuwa na mafanikio ya mafunzo. Pia ni lazima kufahamu kuwa, miongoni mwa washiriki, wapo wenye tabia mbalimbali zikiwemo zile za kutaka kutawala mazungumzo, na wengine wenye aibu. Aina zote hizi za washiriki zinahitaji usimamizi mzuri ili kufanikishwa matumizi ya mbinu shirikishi; vinginevyo wale wenye tabia za kutaka kutawala mazungumzo watatawala somo zima na kuwafanya wengine wasiongee kabisa.

Ili kufanikisha matumizi ya mbinu shirikishi, ni vizuri mwezeshaji akawasaidia washiriki kukubaliana kuhusu kanuni zitakazoongoza mafunzo (angalia mfano hapo chini) au mwongozo wa kimaadili ambao utawafanya washiriki wote waweze kusikilizwa, kuwasikiliza wengine, kueleweka, na kuheshimiwa katika muda wote wa mafunzo. Ili kufanikisha hili, ni vizuri mwezeshaji akawagawa washiriki katika vikundi vidogovidogo vya watu wasiozidi sita. Kila kikundi kichague mwenyekiti na katibu, ambao watatengeneza mapendekezo yao ya kanuni za kundi na kuzijadili na baadaye kuziwasilisha katika majadiliano ya pamoja. Wakati wa majadiliano ya pamoja, mwezeshaji lazima ahakikishe kanuni zinazoshabihiana zinaandikwa kwenye bangokitita ili ziwe wazi kwa washiriki wote katika muda wote wa mafunzo ili kukumbusha umuhimu wa kuzizingatia kanuni hizo na umuhimu wa kuzifuata.

Mifano ya Kanuni za Mafunzo

- Kuwasili kwa wakati ni jambo la maadili
- Simu zote ama zitawekwa katika mfumo wa kutotoa sauti au kuzimwa
- Hatutamdharau mtu yeyote kwa sababu yoyote ile au kudharau mawazo yake
- Kuzingatia ufupisho ni jambo jema
- Kusikikiliza ni ishara ya kuheshimu. Usimkatishe mwenzako, sikiliza kwa makini

SEHEMU YA 2

Kuuchambua Uponyaji Mkamilifu katika Muktadha wa Madai ya Uponyaji wa VVU kwa Imani Pekee

SOMO LA 5

Masimulizi na Shuhuda: Matokeo ya Uponyaji kwa Imani Katika Maisha Yangu

"Amin, nawaambieni, Kila patakapohubiriwa Injili hii katika ulimwengu wote, tendo hilo alilolitenda huyu litatajwa pia kwa kumbukumbu lake." (Mathayo 26:13)

Madhumuni ya somo

Kufikia mwisho wa somo hili, washiriki watakuwa:

- Wamesikiliza simulizi toka kwa watu wanaoishi na VVU na kuongeza uelewa wao wa uponyaji kwa imani.
- Wameweza kudhihirisha madhara na hatari zitokanazo na madai ya kutegemea uponyaji kwa imani pekee kupitia masimulizi ya watu ambao walinusurika kufa kutokana na kutozingatia matibabu yao.
- Wameweza kudhihirisha uelewa chanya kuhusu hali ya kutegemeana iliyopo kati ya uponyaji kwa imani na uzingatiaji wa masharti ya matibabu.

Usuli

Wakati tukiwa kwenye mashauriano pale Kampala mwaka 2017, baadhi ya watu kutoka nchi za Nigeria, Kenya na Uganda waliombwa kusimulia maisha yao na namna wanavyoishi na VVU na athari ya dini au imani maishani mwao. Lengo la somo hili ni kusaidia kupaza sauti za baadhi ya simulizi zilizotolewa pale Kampala na pia kujaribu kutengeneza uwanja ambapo simulizi nyingine za namna hii kutoka kwa washiriki wa mafunzo haya zitatolewa, na hasa wakati wakufanya mazoezi yaliyoko kwenye somo hili.

Simulizi binafsi na shuhuda zisitolewe kwa kuwalazimisha washiriki bali ni zitolewe kwa hiari na washiriki ambao wana utayari wa kuelezea hatua mbalimbali za maisha yao. Iwapo kutakuwa hakuna mshiriki yeyote mwenye utayari wa kuelezea uzoefu wake wa maisha, washiriki wanaweza kuelezea simulizi za maisha ya watu wengine wanaowafahamu wakihakikisha kuwa hawataji majina ya wahusika isipokuwa kama watakuwa wamepata kibali cha kufanya hivyo.

Baada ya kila simulizi na shuhuda binafsi kutolewa, zoezi litatolewa ili kuwafanya washiriki washirikishwe katika simulizi zilizotolewa ili kuongeza uelewa wao wa maudhui na jumbe kuu zilizomo kwenye mafunzo hayo.

Simulizi na Shuhuda

Aisha kutoka Nigeria

Aisha ni mwanamke wa Kiislamu kutoka Nigeria, ambaye alitusimulia kuhusu namna anavyoishi na VVU kule Nigeria. Aisha alipitia uzoefu wa kukeketwa (FGM), ambao wengine huita tohara kwa wanawake. Aisha alitushirikisha uzoefu wake na kutueleza kwamba kutokana na tohara hakuwahi kufurahia tendo la ndoa tangu alipoolewa. Akiwa msichana mdogo aliolewa na mtu mzima ambaye alikuwa akimpiga mara kwa mara. Hatimaye walitengana na mume huyo wa kwanza na baadaye aliolewa na mume mwingine. Hata hivyo matatizo ya Aisha yaliendelea na hivyo alitengana na mume wa pili na kuolewa na mume wa tatu, ambaye alikuwa akiishi na VVU lakini hakuwa amemweleza Aisha. Hivyo Aisha alipata maambukizi ya virusi kutoka kwa mumewe na mara baada kugundulika kuwa ni mwathirika wa VVU kwa waumini wenzake na jumuiya yake ya dini walimuona kama mtu aliyewafedhehesha na hivyo wakamtenga. Alipoanza kuugua, alifungiwa kwenye chumba cha peke yake kwa muda wa miaka miwili, na kutengwa kabisa na ulimwengu wa nje kwa sababu jamii haikutaka watu wa nje wajue kwamba mmoja wa wanafamilia alikuwa akiishi na kuteseka kutokana na VVU. Alitelekezwa na kukataliwa na watu wa jamii ya imani yake na hata ndugu zake hawakujisumbua kumwokoa. Alifungiwa kwenye chumba ili afie huko na kitu pekee alichopewa ili kumliwaza, ilikuwa ni redio ndogo. Hata hivyo badala ya redio kuwa faraja kwake iliendelea kuwa sehemu ya mateso kwa sababu ilijaa ujumbe wa viongozi wa dini na wale wa kijamii wenye kuwahukumu watu wanaoishi na VVU, na hivyo aliamua kutoendelea kusikiliza redio tena.

Kulikuwa na jamii za wakristo katika jamii aliyokuwa akiishi na siku moja, sista wa Kikatoliki aliarifiwa kwamba kulikuwa na mwanamke ambaye alikuwa amefungiwa chumbani kutokana na kuugua VVU. Sista huyu, aliyeitwa Johana aliamua kumchukua Aisha na kumpleka katika kanisa lake, ambapo aliendelea kumuuguza Aisha na alimtafutia dawa na kumuonesha upendo, kumjali na kumpatia dawa za kupambana na virusi. Taratibu afya ya Aisha ilianza kuimarika. Alipokuwa amepata afya kiasi cha kutosha, Sista Johana alil-

iomba Kanisa limwajiri, na hivyo akaanza kupata kipato chake mwenyewe na akaweza kujitegemea. Kwa muda wote huo ambao Aisha alikuwa akitunzwa na Sista Johana, hakuwahi kumwambia abadili dini yake na kuingia kwenye ukatoliki, yeye alionesha tu kumjali kama binadamu wengine walioumbwa kwa mfano wa Mungu. Baadaye alitokea mwanaume mwingine ambaye alimposa Aisha na wakaoana mwaka 2006 na wakaendelea kuwa wanandoa. Mume huyu mpya alimkubali Aisha kwa hali aliyokuwa nayo. Leo, Aisha ana-jisifu kuwa mama na bibi wa watoto waliofanywa yatima na ugonjwa wa VVU na UKIMWI nchini Nigeria.

Alimalizia kutoa ushuhuda wake kwa kueleza kwamba jamii za kiimani na vyombo vya habari – kupitia redio aliyokuwa amepewa vilichangia sana katika kumfanya anyanyapaliwe na kubaguliwa. Alitueleza pia kuwa kupitia kanisa Katoliki, na hasa kupitia Sista Johana, aliuona uponyaji chanya wa imani. Yeye anatafsiri uponyaji wa kiimani kuwa ni hali ya kujikubali kunakotokana na upendo, matunzo, pamoja na matumizi ya dawa za kupambana na virusi ambayo alielekezwa kutumia, vyote hivi vilichangia kumfanya aishi maisha mapya ndani ya mwili uliokuwa unakaribia kupoteza uhai.

Zoezi

Madhumuni ya zoezi: Mwishoni mwa zoezii hili, washiriki watakuwa wametafakari simulizi ya Aisha na kutambua namna ambavyo inaweza kuwahusu. Pia wataelewa hali ambayo watu wanaoishi na VVU wanaipitia na namna wanavyoutazama uponyaji wa kiimani.

Njia za kufundishia: vikundi vidogo vidogo, majadiliano ya pamoja

Vifaa vya kufundishia: bangokitita, kalamu za maka

Muda: dakika 20

Mwezeshaji atawagawa washiriki katika vikundi vya watu wasiozidi sita na kuviruhusu vikundi hivyo kusoma simulizi ya Aisha na baadaye kuitafakari na kufanya mazungumzo kwa kuongozwa na maswali na hoja zifuatazo:

1. Orodhesha mambo mabaya ambayo Aisha ameyapitia maishani mwake na onesha ni nani (mtu au taasisi) amesababisha apitie hali hiyo.
2. Kwa nini Aisha alifungiwa kwenye chumba na familia na jamii yake? Mbali ya kufungiwa, ni mambo gani mengine ambayo watu wanaoishi na VVU katika jamii yako huyapitia?
3. Je, unadhani ni hatua gani ambazo jamii anayoishi Aisha ingetakiwa kuchukua badala ya kumfungia chumbani?
4. Aisha anasema amepona, je ni namna gani Aisha amepata uponyaji huo? Je, uelewa wa Aisha wa uponyaji una maana kwamba sasa hahitaji tena kutumia dawa zake za kupambana na virusi?
5. Kwa mtazamo wako, unadhani Aisha amepona?

Maureen, kutoka Kenya

Maureen ni mwanamke, mkristo ambaye si wa makamo sana, ni mama aliyeolewa. Baba yake Maureen alikuwa na wake wengi na wazazi wake walitengana wakati Maureen akiwa bado mdogo. Maureen alikuwa na wadogo zake wawili. Baada ya kuachika, mama yake aliolewa tena, na Maureen na wadogo zake walikwenda kuishi na bibi yao mzaa mama. Baada ya hapo maisha yalibadilika na kuwa magumu sana kwa kuwa mama yake hakuwa anawajali sana kwa sababu alikuwa akiangalia zaidi maisha yake mapya. Wajomba zake hawakuwakubali kamwe Maureen na wadogo zake; waliwakataa na hawakutaka kuchukua jukumu la kuwatunza. Hali ilizidi kuwa mbaya zaidi pale mama yake Maureen alipokufa. Wakati huu Maureen ndiye ilibidi achukue jukumu la kuwatunza wadogo zake. Ili kumudu hilo alilazimika kutafuta kazi katika shirika la Kikristo la "Young Women's Christian Association" (YWCA) kama mwelimishaji-rika. Aliona kwamba kazi hii ingemfaa maana ingemwezesha kuwatunza wadogo zake. Hata hivyo kazi hii ilihusisha kusafiri sana, na hivyo kumaanisha kuwa mara nyingine alitakiwa kulala mbali na nyumbani kwao. Wajomba zake wakaanza kumtuhumu kuwa ni kiruka njia, na kwamba alikuwa akisingizia majukumu yake ya kikazi na kwamba alikuwa akilala nje na wanaume. Hivyo basi wajomba zake wakamfukuza yeye na wadogo zake kutoka kwenye nyumba ya bibi yao. Yatima hawa waliachwa pasipo mahali popote ambapo wangeweza kupaita nyumbani. Ikabidi Maureen atafute mahali pa kupanga ili aishi na wadogo zake.

Baadae akaanza mahusiano ya kimapenzi na kijana mmoja wa kiume. Kwa kuwa hakuwa na ujuzi wa kutafuta mwenza sahihi na wala hakuwa na ujuzi wa kufanya maamuzi kuhusu masharti ya mahusiano, mahusiano ya kingono kabla ya ndoa ikawa ni jambo halisi kwake. Baadaye rafiki yake wa kiume alikamatwa na kufungwa jela kwa muda wa miaka miwili akiwa tayari amempa ujauzito wa mtoto wake wa kwanza. Baadae Maureen aliolewa na alipopata ujauzito wa mtoto wa pili, alianza kupata homa za mara kwa mara. Alipoenda kliniki kabla ya kujifungua na kupimwa VVU, akagundulika kuwa alikuwa ameathirika na VVU. Maureen alichanganyikiwa na aliogopa sana alipowaza namna ambavyo mume wake angejisikia iwapo angepata taarifa hizo. Baada ya muda Maureen aliachana na masuala ya kliniki na kuamua kwenda nyumbani kwa rafiki yake ambaye alimuamini na alikuwa na uhakika kwamba rafiki yake huyo asingemkana. Rafiki yake huyo akawa mtu wa msaada sana kwake baada ya kupata taarifa kuhusu Maureen. Kupitia rafiki huyu, ndipo mume alipigiwa simu na kupewa taarifa za afya na vipimo vya Maureen. Pasipo kujua kwamba, mumewe pia tayari alikwishajijua kuwa yeye mwenyewe alikuwa ameathirika, alipomueleza alikubaliana na hali na akawa wa msaada sana kwa Maureen.

Hivyo mume na mke wote wakaanza kupata matibabu ya dawa za kupambana na virusi na wakawa wakisaidiana na kukumbushana kuzingatia matibabu. Dawa za kupambana na virusi zilikuwa msaada mkubwa, mtoto wao

alizaliwa akiwa hana VVU na pia wanatarajia kupata mtoto wa tatu. Muda wote ambapo alikuwa na tatizo, na baada ya kubainika kuwa ameathirika na VVU, Maureen alifarijika na kupata nguvu kutoka kwa mchungaji wake ambaye alimhamasisha kuendelea kutumia dawa za kupambana na virusi na kuzingatia matibabu yake na wakati huo huo alimuombea ili apate nguvu zitakazomsaidia kutoacha kutumia dawa. Maombi ya mchungaji yakiambatana na umakini katika kuzingatia matumizi ya dawa za kupambana na virusi na msaada wa uangalizi kutoka kwa marafiki na mume wake vimeleta uponyaji kwa Maureen.

Zoezi

Madhumuni ya zoezi: Mwishoni mwa zoezi hili, washiriki watakuwa wamesikiliza na kutafakari changamoto ambazo husababishwa na mila na desturi kwa watoto wadogo na waone ukubwa wa mateso au usumbufu unaosababishwa na mila na desturi.

Njia za kufundishia: vikundi vidogovidogo, majadiliano ya pamoja

Vifaa vya Kufundishia: bangokitita, kalamu za maka

Muda: dakika 20

Mwezeshaji atawagawa washiriki katika vikundi vidogovidogo vya watu wasiozidi sita na kuvisaidia vikundi hivyo kusoma simulizi ya Maureen na baadae waitafakari, na kuijadili kwa kutumia maswali na hoja zifuatazo:

1. Je, ni mila gani na tamaduni ambazo unadhani zimesababisha matatizo ambayo Maureen na wadogo zake wameyapitia? Kwa nini unafikiri hivyo?
2. Je, unadhani ni kwa namna gani matendo ya watu wazima yaliyofanyika katika maisha ya Maureen yalisababisha yeye aathirike na virusi vya UKIMWI?
3. Pamoja na kwamba Maureen ataishi maisha yake yote yaliyobaki akiwa na virusi, yeye anajisikia kwamba amepona. Je, ni mambo gani katika maisha yake ambayo yanamfanya ajisikie kuwa amepona? Je, unauelewa uelewa wake wa kuponywa?
4. Je, wewe ukiwa ni mtu wa dini, unakubaliana na mtazamo kwamba uponyaji hupatikana kwa wale ambao hawaachi na wanaendelea na matibabu?

Jemima kutoka Uganda

Jemima ni mwanamke mwenye umri wa kati kutoka Uganda ambaye alijiingiza katika mahusiano kwa mategemeo ya kuolewa mara tu baada ya kuanza mahusiano. Jemima anatoka katika kizazi cha watoto ambao walizaliwa kabla ya upatikanaji wa dawa za kupambana na virusi na dawa zenye kuzuia maam-

bukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. Hivyo, Jemima alizaliwa akiwa na maambukizi ya VVU. Mama yake Jemima alipata maambukizi kupitia damu lakini baba yake hana maambukizi ya VVU. Baada ya kugundua kuwa mkewe ana maambukizi ya VVU, hakuikimbia familia yake bali yeye akageuka kuwa nguzo ya familia.

Ingawa Jemima alianza matumizi ya dawa mapema katika maisha yake, alipambana na changamoto kubwa ya unyanyapaa na kukataliwa na marafiki zake na wenzake mara baada ya kugundua kuwa alikuwa akisumbuliwa na magonjwa mbalimbali kwa kuwa alikuwa ameathirika na VVU. Kutokana na kiwango cha unyanyapaa kuzidi sana akalazimika kuacha matibabu na dawa zake na akaanza kudhoofika kiafya. Jemima pia alikuwa akinyimwa chakula na marafiki zake pamoja na watu wengine kule shuleni. Mara kadhaa marafiki zake walikuwa wakigawana chakula chote mezani na kurudisha kwa mpishi chakula kilichobaki ambacho Jemima alipaswa kupewa na hivyo kumshindisha au kumlaza njaa. Kwa kadri muda ulivyozidi kwenda, aliendelea kudhoofu sana kiasi ambacho hata baba yake alipomtembelea shuleni kwao alimbeba mikononi mwake na kumpeleka hospitali. Kipimo chake cha kiwango cha virusi kiliongezeka sana kiasi kwamba kama asingewahi matibabu angeweza kufa. Kwa kuwa shuleni hapakuwa mahali salama tena kwa ajili ya binti yake, baba aliamua kumwondoa na kumpeleka kusoma katika chuo cha fasheni na ubunifu. Hivi sasa Jemima ni mtaalamu wa fasheni na ubunifu.

Alipopelekwa hospitali alianza matibabu ya dawa za kupambana na virusi, Jemima alisisitizwa na baba yake kuzingatia matibabu yake. Akiwa katika chuo cha fasheni na ubunifu, alikutana na kijana mmoja kutoka Uganda kaskazini na wakawa wapenzi. Kijana huyu ndiye mchumba wa Jemima. Mwanzoni alipokuwa amependana na yule kijana, ilikuwa ni vigumu sana kuweka wazi kwa rafiki yake wa kiume kuwa alikuwa akiishi na VVU na alianza kuandaa mkakati wa namna ya kumweleza. Alimtaka rafiki yake wa kiume atafakari mazingira mbalimbali ambayo yanaweza kutokea. Akaja na swali la mtego kwa rafiki huyu wa kiume ambalo lilikuwa "Hivi ukisikia kwamba nimeugua kansa, bado utaendelea kunipenda?" Jibu likawa ndiyo. Akauliza tena. "Je kama utasikia kwamba sina uwezo wa kupata watoto, utaendelea kunipenda?" Hapa jibu tena likawa ndiyo. Majibu haya yakampa Jemima ujasiri, hatimaye akaamua kumweleza ukweli, "Unajua nini, mimi nilizaliwa nikiwa mwathirika wa VVU na ninaishi na virusi." Rafiki yake wa kiume akasema kuwa yeye bado anampenda. Baada ya uhusiano wao kuwa wazi kwenye jamii yao, mchungaji wa yule kijana alimwita na kumshauri avunje uhusiano na kuachana na msichana ambaye tayari alikuwa ameathirika na VVU na wakati yeye alikuwa hajaathirika. Kijana yule aliambiwa kwamba kuingia katika mahusiano ya aina ile, ingekuwa kama mtu anayetia saini kwenye hati yake ya kifo. Pamoja na kuambiwa hivyo, kijana huyo aliendelea kuwa ni nguzo ya kumuimarisha Jemima na chanzo chake cha uponyaji wake. Amejiwekea utaratibu wa kila siku kumkumbusha Jemima kumeza dawa zake pasipo kukosa. Kwa maelezo ya Jemima, rafiki yake wa kiume amekuwa

akimweleza kuwa, “meza dawa zako na uamini kuwa umepona!” Jemima anajiona ana uzima tele na anatarajia kuanzisha familia yake na kuwa na watoto wake mwenyewe. Wazazi na familia yake wameendelea kuwa msaada mkubwa kwake wakimtia moyo kutumia dawa pasipo kuacha.

Hata hivyo, kuna tatizo moja dogo kwa upande wa Jemima, ni kwamba upande wa wazazi wa rafiki yake wa kiume hawajampokea vizuri sana kwa sababu ya hali ya ngozi yake. Jemima akawa na wasiwasi kwamba iwapo hawafurahii hali ya ngozi yake, itakuwaje kuhusu ndoa, na je watachukua maamuzi gani pale watakapojua kuwa yeye ni mwathirika wa UKIMWI. Yeye na rafiki yake wa kiume wamekuwa wakijaribu kufikiri kuhusu wakati sahihi wa kueleza hali ya kiafya ya Jemima kwa familia ya rafiki yake wa kiume. Pamoja na haya yote, wao wote wawili wanaamini kuwa wao waili kuwa pamoja ni mpango wa Mungu.

Zoezi

Madhumuni ya zoezi: Baada ya kumaliza zoezi hili, washiriki watakuwa wamejihusisha na aina na makundi mbalimbali ya changamoto wanazopitia watoto wanaozaliwa na VVU na ambao sasa wamekuwa watu wazima katika jamii ambazo zinaendelea kuliona tatizo la VVU kama ni Kirusi kisichotibika.

Njia za kufundishia: vikundi vidogovidogo, majadiliano ya pamoja

Vifaa vya Kufundishia: bangokitita, kalamu za maka

Muda: dakika 20

Mwezeshaji atawagawa washiriki katika vikundi vidogovidogo vya watu wasiozidi sita na kuviruhusu vikundi hivyo kusoma simulizi ya Jemima na baadaye kuitafakari na kuijadili wakisaidiwa na mwongozo wa maswali na hoja zilizoorodheshwa hapa chini:

1. Je, ni mambo gani katika simulizi ya Jemima unayoyaona kuwa ni changamoto kubwa zaidi? Kwa nini?
2. Ukiangalia simulizi yake, je unadhani Jemima alipitia unyanyapaa mkubwa zaidi na kukataliwa kutoka kwa watu gani?
3. Je, ni watu gani ambao Jemima anawaona kama mashujaa? Ni mambo gani yanayowafanya waonekane kuwa ni wa kipekee?
4. Kuna wakati Jemima alikuwa akiugua mara kwa mara lakini sasa anaonekana kuwa na afya. Je amepona? Je wewe unalielewaje suala la kupona?

Victor kutoka Nigeria

Victor ni kijana kutoka Nigeria, ambaye amekulia mahali ambapo yeye anadhani lilikuwa ni eneo walipokuwepo wazazi wake katika makazi duni huko Lagos. Baba yake alikuwa na wake wengi na Victor anadhani kwamba yeye alikuwa mtoto pekee kwa wazazi wake, lakini mara nyingi Victor alikuwa akiitwa na baba yake kuwa ni mshenzi na kamwe hakuelewa ni kwa nini alikuwa akiitwa hivyo. Akiwa na umri wa miaka kumi, Victor alifukuzwa kutoka kwenye familia yake. Akaenda kuishi na baba yake mdogo ambaye alikuwa akimnyanyasa kingono. Alimpa taarifa hizo mama yake ambaye pia alimwarifu baba yake Victor ambaye hakuamini kama ni kweli mdogo wake alikuwa anamnyanyasa kingono mtoto wake. Baba yake Victor alishughulikia suala hili kwa kusababisha mama yake Victor akamatwe. Tabia ya kunyanyaswa kingono iliendelea kwa muda mrefu mpaka pale mama yake alipompeleka Victor kanisani, ambapo kwa mara ya kwanza alishuhudia uzoefu wa uponyaji dhidi ya huzuni na maumivu yaliyosabaishawa na kunyanyaswa kingono. Kanisa pia lilimsadia kuendelea kuwa thabiti na pia alikuwa na uwezo mzuri kiakili na hivyo kuendelea vizuri kimasomo na akachaguliwa kujiunga Chuo Kikuu.

Ilikuwa ni mpaka pale alipoingia Chuo Kikuu, ndipo hatimaye akaambiwa ukweli kuhusu maisha yake, hali, na utambulisho wake. Kumbe wale watu ambao yeye siku zote alifikiri kuwa ni wazazi wake wa kumzaa hawakuwa wazazi wake wa damu, mama yake mzazi ambaye alifariki wakati akijifungua alikuwa rafiki wa karibu wa mama yake wa sasa. Katika dakika za mwisho za uhai wake, alimuomba rafiki yake huyu amhakikishie kwamba atamtunza mtoto wake. Alikubali na hivyo ndivyo Victor alivyojikuta mikononi mwa mama yake wa sasa. Mama huyu alipokuwa amekutana na mume wake, mume alimwambia kuwa angemuoa iwapo tu angekuwa na mtoto mmoja na si wawili, ndipo akamweleza ukweli kwamba mtoto mwingine aliyekuwa naye hakuwa mtoto wake wa kumzaa bali alikuwa mtoto wa marehemu rafiki yake. Hivyo basi yule mtu akakubali kumuoa. Machoni pa mtu huyu, ambaye siku zote Victor amekua akidhani ndiye baba yake, Victor alionekana kama ni mshenzi, na hasa pale ambapo alikuwa amekosea jambo fulani. Hii pia ndio sababu baba huyu hakuwahi kumchukulia Victor kama mwanae halisi wa kumzaa.

Akiwa Chuo Kikuu, Victor alianzisha mahusiano ya kimapenzi na msichana kabla ya ndoa pasipo kutumia kondomu. Alipoenda kupima VVU, aligundulika kuwa alikuwa ameathirika. Hali hii ilimfanya kwa kiasi kikubwa apoteze hamu ya kufanya mapenzi. Hata hivyo alipomweleza rafiki yake wa kike yeye alimwambia hatamuacha kamwe, pengine ni kwa sababu yeye pia alijihisi kuwa alikuwa ameathirika. Wakaamua kwenda kupima VVU kwa pamoja na majibu yaliyokuja yaliwashangaza – Victor alikuwa ameathirika na VVU lakini rafiki yake wa kike hakuwa ameathirika. Siku chache baadaye, rafiki yake wa kike akapendekeza waanze maombi ya mlimani ya kufunga na kuomba kwa muda wa siku kumi na saba usiku na mchana, ambayo inge-

maanisha Victor aachane na dawa zake lakini yeye alikataa. Rafiki yake wa kike akaamua kuachana na Victor. Kwa muda fulani, Victor alikuwa akihangaika kuhusu namna atakavyoweza kuwaeleza familia yake, lakini hatimaye alimwambia mdogo wake wa kike ambaye alionesha msaada na ushirikiano mkubwa na akawaeleza familia. Badala ya kukataa, familia yake ilimpokea na kumkubali na kumuonesha upendo mkubwa. Jambo hili lilichangia sana katika kuleta uponyaji kwa Victor.

Baada ya kugundua kuwa vijana wengi walikuwa hawana ufahamu na hawajui ukweli kuhusu VVU, Victor aliamua kujiingiza katika masuala ya uhamasishaji. Baba yake hakufurahishwa sana na hili na akamtaka Victor asiwe anatumia jina la familia yao kwa kuogopa kuchafuliwa na kunyanyapaliwa. Ni mpaka pale Victor alipoanza kusafiri nje ya nchi ndipo baba yake alimruhusu aanze kutumia jina la familia.

Mara zote Victor alikuwa mshiriki mzuri wa kanisa. Bahati mbaya mchungaji wake akaanza kuwanyanyapaa watu wengine wanaoishi na VVU na hivyo kumfanya Victor aache kwenda kanisani. Alipogundua madhara ambayo yangetokea iwapo kanisa lingearifiwa na mchungaji kuhusu hali yake, Victor aliamua kujitangaza hali yake mbele ya mchungaji na hii ikawafanya hata watu wengine ndani ya kanisa waliokuwa wanaishi na VVU kutangaza hali zao za afya pia. Hali hii ikabadili kanisa na kulifanya liwe sehemu salama na kimbilio.

Victor anasema, “Nipo hai kwa sababu natumia vidonge vyangu kwa uaminifu kabisa. Hii ndio sababu ya muujiza wangu!” Victor ni mtu mwenye nguvu na kijana mchangamfu, mwenye kuonesha ishara za kupona huku bado akiendelea namatibabu.

Zoezi

Madhumuni ya zoezi: Baada ya kumaliza zoezi hili, washiriki watakuwa wameweza kujihusiaha na mambo mbalimbali aliyoyapitia Victor, ambayo yatawasaidia kupambana na VVU na UKIMWI na visababishi vinavyochochea ugonjwa huu.

Njia za Kufundishia: vikundi vidogovidogo, majadiliano ya pamoja

Vifaa vya Kufundishia: bangokitita, kalamu za maka

Muda: dakika 20

Mwezeshaji atawagawa washiriki katika vikundi vidogovidogo vya watu wasiozidi sita na ataviongoza vikundi hivyo kusoma simulizi ya Victor na kuitafakari na kuijadili kwa kuongozwa na maswali na hoja zilizoorodheshwa hapa chini:

1. Orodhesha mambo yaliyochangia Victor kuambukizwa VVU.
2. Je, wenza wasioendana (discordant couple) humaanisha nini ?
3. Onesha hatua mbalimbali katika maisha ya Victor ambako alishuhudia uponyaji.
4. Kwa kutumia uzoefu wa Victor, Je uponyaji ni nini?

Zoezi

Madhumuni ya zoezi: Baada ya kumaliza zoezi hili, washiriki watakuwa wamejaribu kutoa maana na kuweza kutofautisha matibabu na uponyaji.

Njia za kufundishia: vikundi vidogovidogo, majadiliano ya pamoja

Vifaa vya kufundishia: bangokitita, kalamu za maka

Muda: dakika 30

Mwezeshaji atawagawa washiriki katika vikundi vidogovidogo vya watu wasiozidi sita na kuviongoza vikundi hivyo kutafakari simulizi walizozisoma wakizingatia zaidi aina mbili za tiba zinazohusiana na matumizi ya dawa za kupambana na virusi na uponyaji. Mwezeshaji aweke mkazo zaidi kwenye hoja zilizoorodheshwa hapa chini wakati atakapokuwa anagawa makundi:

- Katika simulizi zote nne, wahusika wanaonekana kuonesha tofauti kati ya matibabu na uponyaji.
- Simulizi hizo zinaonesha pia kwamba si mara zote uponyaji humaanisha ni mwisho wa matibabu au kuachana na visababishi vya ugonjwa.
- Simulizi hizi pia zinaashiria kwamba uponyaji unaweza kufanikiwa kupitia mchanganyiko wa mambo.
- Simulizi zinaashiria pia kuwa matibabu na uzingatiaji wa ushauri wa wataalamu ni miongoni mwa mambo makubwa yanayoweza kufanikisha uponyaji lakini hilo si jambo pekee.

Baada ya kuwaeleza mambo hayo hapo juu, mwezeshaji anaweza kuwagawa washiriki ili wafanyie kazi maswali na hoja zilizoorodheshwa katika vikundi vyao vidogovidogo:

1. Kwa kuzingatia masimulizi haya, je, unadhani mambo gani ni muhimu ili kufanikisha uponyaji hata kama mtu huyo amegundulika kuwa ameathirika na VVU?
2. Kwa kuzingatia masimulizi hayo, je, ni tofauti gani zilizopo kati ya kutibiwa na kuponywa? Je, unadhani dawa za kupambana na virusi zinamsaidia mtu kutibiwa au kuponywa?
3. Kwa kuzingatia masimulizi haya, je, unadhani kuna ujumbe upi ambao viongozi wa dini wanapaswa kuwapa watu wanaoishi na VVU?
4. Je, unadhani dawa za kupambana na virusi ni muujiza toka kwa Mungu? Je, watu wanaoishi na VVU waendelee kutarajia tiba ya kimiujiza, kama inavyoahidiwa na baadhi ya manabii?

SOMO LA 6

Kuelewa Uponyaji kwa Imani na Tiba kwa Imani

"Bwana, usinikemee kwa hasira yako, Wala usinirudi kwa ghadhabu yako. Bwana, unifadhili, maana ninanyauka; Bwana, uniponye, mifupa yangu imefadhaika. Na nafsi yangu imefadhaika sana; Na Wewe, Bwana, hata lini? Bwana urudi, uniopoe nafsi yangu, Uniokoe kwa ajili ya fadhili zako." (Zab 6:1-4)

Madhumuni ya somo

Mwishoni wa somo hili, washiriki watakuwa wameelewa tofauti zilizopo kati ya uponyaji kwa imani na tiba/matibabu kwa imani katika muktadha wa VVU na ugonjwa wa UKIMWI.

Usuli

- Maendeleo ya teknolojia yaliyotokea katika karne iliyopita yamesababisha kubadilika kwa mwelekeo wa matumizi ya dawa kutoka mtazamo wa kujali, au mwelekeo wa kihuduma na kuingia katika mwelekeo wa kiteknolojia, na kuwa katika modeli ya kutibu.
- Ipo tofauti kati ya uponyaji na kutibu. Uponyaji ni mchakato wa asili unaohusiana na imani na umo katika uwezo wa kila mtu. Kutibu na kuudhibiti ugonjwa, ndilo jambo ambalo madaktari hufanya. Kwa kawaida hili linahusisha matibabu ya nje; inaweza ikawa matibabu ya dawa au upasuaji ambavyo hutumika kufunika au kuondoa kabisa dalili za ugonjwa. Kwa upande wa VVU, dawa sio tiba kamili, bali ni njia mojawapo ya kuondoa dalili za ugonjwa, kurefusha maisha, kuongeza ubora wa maisha, na kuondoa uwezekano wa kuambukiza VVU kwa mwenza kupitia ngono.
- Uponyaji unakwenda ndani zaidi kuliko kutibu na hutokea ndani ya mtu. Unahusika na kushughulikia mapungufu yanayotokana na dalili za magonjwa. Uponyaji huleta pamoja mambo ambayo mara nyingi huwa yamefichika katika maisha ya mtu lakini yanayohusiana na ugonjwa. Uponyaji ni tofauti na kutibu, ingawaje kutibu na kurejesha upya kazi za mwili vinaweza kuendana na uponyaji.
- Tunaweza tukawa tumeponywa pasipo kutibiwa. Kutotibiwa hakuondoshi uwezekano wa mtu kuponywa.
- Tunatambua kuwa lugha nyingi za kiasili na hata katika Biblia, hazitofautishi kati ya uponyaji na kutibiwa. Kutokana na kutambua hilo, mwongozo

huu haupingani na kuponywa kwa imani kwa ujumla isipokuwa *madai*ya uponyaji wa matatizo kama vile VVU kwa imani pekee. Madai ya aina hiyo yanaweza kueleweka kama madai ya kutibu VVU kwa imani.

Uponyaji kwa Imani au Kutibu kwa imani? ". . . Basi Yesu, Akamkaribia, akamwinua kwa kumshika mkono, homa ikamwacha, akawatumikia." (Marko 1:29-31)

- Dhana au uelewa kwamba maombi, uingiliaji kati wa Mungu, au huduma ya mtu fulani anayeponya vinaweza kutibu ugonjwa imekuwa ni moja kati ya mambo yaliyotawala kwa muda mrefu sasa. Kupona kwa miujiza kumehusishwa na mbinu nyingi ambazo kwa pamoja huitwa "uponyaji kwa imani."
- Baadhi ya watu wamekuwa wakitafsiri Biblia, na hasa Agano Jipya, kuwa ni maalum kwa ajili ya kufundisha imani katika, na matendo ya, uponyaji kimuujiza. Yamekuwepo madai kwamba imani inaweza kutibu upofu, uziwi, kansa, VVU na UKIMWI, kudumaa, upungufu wa damu, baridi yabisi, shida ya kuongea, shida ya uti wa mgongo na neva, vipele kwenye ngozi, kupooza na maumivu mengine mengi. Madai ya aina hii moja kwa moja yanahusika na madai ya "kutibu kwa imani."
- Neno kuponywa kwa imani linamaanisha uwezo wa imani kusaidia katika kurejesha uwezo wa kujimudu kwa mtu kukabiliana na matatizo ya kisaikolojia, kibiolojia, kijamii, kiuchumi na kiroho ambayo yangeondoa hali ya kujimudu kwa mwanadamu. Kuponywa kwa imani ni jambo kamilifu ambalo hukamilishwa na matibabu yanayotolewa na madaktari wa magonjwa ya mwili au wataalamu wa akili.
- Madai ya uponyaji kwa imani au kutibu kwa imani pekee yanamaanisha uwezo wa imani kuondosha kabisa magonjwa pamoja na visababishi vyake, kimwili, kibiolojia na kiakili. Kutibu kwa imani kuna jitanabaisha kuwa ni njia mbadala wa njia zilizopo za kushughulika na magonjwa ya akili na mengineyo kwa kutumia dawa. Kutibu kwa imani pia kunajitanabaisha kama ni njia yenye kushindana na watoa huduma za dawa na matibabu ya hospitalini.
- Tukiwa katikati ya zama za uwepo wa ongezeko kubwa la ripoti za "kutibu kwa imani" kwa nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, ambapo watu wanaoishi na VVU na UKIMWI wamekuwa wakiambiwa na viongozi wao wa dini kuwa wamepata tiba ya VVU na UKIMWI, tumeshuhudia ongezeko kubwa la maradhi na vifo. Watu ambao wanaambiwa waachane na matibabu ya hospitali wanaendelea kuwa wagonjwa na wanakufa.
- Kuwepo kwa matukio mengi ya watu kufa kwa kuwa tu wameshindwa kuzingatia matibabu kwa ajili ya kuamini madai ya kutibu kwa imani pekee kunamaanisha kwamba ni lazima tusimame na kutetea uponyaji kwa imani mbao unajikita katika kuleta njia inayokamilisha aina nyingine za uponyaji

zilizopo na si kusimamia madai ya uponyaji kwa imani pekee. Uponyaji kwa imani ni njia ya uponyaji mkamilifu wa VVU na UKIMWI, ambayo huhimiza matumizi ya njia zote mbili, maombi pamoja na uzingatiaji wa dawa.

Maana ya Kiteolojia ya Uponyaji kwa Imani

- Neno uponyaji ni tofauti na neno kutibu/matibabu. Uponyaji unamaanisha kujenga upya hali ya kujimudu kwa mwili, roho na nafsi. Uponyaji unahusiana na maisha yetu kwa ujumla kama wana wa Mungu. Kutibu majeraha na homa vinaweza kuwa ni sehemu ya uponyaji, lakini ni sehemu ndogo *tu*. Hivyo basi, kutibu si sawa na kuponywa.
- Injili huhusiana na suala la uponyaji. Ingawa injili hujumuisha mambo yote mawili, matibabu na uponyaji. Kwa mfano mama mkwe wa Simon wa Petro alikuwa na homa, na Yesu akamponya (Mt 8:14-15). Hakurejeshwa tu katika hali yake ya kawaida; bali alirejeshwa katika hali ya ushirika na uwepo katika huduma ya Yesu. Akawa ni sehemu ya Habari Njema, sehemu ya injili, Sehemu ya wanajumuiya ya watu wa Mungu. Huo ndio Uponyaji.
- Tunashuhudia kwamba Yesu alipokuwa akipita Galilaya, alitumia muda mwingi kuwatibu wagonjwa, lakini pia alitumia muda mwingi kuombea na kuhubiri na kuzungumza pia. Hii ni kwa sababu kutibu watu ni sehemu moja tu kati ya mambo mengi. Yesu hataki tu homa iondoke na miguu iliovunjika ipone – anataka kufanya zaidi ya hapo. Anataka kutuponya. Si tu kama mtu mmoja mmoja, bali kama jamii na ulimwengu. Anataka tuwe *wazima*. Anataka pia tuhuishwe upya.
- Wakati mwingine, uponyaji humaanisha kujifunza kuishi na yale mambo yasiyoweza kutibika. Na mara nyingine, uponyaji unaweza kumaanisha kukubaliana na mambo *yasiyoweza* kurekebishika, na kukubali kwamba hata hivyo wewe ni mtoto mpendwa wa Mungu. Hii inamaanisha kuna wakati inabidi ufike tuseme “Nenda nyuma yangu Shetani,” kwa wale wote wanaotoa ahadi za kutibu mambo ambayo hayawezi kutibika, bali yanaweza kuponyeka.

Zoezi la 1

Madhumuni ya zoezi: Kufikia mwisho wa zoezi hili, washiriki watakuwa wameweza kutofautisha kati ya kuponywa kwa imani na kutibu/matibabu.

Njia za kufundishia: vikundi vidogovidogo, majadiliano ya pamoja

Vifaa vya kufundishia: bangokitita, kalamu za maka

Muda: dakika 20

Mwezeshaji atawagawa washiriki katika vikundi vidogo vidogo vya watu wasiozidi sita na kuviongoza vikundi hivyo kutafakari tofauti zilizopo kati ya uponyaji kwa imani na madai ya kutibu/matibabu.

1. Je, uponyaji kwa imani ni nini? Ni maeneo gani katika maisha ya mwanadamu yanaweza kufaidika kutokana na uponyaji kwa imani?
2. Je, imani pasipo dawa inaweza kuponya VVU na UKIMWI?
3. Je, unaweza kumwambia nini kiongozi wa dini ambaye atakwambia, ana uwezo wa kukuponya VVU na UKIMWI?

Umuhimu wa Uponyaji kwa Imani na Tiba kwa Imani katika Muktadha wa VVU na UKIMWI

Imani huponya, ila dawa hutibu, wakati mwingine, inakuwa yote ni kwa ajili ya utukufu wa Mungu bila ya kujali yale ambayo watu wanaweza kuamini na kufundisha. Je, Biblia inatueleza chochote kuhusu matumizi ya dawa? Je, kuna mahali kwenye Biblia pananasema ni dhambi kutumia dawa au kwamba kutumia dawa inaonesha uhaba wa imani?

Ili kuanza mapitio yetu, hebu tuangalie kitabu cha **Mwanzo 37:25** panapozungumzia Waishmaeli kufanya biashara na "zeri." ¿Je neno "zeri" lina maanisha nini? Ni nini hii na namna gani linatumika? Kitabu cha **Kutoka 30:34–35** kinatoa sehemu ya jibu.

Mwanzoni tulisoma malalamiko ya Yeremia katika kitabu cha **Yeremia 8:22**: "Je hapana zeri katika gileadi? Huko hakuna tabibu? Mbona, basi, haijarejea afya ya binti ya watu wangu?"

Yeremia 46:11, inasema: "Panda uende Gileadi, ukatwae *zeri*, Ee binti, bikira wa Misri; unatumia dawa nyingi bure tu; hupati kupona kamwe.

Ili kuthibitisha jambo hilo, angalia **Yeremia 51:8–9**: "Babeli umeanguka na kuangamia ghafla; mpigieni yowe; twaeni zeri kwa maumivu yake; ili labda apate kuponywa."

Ni wazi kutokana na mifano ya kibiblia hapo juu (japo ni michache) kwamba uponyaji kwa imani hauwi mbadala wa matibabu ya hospitali kama njia kamilifu ya kuwa na ustawi kwa yeyote. Hivyo basi, ni muhimu kwa watu wanaoishi na VVU kuhamasishwa ili watumie dawa zao kwa uaminifu pamoja na kufanya maombi. Njia kamilifu ya aina hii itasaidia kuleta uponyaji mkamilifu, hata pale ambapo imeshindikana kupona.

Zoezi la 2

Madhumuni ya zoezi: Ifikapo mwisho wa zoezi hili, washiriki watakuwa wameelewa hali ya kutegemeana iliyopo kati ya kuponywa kwa imani na matibabu ya daktari.

Njia za kufundishia: vikundi vidogovidogo, majadiliano ya pamoja

Vifaa vya kufundishia: bangokitita, kalamu za maka

Muda: dakika 40

Mwezeshaji atawagawa washiriki katika vikundi vidogovidogo vya watu wasiozidi sita na kuviongoza vikundi hivyo kusoma maandiko yaliyotajwa hapo juu kuyatafakari, na kuyajadili kwa kuongozwa na maswali yafuatayo:

1. Je, kuna mahali popote kwenye Biblia panatuhumu uponyaji/matibabu au tiba ya dawa za hospitali?
2. Toa mifano ya "zeri" zilizoko katika mazingira yako, yaweza kuwa ama zile za kienyeji au zile za kutoka nchi za Magharibi//zilizoagizwa toka nje?
3. Je, kuzingatia matibabu ni dalili ya mtu kukosa imani au alama ya imani katika uwezo ambao madaktari wamepewa na Mungu?
4. Je, serikali au nchi yako inaelewa chochote kuhusiana na suala la uponyaji kwa imani pekee? Je, wanafanyia kazi suala hilo sasa?
5. Je, kwa kuzingatia uelewa wako wa somo hili, unaweza kuishauri nini serikali kuhusu watu wanaohubiri (makanisani, kwenye runinga, kupitia maandishi ya kawaida na yale ya kieletroniki) wakipinga uzingatiaji wa matibabu kwa washiriki wao walioathirika na VVU?

SOMO LA 7

Dawa za Kupambana na Virusi ni Muujiza wa Mungu

"Akasema, 'Mtoto alipokuwa hai, nalifunga, nikalia; kwa maana nalisema, Ni nani ajuaye kwamba Bwana atanihurumia, mtoto apate kuishi?'"
(2 Sam 12:22)

Madhumuni ya somo

Kufikia mwisho wa somo hili, washiriki watakuwa wametambua na kuukubali umuhimu wa kiteolojia wa dawa za kupambana na virusi katika muktadha wa VVU.

Usuli

Muda ambapo tiba hii imekuja na matokeo ya matumizi ya dawa za kupambana na virusi ni kigezo tosha kuifanya iitwe "Muujiza wa Mungu."

- Kuna mtindo umezuka hivi karibuni ambapo baadhi ya viongozi wa dini wamekuwa wakiwahamasisha watu wanaoishi na VVU kutotumia dawa za kupambana na virusi. Wamekuwa wakidai kuwa dawa za kupambana na virusi "Haitoki kwa Mungu," au kwamba "imegunduliwa na wanasayansi wa kidunia."
- Mahala pengine, kumekuwa na madai kwamba kuachana na matumizi ya dawa za kupambana na virusi ni dalili inayothibitisha kwamba mtu ana "imani kamilifu" kwa Mungu. Kwa mtazamo huo, kutotumia dawa za kupambana na virusi ni udhihirisho au uthibitisho wa imani kwa Mungu.
- Tabia ya kupambanisha uponyaji wa kiimani na dawa za kupambana na virusi kwa kuziweka katika pande mbili zinazopingana katika mizani imesababibisha vifo vingi visivyo vya lazima katika maeneo yetu. Kwingineko, tabia hii imesababisha watu kugomea matumizi ya dawa na kusababisha miili kuwa sugu na kutotibika.

Hebu Tusisahau: Idadi ya Vifo vyenye kuhusiana na UKIMWI Kabla ya Ugunduzi wa Dawa za Kupambana na Virusi

Katika miaka ya 1990 kulikuwa na idadi kubwa ya vifo vilivyotokana na UKIMWI. Familia na jamii nyingi barani Afrika ziliteketea tokana na UKIMWI. Hali hii ilisababisha hofu kubwa kutawala, na kuona kuwa ukigundulika kuwa ni mwathirika wa VVU basi ni sawa na kupewa "hukumu ya kifo." Kwa sababu ya ukosefu wa dawa za kupambana na virusi, watu wengi walicheza "mchezo wa kusubiri," ambao matokeo yake yalikuwa "kupatwa" na mauti. Wakati huo, kulikuwa na vifo vingi vilivyotokana na UKIMWI katika nchi nyingi za kusini na mashariki mwa Afrika hadi baadhi ya viongozi wa maeneo ya mijini wakaanza kuzungumzia uhaba wa maeneo ya kuzikia. Hii ikasababisha ongezeko kubwa la watoto yatima na watoto kuachwa katika mazingira magumu. Bado madhara ya kushindwa kupata dawa za kupambana na virusi kwa wakati yanaendelea kuonekana katika nchi nyingi za Afrika leo. Katika siku hizi pia wachungaji wamekuwa wakiomba kwa ajili ya uponyaji lakini hatusikii miujiza ikimtibu kila mwenye VVU – bila matibabu anakufa.

Zoezi

Madhumuni ya somo: Mwishoni mwa zoezi hili, washiriki watakuwa wametambua kwa undani matokeo chanya ya kutumia dawa za kupambana na virusi katika kukabiliana na VVU na UKIMWI. Washiriki watakuwa wametafakari namna ambavyo UKIMWI ungeangamiza jamii na mataifa mengi na namna ambavyo uwepo wa dawa za kuokoa maisha kumesaidia kuleta matokeo chanya ya kiafya kwa watu binafsi, familia, jamii pamoja na taifa kwa ujumla.

Njia za kufundishia: vikundi vidogovidogo, majadiliano ya pamoja

Vifaa vya kufundishia: bangokitita, kalamu za maka

Muda: dakika 30

Mwezeshaji atawagawa washiriki katika vikundi vidogovidogo visivyosidi watu sita na kuviongoza vikundi hivyo kutafakari hali ilivyokuwa kipindi kabla ya ugunduzi wa dawa za kupambana na virusi, kwa kutumia maswali yaliyoorodhesshwa hapa chini kama mwongozo.

Washiriki wenye umri mdogo wasaidiwe kwa kuwapa takwimu za vifo vilivyosababishwa na UKIMWI tokea siku za nyuma. Takwimu za nchi zinaweza kufaa zaidi kuliko za dunia nzima.

Ni muhimu pia mwezeshaji akajua kwamba zoezi hili linaweza kuibua hisia kali kwa baadhi ya washiriki. Hivyo basi ni muhimu mwezeshaji akajiandaa kukabiliana na hilo, kwa mfano anaweza kumuweka tayari mtaalamu wa ushauri nasaha ili atoe huduma.

1. Je, ni madhara gani yalikuwepo kwenye jamii yako tokana na kutokuwepo kwa dawa za kupambana na virusi?
2. Nini maoni yako kuhusu madhara yatokanayo na idadi kubwa ya vifo vitokanayo na UKIMWI katika jamii yako (kama yapo) na ambayo chanzo chake kikubwa ni matendo yaliyotawala katika jamii yako.
3. Je, unajisikiaje kuhusiana na watu (ikiwa ni pamoja na ndugu, marafiki, majirani na wengineo) ambao wamekufa kwa sababu tu walikosa dawa za kupambana na virusi?
4. Tafakari kuhusu hali ambavyo ingekuwa leo iwapo kiwango cha vifo vitokanavyo na UKIMWI isingebadilika (au kama idadi ya vifo ingeongezeka).

Matokeo ya Lazaro: Dawa za Kupambana na Virusi na Urejeshaji wa Uhai

Miongoni mwa simulizi zinazosisimua sana katika Biblia ni ile inayohusu kufufuliwa kwa Lazaro (Yoh 11:1-44). Simulizi hii imekuwa ndiyo kiini cha baadhi ya nyimbo maarufu zenye kuhadithia muujiza wa kufufuka kwa Lazaro. Lazaro, ambaye alipoteza uhai, anarejeshwa na Yesu katika uhai. Katika muktadha wa VVU na UKIMWI, kuna kila sababu ya kutambua matokeo ya kimuujiza ya tiba ya dawa ya kupambana na virusi. Watu wengi ambao walikuwa wanakaribia kufa wanarudi uzimani kutokana na matumizi ya dawa ya kupambana na virusi. Watu ambao miili yao ilikuwa imeathirika kwa VVU na UKIMWI wamejikuta miili yao ikirejeshwa upya kwa kutumia dawa ya kupambana na virusi. Vifo vingi ambavyo vilikuwa vimeenea katika jamii vimezuiwa kwa kutumia dawa ya kupambana na virusi. Wakati ule madaktari, walipovumbua na kuanzisha tiba ya ART ulikuwa ni wakati wa furaha sana na jamii nyingine ziliuita uvumbuzi huu kama matokeo ya Lazaro.

Zoezi

Madhumuni ya zoezi: Hadi mwisho wa zoezi hili, washiriki watakuwa wametafakari matokeo ya matumizi ya dawa za kupambana na virusi katika maisha ya watu wanaoishi na VVU, kwenye familia zao, jamii, na nchi zao. Kwa umahususi, watakuwa wameelewa ukweli kwamba kwa kiasi kikubwa tatizo la VVU linatatulika, na kuwasaidia watu wanaoishi na VVU kuishi maisha ya kawaida, wakizaa watoto pasipo kuwaambukiza VVU wenza wao au watoto wao na wanaendelea kuwa na nguvu za kufanya kazi za uzalishaji.

Njia za kufundishia: vikundi vidogovidogo, majadiliano ya pamoja

Vifaa vya kufundishia: bangokitita, kalamu za maka

Muda: dakika 30

Mwezeshaji atawagawa washiriki katika vikundi vya watu wasiozidi sita na kuvisaidia vikundi hivyo kutafakari matokeo ya kutumia dawa za kupambana na virusi katika maisha ya watu wanaoishi na VVU, familia zao, jamii na nchi zao kwa kutumia mwongozo wa maswali yaliyopo hapa chini. Kama upo wimbo ambao unatoka katika simulizi ya Lazaro, basi washiriki wanaweza kuuimba wakati wa majadiliano ya kundi zima.

1. Je, ni kwa namna gani upatikanaji wa dawa za kupambana na virusi umebadilisha maisha ya watu wanaoishi na VVU?
2. Toa maoni yako kuhusu madhara ya kiafya na kiuchumi ya kutumia dawa za kupambana na virusi. (ukizingatia pia watu wanaotumia dawa za kupambna na virusi wanaweza kupata mimba na kujifungua pasipo kumwambukiza mtoto VVU kwa kufuata ushauri sahihi wa madaktari).
3. Je, ni kwa kiwango gani dawa ya kupambana na virusi inapatikana katika jamii yako? Iwapo haipatikani sana, pendekeza mambo yanayoweza kusaidia upatikanaji wake.
4. Je, ni matokeo gani yamekuwepo kutokana na uwepo wa uponyaji kwa imani kwa watu wanaoishi na VVU katika jamii yako?
5. Je, ni mambo gani katika jamii yako ambayo unaona kuwa yanatokana na unyanyapaa na ubaguzi kwa watu wanaoishi na VVU (na wale walioathirika na VVU na UKIMWI) katika jamii yako?

"Miujiza ya Mungu ipo Katika Namna Nyingi": Dawa ya Kupambana na Virusi kama Muujiza wa Mungu

Wapo baadhi ya viongozi wa dini (wanaotoka katika dini za jadi za kiafrika, wakristo, waislam, au wanaotoka kwenye dini nyinginezo) wamedhoofisha uzingatiaji wa matibabu kwa madai kwamba uponyaji wa kiimani pekee ndio uponyaji wa Mungu. Wakati mwingine viongozi hao hudai kwamba kuacha kutumia au kutokuanza matumizi ya dawa za kupambana na virusi na kutegemea imani pekee ni ushahidi kwamba wewe unamtegemea Mungu kikamilifu. Kwa bahati mbaya hali hiyo imesababisha vifo vingi visivyo vya lazima, ugumu wa matibabu na mtazamo hasi wa matumizi ya dawa za kupambana na virusi. Jambo hili limekuwa kama janga, hasa ukizingatia kwamba waafrika wengi walishirikishwa katika juhudi za awali za kupatikana kwa dawa za kupambana na virusi. Je, ni kwa nini sasa baadhi ya viongozi wa dini wanawashawishi watu wasitumie dawa za kupambana na virusi, na wakati zinapatikana kwa wingi zaidi na zinaokoa maisha?

Madhumuni ya zoezi: Hadi mwisho wa zoezi hili, washiriki watakuwa wamethamini mtazamo kwamba dawa ya kupambana na virusi inaweza ikakubalika kama muujiza utokao kwa Mungu. Kwa maana hiyo, katika muktadha wa VVU na UKIMWI, uponyaji wa kiimani si aina pekee inayoonyesha uingiliaji kati wa Mungu.

Njia za kufundishia: usomaji wa biblia kwa kuzingati muktadha wake[3]

Vifaa vya kufundishia: biblia, bangokitita, kalamu za maka

Muda: dakika 45

Wasomee washiriki wote 2 Wafalme 5:1-15. Kisha wagawe washiriki katika makundi ya si zaidi ya washiriki sita na yaruhusu makundi kutafakari fungu hilo, kwa kutumia maswali haya hapa chini kama miongozo.

Simulizi hii inajumuisha watu wakuu sana kama vile Naamani, jemadari wa jeshi la mfalme wa Shamu; mfalme wa Shamu; na mfalme wa Israeli. Hata hivyo, si watu hodari, bali watu wanyenyekevu, na hasa yule msichana mdogo, ambaye alikuwa ni msaada sana katika kuleta uponyaji wa Naamani. Hawa ni watu wa muhimu pia katika kumfanya Naamani apate uelewa mpya wa uponyaji. Nabii wa Mungu Elisha alikuja na aina mpya ya uponyaji ambayo Naamani hakuwa anaitarajia. Naamani alikuwa anatarajia aina ya uponyaji ambayo ni ya ajabu, lakini Mungu akatoa njia rahisi ya kivitendo lakini yenye uwezo mkubwa wa kuponya.

- Mwezeshaji anatakiwa kukazia kwamba ugunduzi wa tiba ya dawa za kupambana na virusi umesaidia kuondoa "hukumu ya kifo" ambayo siku za nyuma ilikuwa ikihusiana na VVU na UKIMWI. Upo uwezekano wa watu kurejea kwenye afya njema, kupitia maombi na matibabu, wakati ambapo VVU hubaki kwenye miili yetu.

Uponyaji ni tofauti na tiba. Hadi leo hakuna tiba ya VVU inayojulikana. Hata hivyo miujiza ya Mungu inatokea kwa watu tofauti tofauti kwa njia tofauti. Tunaomba Mungu awasaidie madaktari ili waweze kupata njia ya kutibu maambukizi ya VVU. Dawa ya kupambana na virusi ni njia ya kimiujiza aliyoitoa Mungu, ambayo sasa inapatikana kwa mamilioni ya watu (hadi asilimia 70% katika nchi za Afrika zilizo kusini mwa jangwa sahara)[4]. Uponyaji wa kila aina hutoka kwa Mungu, na ni Mungu huyo huyo ambaye husaidia vumbuzi zote za kisayansi, ni Mungu ndiye huleta uponyaji wa kiroho.

1. Je, ni uponyaji wa aina gani ambao Naamani alikuwa akiutarajia toka kwa nabii Elisha? Ni kwa nini mwanzoni Naamani alikuwa anasita kufuata ushauri wa Elisha?

3. https://www.tearfund.org/Sites/TILZ/Resources/Publications/Footsteps/Footsteps_91-100/Footsteps_98/Bible_study_Healing_and_antiretroviral_therapy_ART

4. Taarifa mbalimbali (Factsheets) kutoka shirika la UKIMWI duniani (UNAIDS) June 2017

2. Je, Naamani alisaidiwaje na watumishi wake?
3. Je, unadhani katika simulizi ulizosoma miongoni mwetu kuna watu wanaofanana na wahusika wa kwenye simulizi hii? Je, kuna watu miongoni mwetu ambao huwatia moyo au kuwashawishi watu kwenda kupima na kupata matibabu? Je, ni watu gani huwasaidia wengine kuendelea kutumia dawa zao za kupambana na virusi?
4. Je, ni aina gani ya matibabu na uponyaji ambao Mungu ametoa kwa wale wote ambao tunaishi na VVU? Kwa nini unafikiri ni muhimu kwetu kundelea na matibabu pamoja na maombi hata kama tumeanza kujisikia vizuri?
5. Je, ni mambo gani ambayo sisi kama viongozi wa dini tunapaswa kuyafanya ili kukuza kiwango cha afya na uponyaji kwa sisi tunaoishi na VVU?

SOMO LA 8

Je, ni Nani Mwenye Uhitaji wa Uponyaji? Teolojia ya Kufuatana nao

"Na Petro alikuwa akiyafikiri yale maono. Roho akamwambia, 'Wako watu watatu wanakutafuta. Basi ondoka ushuke ufuatane nao, usione tashwishi, kwa maana ni mimi niliyewatuma.'" (Matendo 10:19-20)

Madhumuni ya somo

Hadi mwisho wa somo hili, washiriki watakuwa wameweza kujihusisha na ukweli kuhusu madhara mbalimbali yatokanayo na VVU na UKIMWI kwa watu tofautitofauti ili kuja na njia na mkakati toshelevu wa kusaidia kuleta uponyaji kamilifu wa VVU na UKIMWI.

Usuli

- Sote tunafahamu kwamba kuna watu wanaoishi na VVU. Miaka michache iliyopita wengi miongoni mwao wangeshuhudia hali zao kubadilika na kuwa UKIMWI. Hata hivyo kutokana na uwepo wa dawa za kupambna na virusi, idadi kubwa ya watu wanaoishi na VVU wanaishi maisha ya kawaida ya afya. Ijapokuwa tunafahamu kwamba mara virusi vinapoingia mwilini mwa mtu, huwa haviondoki, hata kama ukifanikiwa kuvidhoofisha. Kwa kawaida wengi wetu tunadhani hao ndio watu pekee ambao wanahitaji uponyaji.
- Tunafahamu pia kwamba watu wanaoishi na VVU ni sehemu ya familia, sehemu ya jamii na sehemu ya nchi zao. Hali zao za ugonjwa zinaathiri jamii hizi katika namna tofauti tofauti. Je, unadhani jamii hizi pamoja na watu wanaoishi na VVU wanahitaji uponyaji pia?
- Kwa upande fulani familia huwa zinaathiriwa pia kwa sababu hushuhudia watu wao wanaoishi na virusi vya UKIMWI wanavyoteseka kwa kuwa virusi hukataa kuachia mifumo yao ya kinga. Mara nyingine wanafamilia hulazimika kufuatana na ndugu zao kwenda kliniki na hospitalini kwa ajili ya kupima afya na kupata matibabu. Wanakuwa ni mashuhuda na mara nyingi, wao ndio huwasaidia ndugu zao kuzingatia matibabu yao. Na pale ambapo mmojawapo anapougua, familia zao ndizo huwa na jukumu la kuwahudumia wakiwa nyumbani.
- Hata jumuiya za kiimani pia zinakumbana na changamoto ambazo zinazotokana na VVU. Katika miaka ya hivi karibuni jumuiya za kiimani zimejulikana sana kwa kushirikiana na watu wenye afya na hata wagonjwa.

Wakati mwingine jumuiya za kiimani zimekuwa zikiwatunza watu ambao wameathirika au kuathiriwa. Ndani ya jumuiya za kiimani wapo pia wataalam mbalimbali kama vile manesi, madaktari, washauri nasaha na wengine wengi ambao mara nyingi utalaamu wao hutumika na wanajamii katika kuwatunza waathirika na walioathiriwa wa UKIMWI.

- Taasisi za afya ambazo ni pamoja na serikali au jumuiya na mashirika ya dini, yanashirikishwa sana katika kuwatunza na kuwatibu watu wanaoishi na VVU na UKIMWI. Madakari, wauguzi na makasisi wanalo jukumu kubwa sana katika kuzisaidia taasisi nyingine kama vile, kliniki na mahospitai, na hii ni sehemu muhimu ya kuwahudumia na kutoa matibabu kwa watu wanaoishi na VVU na UKIMWI.
- Viongozi wa dini ambao huongoza jumuiya za kidini mara nyingine hufanya kazi za ziada kama makasisi kwenye kliniki na mahospitalini. Hawa pia wanalo jukumu kubwa katika kuhakikisha wanatoa matibabu na kuwahudumia watu wanaoishi na VVU na UKIMWI. Maneno wanayotamka yanaweza kuwa ni chanzo cha uzima lakini pia yanaweza kuwa ni ya kuwaua wale ambao bado wanaishi.
- Hoja zilizotolewa hapo juu, zinaonesha wazi kwamba watu wanaoishi na VVU, na wale ambao wameathiriwa na VVU wote wanahitaji uponyaji. Ili kufanikisha hilo tunahitaji kuongozwa na ufahamu wetu wa kuuona uponyaji kuwa ni kitu tofauti na kutibu au matibabu. Uponyaji una maana pana zaidi, unajumuisha matibabu, lakini pia tiba, unajumuisha masuala yahusuyo ustawi wa mwanadamu kijamii, kisaikolojia, kiuchumi na kidini.

Zoezi la 1

Madhumuni ya zoezi: Baada ya kumaliza zoezi hili, washiriki watakuwa wamegundua aina za makundi kwenye jamii zao yanayonahitaji uponyaji kutokana na kuathiriwa na VVU.

Njia za kufundishia: vikundi vidogovidogo, majadiliano ya pamoja

Vifaa vya kufundishia: bango kitita, kalamu za maka

Muda: dakika 20

Mwezeshaji awagawe washiriki katika vikundi vidogovidogo vya watu wasiozidi sita na awasaidie washiriki kuchagua muongozaji na katibu katika kila kundi atakayeandika mawazo yote watakayokubaliana, na kuyawasilisha wakati wa majadiliano ya pamoja. Maswali na hoja zilizoorodheshwa hapa chini zinaweza kuliongoza kundi wakati wa majadiliano:

1. Angalia jamii yako na jaribu kuorodhesha makundi ya watu ambao wanahitaji uponyaji kutokana na madhara yatokanayo na VVU.
2. Yapange makundi uliyoyapata kwa kuzingatia vipaumbele na uhitaji wao wa uponyaji, namba moja ikionesha kundi ambalo linauhitaji mkubwa zaidi.

Zoezi la 2

Madhumuni ya zoezi: Mwisho wa zoezi hili, washiriki watakuwa wamegundua mahitaji maalum ya makundi mbalimbali katika jamii zao ambayo yameathiriwa na VVU.

Njia za kufundishia: vikundi vidogovidogo, majadiliano ya pamoja

Vifaa vya kufundishia: bango kitita, kalamu za maka

Muda: dakika 30

Mwezeshaji atawagawa washiriki katika vikundi vidogovidogo vya watu wasiozidi sita. Katika vikundi hivyo, washiriki wachague muongozaji na katibu ambaye ataandika mawazo yote watakayokubalina, na kuyawasilisha wakati wa majadiliano ya pamoja. Maswali na hoja zilizoorodheshwa hapa chini zinaweza kulisaidia kundi wakati wa majadiliano:

1. Orodhesha aina mbalimbali za uponyaji kwa watu tofautitofauti (mfano uwezeshaji wa kiuchumi nk).
2. Onyesha aina za uponyaji ambazo makundi tofautitofauti yametaja kuwa zinazihitajika katika zoezi la 1. Kundi moja linaweza likahitaji zaidi ya aina moja ya uponyaji. Orodhesha aina zote ambazo unadhani zimetajwa kuwa muhimu kwa kila kundi.
3. Gawa aina hizo tofautitofauti za uponyaji katika makundi mawili, kundi la kwanza linajumuisha mambo ambayo unadhani kwamba yanaweza kutekelezwa pasipo kuhitaji usaidizi wowote toka nje, wakati kundi la pili linajumuisha mambo ambayo unadhani jamii itahitaji usaidizi kutoka nje ili kuyatekeleza.
4. Je, viongozi wa dini pamoja na jumuiya za kiimani wanaweza kufanya nini ili kuiponya jamii na mtu mmoja mmoja walioathiriwa na VVU na UKIMWI?

Teolojia ya Kufuatana nao kama Zana Muhimu ya Uponyaji wa Kiimani

- Baada ya kugundua kuwa watu wengi katika jumuiya zetu za kidini wamepata madhara yatokanayo na VVU na UKIMWI, viongozi wa dini na washirika wa jumuiya za kiimani wanaalikwa ili wawe washirika wa wale wote wanaoishi na VVU na wale walioathiriwa na VVU. Huu ndio msingi mkuu wa Teolojia ya Kufuatana nao, ambayo ni lazima idhihirike katika jamii zetu.
- Neno teolojia lina maanisha namna ambavyo huwa tunafikiri, kutafakari na kuzungumza kuhusu Mungu. Hii ina maana kwamba katika kila siku ya maisha yetu kila mmoja wetu huwa anajihusisha na tafakari za kiteolojia.
- Neno kufuatana nao linamaanisha kutembea pamoja na mtu mwingine au wengine katika umoja. Mapito ya watu wengine yanakuwa ni mapito yako pia. Kupitia ufuasi, tunakuwa marafiki wa hiari. Watu waliopata shida ya

kuathiriwa na VVU na UKIMWI wapo safarini na hivyo basi jumuiya za kiimani zinakaribishwa kufuatana nao na kuwaunga mkono katika safari hiyo (Matendo ya Mitume 16:1-40).

- Tukiwa kama waamini, tunaamini kwamba Mungu yu pamoja nasi popote pale tuendapo na katika yote tuyafanyayo na kwa kuwa Mungu anataka tuwe kama yeye siku zote; tunaamini kuwa Mungu anataka sisi pia tuungane na wengine katika kuwatia moyo katika safari zao. Hii ni muhimu zaidi hasa pale safari hizo zinapokuwa na changamoto nyingi za kufa na kupona, safari ambazo zinaweza kuwa ni za kutisha iwapo kila mmoja atasafiri peke yake (Yer. 1:7-8).
- Hakuna mahali popote kwenye Biblia ambapo tunaweza kujifunza vizuri zaidi juu ya umuhimu wa jambo hilo kuliko sehemu inayozungumzia "njiani kuelekea Emau" (Luka 24:13-53), pale Kristo alipowatokea wale watu wawili akafuatana nao na hata akakaa meza moja nao. Kufuatana nao ndio namna pekee ya kuiishi na kuihubiri injili hai kwa wale ambao wanaojisikia kutengwa.
- Tukiwa kama waamini, kufuatana nao kunaweza kuwa kwa namna nyingi, zikiwemo zifuatazo:

1. Kufuatana nao kupitia Maombi

Omba kwa ajili ya wale ambao kwa umahususi wana uhitaji wa marafiki na usaidizi na kutiwa moyo kutokana na madhara yatokanayo na VVU na UKIMWI (Mwa. 20:1-18). Baadhi ya mifano ni kama vile watu ambao

- Wamepoteza wapendwa wao
- Wanahisi upweke
- Wametengwa
- Wananyanyaswa
- Wanasumbuka kutokana na imani zao
- Wametelekezwa
- Wapo kizuizini
- Wapo kwenye makazi ya kulelewa
- Wanakufa
- Ni wagonjwa
- Wapo katika hali ya mpito.

2. Kufuatana nao kupitia kujifunza

Soma Luka 2:1-20.

- Je, inamaanisha nini kusema Mungu alifanyika mwanadamu kamili?
- Je, hiyo inamaanisha nini kuhusiana na sisi kufuatana nao?
- Je, unaposema kufuatana na mtu fulani inamaanisha nini?

Soma Mwanzo 2-3.

- Je, ni nani aliyeumba vitu vyote duniani?
- Ni namna gani matendo ya Mungu yanakuwa kifani cha kufuatana nao?

- Je, tunajifunza nini kutokana na matendo ya Mungu tunapojiuliza kwamba tufanye nini kwa ajili ya watu wanaosumbuliwa na madhara ya VVU na UKIMWI?

3. Kufuatana nao kupitia Ibada

Kwenye simulizi kuhusu safari ya Emau, Yesu alikuwa akitembea pamoja na wanafunzi wake. Kutembea pamoja, kwa maana ya kawaida, yaweza kuwa aina fulani ya ibada. Tafakari kutembelea nyumba za jirani, na kuwaombea watu. Wimbo usemao "Tunatembea pamoja" ni wimbo wa kuabudu wenye nguvu sana unaozungumzia suala la kufuatana nao (Hapa mwezeshaji anaweza kutafuta nyimbo nyingine za kawaida zenye kueleza mshikamano na umoja). Usiishie tu kuwaombea wale ambao wana uhitaji wa marafiki, bali abudu pamoja nao pia. Wafanye wasijione kama unawaombea tu wakati hawapo; wafanye wajisikie kwamba hawako peke yao katika safari yao ya Imani kwa kuabudu pamoja nao.

4. Kufuatana nao kwa kuwatia moyo (Mt. 28:18-20)

Watu wanaoishi na VVU na wale walioathirika na UKIMWI wanaweza kuwa wamechoshwa na maisha kwa sababu ya msongo wa mawazo na ugumu wanaoupitia. Watu hawa wanapaswa kutiwa moyo ili wasikate tamaa maishani mwao, wasikate tamaa katika Mungu na kwenye jamii zao. Tunaweza tukafuatana nao kwa kuwatia moyo na kuwapa uzoefu wa namna ambavyo sisi pia tumekuwa tukitiwa moyo.

- Je, ni maneno gani au vifungu gani vya maneno vya kutia moyo ambavyo unaweza kuvitumia kumfariji mtu fulani?
- Je, una simulizi yoyote yenye kuonesha kufuatana na mtu? Ni nani ambaye alifuatana na wewe? Na je, ni kwa namna gani jambo hilo lilikubadilisha? Simulizi yako inaweza kuwa ni chanzo cha kuwatia moyo watu wengine.
- Je, ni watu gani ambao wapo katika jumuiya yako ya kiimani ambao unadhani wanahitaji kutiwa moyo na kukumbushwa au kuhakikishiwa kwamba kamwe hawapo peke yao? Je, wewe unaweza kuwafikia kwa namna gani?

5. Kufuatana nao kupitia Kutumika (Mt. 23:11)

Bila shaka tunafahamu kuhusiana na watu ambao hawana uwezo tena wa kufanya jambo lolote pasipo msaada. Tunaweza kuwa marafiki wa watu wa aina hiyo kwa kutafuta muda wa kuwa nao ili kuwasaidia kufanya mambo ambayo hawana uwezo nayo. Sisi kama waamini, tumeitwa kwa ajili ya kutumika kama vile Kristo alivyotumika.

- Je, kuna fursa zozote za kujitolea katika eneo lako ili kutimiza zoezi la kufuatana nao?

Mifano inaweza kuwa ni pamoja na kutembelea jela na vituo vya wasiojiweza, kufundisha shule ya jumapili, kufanya kazi za kipaimara, kujitolea shuleni, kutembelea waathirika majumbani mwao (kusaidia kazi za kufua

na kuandaa vyakula nk.). Kazi hizi ambazo zinaweza kuonekana kama si za umuhimu mkubwa ni miongoni mwa mambo makuu yenye kudhihirisha kufuatana nao.

6. Kufuatana nao kwa njia ya utoaji (Kumb. 24:19-22)

Madhara ya VVU na UKIMWI yamewaacha watu wengi wakiwa kwenye mazingira magumu, yamesababisha wazee wengi wawe na majukumu ya kuwatunza watoto walioachwa yatima kutokana na vifo vya mapema vitokanavyo na UKIMWI. Baadhi ya walezi hawa wamekuwa ni wazee sana na hivyo kushindwa kuwahudumia ipasavyo wajukuu zao. Katika mazingira mengine, watoto wadogo wameachwa ili wajitunze wenyewe, huku wakubwa wao wakibeba majukumu ya kuwa wakuu wa kaya.

- Katika mazingira ya aina hiyo, kufuatana nao kunaweza kukamaanisha pia kutoa msaada wa vitu kama vile vyakula, mavazi na malazi kwa ajili ya watu walio kwenye mazingira magumu. Angalia uwezekano wa kutoa baadhi ya mahitaji kwa kwa familia zilizopo kwenye mazingira magumu kama njia ya kufuatana nao.

7. Kufuatana nao kupitia Uwezeshaji (Mwa. 12:7)

Mara nyingi yatima, wajane na wazee wamekuwa ni miongoni mwa watu ambao huathirika sana na madhara yatokanao na VVU na UKIMWI, na hasa kwa sababu wengi wao wamekosa uwezo wa kujihudumia na kutokuwa na uwezo kiuchumi. Kufuatana na watu wa aina hii kunaweza pia kumaanisha kuwawezesha. Kwa mfano kuwawezesha ili waweze kujihudumia wao pamoja na familia zao. Aina hii ya kufuatana nao inaweza kujumuisha mambo yafuatayo:

- Kuwalipia watoto yatima ada ya masomo na ya mitihani
- Kutoa mitaji ya biashara kwa wajane na wazee wanaowahudumia yatima ili waweze kuanzisha miradi yenye kuzalisha mali.

Zoezi

Madhumuni: Hadi mwisho wa zoezi hili, washiriki watakuwa wamepata uelewa kuhusiana na umuhimu wa kufuatana nao na kuweka mipango ya namna ambavyo watafuatana na watu ambao wameathirika na VVU na UKIMWI katika jamii zao.

Njia za kufundishia: vikundi vidogovidogo, majadiliano ya pamoja

Vifaa vya kufundishia: bango kitita, kalamu za maka

Muda: dakika 30

Mwezeshaji awagawe washiriki katika vikundi vidogovidogo vya watu wasiozidi sita. Katika vikundi hivyo, washiriki wachague muongozaji na katibu atakayeandika mawazo yote watakayokubaliana na kuyawasilisha wakati wa majadiliano ya kundi zima. Maswali na hoja zilizoorodheshwa hapa chini zinaweza kusaidia kutoa mwongozo wa majadiliano.

1. Je, kufuatana nao kuna maana gani kwako katika muktadha wa VVU na UKIMWI?
2. Je, unadhani ni makundi gani ya watu katika jamii uliyopo ambao wanahitaji ufuatane nao?
3. Je, ni mambo gani unayoweza kufanya ili kufuatana na watu ambao wameathirika na VVU na UKIMWI katika jamii yako pasipo usaidizi toka nje?
4. Ni mambo gani ungependa kuyafanya ili kufuatana na watu waliopata shida ya VVU na UKIMWI katika jamii yako lakini mambo hayo yanahitaji usaidizi toka nje?

SOMO LA 9

Watoto, Vijana na Wenye Umri wa Kati, na Uponyaji wa Kiimani Katika Muktadha wa VVU

"Maana ndiwe taraja langu, Ee Bwana MUNGU, Tumaini langu tokea ujana wangu. Nimekutegemea Wewe tangu kuzaliwa, Ndiwe uliyenitoa tumboni mwa mama yangu, Ninakusifu Wewe daima. Nimekuwa kitu cha ajabu kwa watu wengi, Na Wewe ndiwe kimbilio langu la nguvu." (Zab 71:5-7).

Madhumuni ya somo

Kufikia mwisho wa somo hili washiriki watakuwa:

- Wameelewa namna ambavyo watoto, vijana na wenye umri wa kati walioambukizwa VVU wanavyoathiriwa na dhana zinazohusiana na kuponywa kwa imani
- Wamejifunza namna ambavyo watoto, vijana na wenye umri wa kati wanaoishi na VVU wanavyoweza kuishi maisha mazuri katika muktadha wa gonjwa hili
- Wameelewa namna ambavyo unyanyapaa na kutengwa kunavyoendelea kuwa ni tatizo linaloathiri watoto, vijana na wenye umri wa kati walioambukizwa au kuathiriwa na VVU na UKIMWI.

Usuli

- Vijana na wenye umri wa kati wanajumuisha moja ya makundi yaliyofichika kwa upande wa watu walioathiriwa na VVU barani Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara na duniani kwa ujumla.
- Mbali na kundi hilo ambalo linaendelea kuathirika kwa sababu ya shughuli mbalimbali za kiuchumi, kidini, kijamii na kisiasa, lipo kundi lingine la watu wanaokaribia utu uzima waliozaliwa wakiwa tayari wameambukizwa virusi. Kuanzishwa kwa shirika la Mpango wa Kuzuia Maambukizi kutoka kwa Mama kwenda kwa Mtoto (PMCT) na uwepo wa tiba vimeleta ongezeko la kundi la watoto ambao hawajaathirika na VVU waliozaliwa na wazazi wenye VVU. Pamoja na hayo kabla ya uvumbuzi huu wa kisayansi, watoto wengi walizaliwa wakiwa tayari wameathirika na VVU ambao baadae walianzishiwa dawa za kupambana na virusi na kwa sasa tayari wanakaribia utu uzima.
- Je, ni namna gani viongozi wa dini wanaikabili hali halisi kuhusiana na vijana hawa, ujinsia wao, uponyaji wa kiimani na dawa za kupambana na virusi?

Kwa kipindi kirefu sasa, jumuiya za kidini zimekuwa na tabia ya kuwaacha kama walivyo na kuwaficha watoto na vijana mambo ya ngono, hasa pale ambapo mjadala kuhusiana na ngono na mapenzi huibuka. Mara kwa mara kwa vijana wa makamo, masuala ya mapenzi yamekuwa yakizungumziwa kwa misimamo mikali, na kuwataka kujizuia mpaka watapofikia wakati wa ndoa, hata pale ambapo ujumbe wa aina hii umekuwa hautekelezeki au wakati ambapo vijana, na hasa wale wa kike, hawana nafasi kubwa ya kuchagua mtu wa kufanya naye mapenzi. Katika maeneo mengine watu wengine wamefikia hatua ya kuwafanyia maamuzi au kuwalazimisha kufanya ngono.

- Ni namna gani viongozi wa dini wanaweza kutengeneza mazingira ambapo unyanyapaa hautakuwa ni kikwazo kwa ustawi wa watoto, vijana, na wale wanaolekea utu uzima? Unyanyapaa katika UKIMWI imekuwa ni kikwazo kikubwa katika kuzuia VVU na kuwajali wenye UKIMWI, na baadhi ya tafiti zimefanyika kuangalia athari za mitazamo ya taasisi za kiimani kwa watu wanaoishi na VVU. Sekta ya dini imetiwa hatiani kutokana na kuchelewa kushughulikia masuala haya, na kushindwa kukiri kuhusu ukubwa wa tatizo kutokana na kuongezeka kwa kiwango cha maambukizi ya VVU, na kwa masuala ya uadilifu, na kuwa watu wenye mitazamo ya kuhukumu, na kwa kuonesha misimamo mikali kuhusiana na masuala ya VVU na UKIMWI katika jamii, hali ambayo imechangia sana kuendelea kuwepo kwa ukimya na usiri. Kuhusianisha kuambukizwa VVU na maadili mabaya au uzembe, na kushindwa kujadili kwa uwazi mambo yanayosababisha maambukizi ya VVU – hasa tofuati za kimamlaka – kumechangia pia kuwepo kwa unyanyapaa na ubaguzi ndani ya kanisa na kwa watu wanaoishi na VVU na UKIMWI.

Vijana Wanaoishi na VVU Katika Taasisi za Kikristo

- Hali ya vijana wanaoishi na VVU na UKIMWI katika taasisi za Kikristo ni simulizi inayosikitisha, na hasa tukiangalia mtazamo hasi wanaoupata katika makanisa yao. Hakuna ubishi kwamba taasisi hizo zinahubiri ujumbe wa kujizuia, lakini namna wanavyotafsiri ujumbe huu kwa wale ambao tayari wanaishi na VVU ni jambo linalotia shaka. Mtazamo hasi wa kuona VVU na UKIMWI kuwa ni laana kutoka kwa Mungu kwa hali ya kuruhusi itokee umefasili namna ambavyo teolojia ya Kikristo imetafsiri Biblia kuhusiana na suala VVU na UKIMWI. Wakati mwingine vijana wanaoishi na VVU wanakuwepo kwenye orodha ya washiriki wa kanisa lakini katika hali halisi hawashirikishwi katika mambo muhimu. Unyanyapaa na kutengwa kwa watu wanaoishi na VVU upo katika namna nyingi kuanzia ule uliofichika mpaka ule ambao ni wa wazi na wenye kujionesha kupitia mahubiri ya wachungaji, namna wanavyowaita watu kuombewa madhabahuni na katika mafundisho yao ya Biblia.
- Baadhi ya vijana wanaoishi na VVU wanaachana na matumizi ya dawa za kupambana na virusi baada ya kuambiwa na wachungaji wao makanisani kuwa wategemee maombi ya imani, ambayo yanafundisha kufuata tiba ya

kiimani ambayo haitegemeani na dawa za kupambana na virusi. Uponyaji ni jambo la msingi sana kwa makanisa mengi na kuna misimamo mikali ya kiimani katika nguvu ya maombi na miujiza, na vijana hawa ambao maisha yao yanasumbuliwa na VVU, unyanyapaa na kutengwa hudanganywa na kupandikizwa imani kwamba wakiacha dawa za kupambana na virusi na kuongeza maombi na imani, watapona kabisa VVU. Vijana wengi na wale wanaoelekea utu uzima katika kundi hili huishia kwenye vitanda vya mauti ikiwa ni matokeo ya kulazimishwa kutozingatia matibabu. Wakati mwingine, wazazi wanalazimishwa kuacha kuwapa watoto wao wadogo dawa za kupambana na virusi kwa sababu ya kuahidiwa uponyaji wa kimiujiza kwa ajili ya watoto wao.

"Tiba Ya Kimiujiza"

Kijana mmoja mwenye umri wa mika kumi na sita anayeitwa Oliva (si jina lake halisi) alituambia kuwa alikuwa ameambiwa na mchunguji wake kuwa wabadilishane dawa zake za VVU na chupa moja ya maji ambayo yangemponya. Akasema, watu wengine wengi wamewahi kuambiwa hivyo hivyo. "Nimewahi kwenda kwenye makanisa mengine pia mbapo mchungaji anasimama mbele, na kusema, 'Njooni mchukue maji haya ukinywa kiasi fulani cha maji hayo kwa idadi fulani ya siku, utapona," Siku chache baadae, baada ya mama yake kuhisi kile ambacho aliamini kuwa kilikuwa ni tiba ya kimuujiza, Oliva aliachana na matumizi ya dawa za hospitalini, na hali yake ya afya ikaanza kuzorota kwa kasi. Tangu hapo aliamua kurudia matumizi ya dawa zake na kusema kuwa anaamini kwamba alitakiwa kuchanganya matumizi ya dawa na imani yake ili kuponywa kwa imani. Wafanyakazi wa vituo vya afya pamoja na/au mashirika yanahitaji kuendelea kushughulika na familia ili zielewe kwamba imani zao zina nafasi na umuhimu mkubwa katika kuwasaidia warejee katika hali ya kawaida.

- Ni makosa sana kwa viongozi wa kiimani kufanya juhudi kubwa ya kuwashawishi waumini wao wanaoishi na VVU kuachana na matumizi ya dawa.
- Maombi si mbadala wa matibabu ya VVU; ila maombi yanakamilisha matumizi ya dawa za kupambana na virusi ili kuwa na uponyaji mkamilifu.
- Zipo fursa nyingi na uwezekano mkubwa kwa sekta za dini kujihusisha katika kuwajali, kuwafariji na kutoa misaada ya kipekee ya kiroho kwa jamii za watu wanaoishi au waliambukizwa VVU na UKIMWI.
- Upo umuhimu mkubwa kwa viongozi wa dini kujihusisha na suala la VVU kama suala muhimu na kutoa usaidizi wa kweli na wenye ufanisi na kuzungumza kuhusu mada hiyo. Vikundi na mashirika ya kiimani wanaweza kutoa michango chanya kwa kusaidia kuleta mwamko kuhusiana na VVU, wakio-

nesha faida za kupima na kuzingatia kikamilifu matumizi ya dawa za kupambana na virusi kwa vijana wote waishio na VVU na hasa pale inapokamilisha kwa maombi na imani.

Stadi za Maisha ili Kuwasaidia Vijana Kusalimika katika Muktadha wa VVU na UKIMWI

- Katika nyakati hizi ambapo kuna vijana wa kizazi kipya ambao ama wana maambukizi ya VVU au hawajaambukizwa, viongozi wa dini wana jukumu kubwa katika kufundisha stadi za maisha na taarifa sahihi zitakazowasaidia kujadili na kupanga ngono salama na pia kuzingatia tiba (kama ni muhimu kufanya hivyo) ili kuzuia maambukizi ya zamani au mapya.
- Vijana wenye maambukizi ya VVU wanaweza kutumia vyote viwili kwa pamoja, kuponywa kwa imani, na matibabu ya kitaalamu ya hospitali kama stadi yamaisha itakayowasaidia kusalimika. Matibabu ya kitaalamu ya hospitali, yanamaanisha utumiaji wa dawa za kisasa, zinazofanya kazi kwa pamoja na sala kutokana na nguvu zisizo za kawaida na wala hazifanyi kazi kinyume chake. Ni vizuri kuwafanya vijana na wale wanaoelekea utu uzima wawe na mtazamo kwamba mambo mawili haya hayapingani bali yanategemeana.
- Ushauri nasaha na kupima VVU (HCT) ni jambo muhimu kwa ajili ya kinga, matibabu, kuwatunza, na kuwategemeza vijana kikamilifu. Inawahamasisha vijana, mtu mmoja mmoja, wanandoa, wanafamilia na wanajamii kufahamu hali zao za VVU na kuwasaidia kuishi maisha mazuri, pamoja na mtindo mzuri wa maisha wenye kuzingatia afya na lishe nzuri. Inasaidia pia kutambua na kupunguza tabia hatarishi zenye kuchangia hatari ya kusambaa kwa VVU.
- Viongozi wa dini ni lazima wafanye kazi kwa kushirikiana na wahudumu wa afya na vijana na wale wanaoelekea utu uzima ili kuwafundisha tabia ya kulinda afya za watu walioathirika (k.m. kujiunga katika kutoa huduma za matunzo na kusaidia uzingatiaji wa sawa za kupambana na virusi). Hii inamaanisha kwamba viongozi wa dini watatakiwa kuwa na ujuzi wa kufundisha CSE au elimu ya mambo ya ngono, afya ya uzazi pamoja na haki (SRHR) kwa vijana na wale wanaoelekea utu uzima.
- Viongozi wa dini ni lazima wafanye ubia na vijana na wale wanaolekea utu uzima, ambao wanaweza kufanya kazi kama vile waelimishaji-rika kuhusu kupima, kujiweka wazi na kuzingatia matibabu.
- Kanisa linaweza kuwa ni mbia wa thamani sana katika kushughulika na vijana wanaoishi na VVU. Linaweza kukuza huduma hiyo na kushirikiana na wengine kupitia maombi na sala, pamoja na huduma na msaada wa kisaikolojia. Sekta ya afya hutoa msaada wa kitabibu na kufanya kampeni za afya. Ni jukumu la kanisa zima kutambua mambo ambayo Mungu anataka wakristo kuyafanya wakati huu wa uwepo wa VVU na kuwasaidia kutambua wajibu wao. Kufikia hapa, tunasisitiza matumizi chanya ya imani wakati huo huo vijana wakiendelea kutumia dawa au kuzingatia matibabu.

Zoezi

Njia za kufundishia: vikundi vidogovidogo, majadiliano ya pamoja
Zana za kufundishia: bango kitita, kalamu za maka
Muda: dakika 30

Mwezeshaji atawagawa washiriki katika vikundi vya watu wasiozidi sita na kuvisaidia vikundi hivyo kutafakari juu ya vijana na uponyaji kwa imani katika muktadha wa VVU na UKIMWI. Pia watafakari na kujadili namna ya kuzitumia familia katika kutoa huduma za VVU, vijana walioathirika na VVU katika makanisa/ taasisi nyingine za kikristo, na namna ya kuongeza ufahamu wa VVU na UKIMWI na kuwafundisha vijana stadi za maisha za namna ya kujikinga; kwakutumika mwongozo wa maswali na hoja zifuatazo:

1. Mkiwa kama familia, ni namna gani mtamshughulika au kuwa na uhusiano na mwanafamilia ambaye ameathirika na VVU?
2. Ni kwa namna gani vijana wanaoishi na VVU (kama wapo kanisani kwako) wanashughulikiwa au kushirikiana na wengine?
3. Je, umewahi kuona unyanyapaa wowote au hali ya kutengwa kwa vijana au wale wanaoelekea utu uzima walioathirika na VVU katika kanisa lako?
4. Je, vijana na wale wanaoelekea utu uzima walioko kanisani kwako wanayo nafasi ya kupata dawa ya kupambana na virusi? Je, kuna changamoto na fursa zipi kuhusiana na upatikanaji dawa za kupambana na virusi kwa vijana?
5. Je, ni kwa namna gani jumuiya za kiimani zinaweza kuwafikia (vijana) wanaoishi na VVU kwenye mashule yakiwemo yale ya bweni?

SOMO LA 10

Kuitazama Upya Maana ya Uponyaji kwa Jamii za Kiimani za Kimageuzi

"Roho wa Bwana yu juu yangu, Kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, Na vipofu kupata kuona tena, Kuwaacha huru waliosetwa." (Luka 4:18)

Madhumuni ya somo

Hadi mwisho wa somo hili, washiriki watakuwa na uelewa na taswira ya jamii za kiimani zenye mtazamo wa kimageuzi baada ya kushiriki katika kuitazama dhana ya uponyaji wa kiimani katika mtazamo kamilifu.

Usuli

Somo hili linalenga kutoa ufahamu wa mtazamo kwamba uponyaji kwa imani ni dhana pana kuliko tiba, kama tulivyoona huko nyuma. Somo hili pia linazingatia ukweli kwambamara VVU vikishaingia kwenye damu vinabaki humo milele, mpaka itakapotokea bahati ya kugundua dawa ya kuvifukuza. Hata hivyo, tunaamini kwamba watu wanaoishi na VVU ni watu wenye imani, wanaweza kuponywa kwa maana ya kufikia hatua ambapo watu wataona kwamba:

- Wanaweza kuvitawala VVU pamoja na madhara yake
- Wanaweza kuishi maisha ya kawaida kama watu wengine, ikiwa ni pamoja na kuweza kuoa na kupata watoto
- Hawanyanyaswi tena wala kutengwa na jamii, bali hujumuishwa kwenye jumuiya na jamii kwa ujumla
- Wanaweza kujitegemea kiuchumi wao mwenyewe pamoja na wategemezi wao.

Katika hali hiyo, watu wanaoishi na VVU wataweza kujikubali wao wenyewe (kuishinda hali ya kujinyanyapaa wenyewe) na kukubalika katika jumuiya na jamii zao kama ilivyo kwa watu wengine. Watu wa aina hiyo wanakuwa wameponywa japo hawajatibika. Kwa hiyo uponyaji wa kiimani unalenga kuwasaidia watu wanaoishi na VVU waweze kupata huduma zote zitakazowasaidia kuishi maisha ya kawaida. Pale jumuiya za kiimani zinapotimiza jukumu hili, wanakuwa wamefanya mageuzi kwa kufanya kazi na wataalamu wengine ili kuleta uponyaji mkamilifu kwa watu wanaoishi na VVU. Uponyaji wa aina hii utapenya pia kwa watu walioathirika na VVU.

Kuitazama Upya Dhana ya Uponyaji kwa Imani

- Tunaweza kusema kwamba Kuangalia Upya dhana ya Uponyaji kwa imani kunaweza kuelezwa kuwa ni kuutazama uponyaji kama aina ya tatu ya mifumo ya tiba yenye kwenda pamoja na makundi mengine ya dawa yaliyopo na tunayoyajua yaani, dawa za hospitalini na zile za kienyeji.
- Vidokezo kutoka katika Biblia kuhusu uponyaji vinaweza kutusaidia pia katika kuweka suala la uponyaji kwa imani kwenye muktadha wake. Uwepo wa tatizo la VVU na UKIMWI umesababisha uwepo wa mitazamo mipya ya kiroho katika suala la uponyaji na kwa kiasi fulani hali hiyo imefichua makundi ya watu (wakristo na wasio wakristo), wanaofanya utapeli kwa kujifanya waponyaji, wachungaji na manabii ambao wanadai kwamba Roho Mtakatifu anashinda magonjwa yote. Katika malekezo yao kwa wagonjwa mara nyingi hutumia vitu kama mafuta, maji matakatifu na vingine vingi ili kuleta uponyaji. Wakati mwingine watumishi hawa hupingana na juhudi zilizopo za kukabiliana na VVU na UKIMWI kwa kuwa wale ambao husema wamepona huamua kuacha matumizi ya dawa za kupambana na virusi na mwishowe huishia kufa. Vitendo hivi si uponyaji wa kiimani na ni lazima vipingwe na wakristo wote ambao hawajapotoka katika muktadha wa VVU na UKIMWI.
- Wakristo na jamii zao wana jukumu kubwa katika kukataa mateso, hasa katika zama hizi za uwepo wa VVU na UKIMWI. Uponyaji si tu ule wa kimwili bali pia ni ule wa kiroho. Iwapo kuna watu wanaamini kuwa wamepona, na jamii inakubali kuwa wameponywa, basi itakuwa ni kweli wamepona. Kama ilivyokuwa kwa suala la wale wakoma ambao walihukumiwa karibia hata kufikia hatua ya kutolewa uhai kutokana na hali zao, VVU na UKIMWI vitaweza kushindwa iwapo tu suala la uponyaji halitatazamwa kuwa ni kama juhudi za mtu mmoja. Kila mtu ashirikishwe, ikiwa ni pamoja na wataalamu kama vile madaktari na kadhalika, na kanisa lifanye nao kazi bega kwa bega na si kuvutana au kupingana nao kama washindani.
- Watu waelimishwe kwamba dawa za kupambana na virusi zipo katika mpango wa Mungu wa kushinda VVU na UKIMWI, na kwamba madaktari kama ilivyo kwa manabii, waponyaji na wachungaji – ni vyombo vya Mungu. Uponyaji hutokea kwa msaada wa nguvu za asili na zile zisizo za kawaida. Kuna namna tofauti tofauti ambazo Mungu anaweza kuingilia kati. Jambo muhimu ni kutambua kuwa uponyaji kamili hautokani na juhudi za mtu mmoja mmoja.
- Uponyaji kwa kutumia dawa za hospitali, ambao hujumuisha matumizi ya dawa za kisasa, ni wa asili kama ilivyo kwa matumizi ya mafuta matakatifu, maji, matope, majani na mizizi. Hivi vyote hufanya kazi sambamba na maombi ya nguvu sizizo za kawaida na si kwamba vinafanya kazi kwa kupingana.

- Neno uponyaji kwa imani linamaanisha uwezo wa imani kusaidia katika kurejesha hali ya ulinganifu kwa mtu kwa kushughulikia masuala ya kisaikolojia, kibiolojia, kijamii, kiuchumi, na kiroho ambayo yanasababisha kukosekana kwa ulinganifu ndani ya mtu. Uponyaji kwa imani upo kwa ajiili ya ukamilifu yaani hukamilisha aina nyingine za matibabu toka kwa wataalamu wa dawa na akili.
- Ni lazima jamii zikumbuke kwamba manabii wa kweli ni mawakili wa uzima na si mawakili wa mauti. Iwapo kuna mtu yeyote anadai kuwa yeye ni nabii wa Mungu, na hali anatangaza na kutoa ushawishi kwa kutumia ujumbe wenyw kuleta mauti, basi mtu huyo hawezi kuwa nabii wa kweli wa Mungu. Manabii wa uongo huwashawishi walio kwenye matibabu ya dawa za kupambana na virusi kuacha, na kusababisha kuzorota kwa afya zao hadi vifo.

Sifa za Jamii za Kimageuzi Kiimani

Kuna fursa nyingi zilizopo kwenye jumuiya na kwenye jamii za kiimani/kidini zinazotoa nafasi ya kuwajali, kuwafariji na kutoa msaada wa kipekee wa kiroho kwa jamii zilizoathirika au kuathiriwa na VVU na UKIMWI. Aidha, jamii za kiimani za kimageuzi zenye kuyaishi mafundisho yao. Mafundisho hayo husisitiza kumpenda jirani, na wenye shida, kuwa na huruma, kuwakubali na kuwavumilia "wengine" ambao wanaweza kuwa ni wa dini, rangi na imani tofauti. Jamii za Kiimani za kimageuzi zinapingana na aina zote za unyanyapaa na ubaguzi kwa watu walioathirika na VVU na UKIMWI.

- **Jamii za kimageuzi ni wajumbe wa jamii zenye imani tofautitofauti**. Wameitwa na Mungu kwa ajili ya kuyathibitisha maisha ya matumaini na uponyaji katikati ya uwepo wa VVU na UKIMWI. Ukubwa wa Janga la ugonjwa limesababisha jamii hizo ziunganishe nguvu bila kujali tofauti zao za kiimani. Taratibu zao zianawataka watangaze na kuhubiri matumaini, na kusherehekea uhai na uponyaji katikati ya mateso. VVU na UKIMWI ni janga la jamii yote ya wanadamu, hali ambayo wote wanaishiriki.
- **Jamii za kimageuzi kiimani zimeitwa kwa ajili ya kupenda.** Mungu huwa haadhibu kupitia maradhi au magonjwa bali yupo pamoja na watu wake akiwa kama nguvu yao, ujasiri kwao na tumaini lao. Mungu wamjuaye, kwa hakika, ni mkuu kupita VVU na UKIMWI.
- **Jamii za kimageuzi kiimani wameitwa kwa ajili ya kuhudumia kwa upendo.** Ni lazima kwao kuhakikisha kwamba wale wote walioathirika au kuathiriwa na ugonjwa huu (pasipo kujali dini, kabila, daraja, umri, taifa, uwezo kimwili, jinsi, au mwelekeo wa kijinsia) wanapata nafasi ya kuhurumiwa, kupewa matunzo yasiyobagua, kuheshimiwa, kufadhiliwa, na kupewa msaada.
- **Jamii za kimageuzi kiimani wameitwa kwa ajili ya kushuhudia na kutenda haki.** Wamejizatiti kubadili sera na mitazamo ya jamii, wanaunga

mkono mila na sheria za nchi zenye kulinda haki za raia wote wanaoishi na VVU na UKIMWI na wasiojiweza. Wamejitoa pia kuzungumza waziwazi kuhusu kuzuia, kuzingatia matibabu ya VVU na UKIMWI, na huruma kwa watu wote.

- **Jamii za kimageuzi kiimani zinahamasisha kinga.** Ndani ya mazingira ya tofauti zao za kiimani, wanahamasisha taarifa sahihi na zenye kujitosheleza kwa jamii kuhusiana na maambukizi ya VVU na njia za kujikinga. Wameahidi kutengeneza mpango madhubuti wa kuzuia maambukizi ya VVU na UKIMWI kwa vijana na watu wazima.
- **Jamii za kimageuzi kiimani hukiri kwamba wao ni sehemu ya jumuiya yote ya dunia.** Ijapokuwa VVU na UKIMWI zinaharibu jamii, na madhara yake ni makubwa zaidi katika maeneo mengine ya dunia na jamii. Jamii za kimageuzi kiimani hutambua na kuuthamini ubia na ushirikiano na watu wengine duniani.
- **Jamii za kimageuzi kiimani hupinga dhambi ya kutokuvumiliana na uadui.** VVU na UKIMWI si gonjwa lenye "kutenganisha" watu. Linaathiri wanaume, wanawake na watoto wa rangi zote. Jamii za kimageuzi kiimani hukataa hali ya kushindwa kuvumiliana na uadui ambayo imesababisha watu wengi kutumia nguvu zao katika kuwalaumu wale walioathirika na VVU na UKIMWI, na wanakuwa wanakaziania masuala ya ngono, kujithamini, hadhi ya madaraja, au uraibu wa kemikali.
- **Jamii za kimageuzi kiimani huzihamasisha jamii zinazowazunguka.** Hii ni kwa sababu masuala kama vile tofauti za kiuchumi na umaskini ni miongoni mwa mambo makuu yenye kuchangia uwepo wa gonjwa la VVU na UKIMWI na kuzuia kinga na matibabu, jamii za kimageuzi kiimani huzishawishi sekta zote katika jamii kutafuta namna ya kuondoa umaskini ili kuwa na mustakabali wenye matumaini na ulinzi.
- **Jamii za kimageuzi kiimani zimejizatiti kufanya mambo kivitendo zaidi.** Hutafuta njia za kivitendo za kukidhi mahitaji yanayowazunguka.
- **Jamii za kimageuzi kiimani huhamasisha uponyaji kwa imani uliomkamilifu.** Kwa kusoma maandiko, kanisa linawasaidia wale walioathirika au kuathiriwa kimaadili na kiroho na pia linawaombea na kufanya sala pamoja nao. Linawasaidia kupitia maandiko ambayo husomwa na kuwatia moyo walioathirika au kuathiriwa. Pia hutoa usaidizi kwa kutekeleza teolojia ya kufuatana nao.
- **Jamii za kimageuzi kiimani huzingatia njia za uponyaji za kibiolojia, kisaikolojia, kijamii na kiroho na ya kiroho.** Jamii hizo hutambua mchango wa wadau mbalimbali, kama vile waganga, manesi, washauri nasaha na wafamasia katika kufanikisha uponyaji mkamilifu wa waathirika na waliopata madhara.

Zoezi

Njia za kufundishia: vikundi vidogovidogo, majadiliano ya pamoja
Vifaa vya kufundishia: bango kitita, kalamu za maka
Muda: dakika 30

Mwezeshaji atawagawia washiriki katika vikundi vidogovidogo vya watu wasiozidi sita na ataviruhusu vikundi hivyo kutafakari kuhusu mambo ambayo jamii za kimageuzi kiimani hufanya pamoja na kujadili sifa za jamii hizo kwa kuongozwa na hoja na maswali yafuatayo:

1. Je, unadhani kuna haja yoyote ya kuitazama upya maana ya uponyaji kwa imani katika muktadha wa VVU na UKIMWI?
2. Je, unadhani mtazamo mpya wa maana ya "uponyaji kwa imani" iliyotolewa kwenye somo hili inajitosheleza? Iwapo jibu ni hapana, nini kiongezeke kwenye maana mpya ya "uponyaji kwa imani" iliyotolewa?
3. Kwa maoni yako, unadhani sifa za jamii za kimageuzi kiimani zina halalisha uwepo wake?
4. Je, una maoni gani kuhusiana na makanisa yaliyopo kwenye eneo lako ukilinganisha na sifa za jamii zilizogeuzwa kiimani?

SOMO LA 11

Mikakati ya Uponyaji Mkamilifu – Kuchagua Mbinu ya Uponyaji Inayotumia Njia za Kibiolojia, Kisaikolojia, Kijamii na Kiroho

"Bwana, unifadhili, maana ninanyauka; Bwana, uniponye, mifupa yangu imefadhaika. Na nafsi yangu imefadhaika sana; Na Wewe, Bwana, hata lini? Bwana urudi, uniopoe nafsi yangu, Uniokoe kwa ajili ya fadhili zako."
(Zab 6:2-4)

Madhumuni ya somo

Ifikapo mwisho wa somo hili, washiriki watakuwa wameelewa madhara mbalimbali yatokanayo na VVU na UKIMWI na namna ya kufanikisha uponyaji mkamilifu kwa wale wote walioathirika au kuathiriwa na VVU na UKIMWI.

Usuli

Somo hili linalenga kuelezea uponyaji mkamilifu, ambao ni jaribio la kuondoa aina zote za mateso ambayo wanadamu wanayapitia katika maisha yao ambayo huwafanya si tu kuwa wagonjwa bali pia kutokuwa na afya. Uponyaji mkamilifu unaweza kuapatikana tu ikiwa sisi sote tutaungana ili kushughulikia mambo yote yanayowaathiri watu.

Madhara Mbalimbali ya VVU na UKIMWI

VVU na UKIMWI vimeathiri kwa namna mbalimbali watu binafsi, familia na jamii. Madhara yake yamesababisha jamii kuugua kwa namna tofauti tofauti. Ni vigumu au haiwezekani kabisa, kukuta watu au familia ambazo hazijawahi kupata madhara yatokanayo na VVU na UKIMWI kwa siku za leo. Zifuatazo ni miongoni mwa athari mbalimbali za VVU na UKIMWI kwa watu:

- Baadhi ya watu wameambukizwa virusi. Watu hawa wanalazimika kuishi na virusi kwa maisha yao yote yaliyobaki kwa sababu hakuna tiba.
- Baadhi ya watu wamekufa kutokana na magonjwa yatokanayo na UKIMWI. Wengine pia wanaendelea kufa kutokana na sababu hizo katika jamii mbalimbali, ijapokuwa idadi ya watu wanaokufa imepungua sana kutokana na matumizi ya dawa za kupambana na virusi.

- Watu wengine wamekuwa wagonjwa na kushindwa kufanya kazi kutokana na mifumo yao ya kinga kuvamiwa na VVU. Kutokana na kushindwa kuzihudumia familia zao, familia zao zimejikuta katika mazingira magumu na ya umasikini.
- Jamii na familia nyingi zimeshuhudia nguvu kazi ya wale wanaotegemewa kiuchumi kuuawa na UKIMWI, na kusababisha upungufu mkubwa wa wazalishaji mali. Hali hiyo imesababisha familia nyingi kuwa katika mazingira hatarishi na ya umaskini. Jamii za aina hiyo zimebaki na watoto wadogo ambao hawana uwezo wa uzalishaji mali wa kuaminika na nyingine zimebaki na wazee ambao kutokana na umri wao hawawezi kuzalisha chochote.
- Kutokana na kupoteza nguvu kazi, jamii nyingi zimeshuhudia ongezeko la ajira za utotoni kutokana na watoto wengi kulazimika kuwa wakuu wa familia zao na kulazimika kuwatunza wadogo zao. Wazee pia wamejikuta katika hali ambayo hawana uwezo wa kufanya kazi lakini wanahitaji kuwalea wajukuu zao.
- Jamii nyingi zimeshuhudia uwepo wa watoto waliojeruhiwa kisaikolojia, waliomizwa mioyo na kuhuzunishwa kutokana na kuwaona wazazi wao wakiwa wagonjwa na kuteseka hadi kufa wakati huo huo wao wakilazimika kubeba majukumu kabla ya wakati wao, wakijikuta wakihama kutoka katika hatua ya utoto na kuwa wakuu wa familia.
- Baadhi ya wazee (babu au bibi) pia wamejeruhiwa kisaikolojia kutokana na kushuhudia watoto wao wakifa wakati bado wakiwa wanakabiliwa na majukumu ya kulea watoto na wakati ambao wazee hao pia walidhani ingekuwa ni fursa yao ya kutunzwa na watoto wao.
- Jumuiya za kiimani zimetikiswa pia kutokana na kushuhudia mashujaa wao wa imani wakiugua UKIMWI, na hasa pale, jamii za kiimani wakati fulani walipokiri (na baadhi mpaka leo huendelea kukiri) kwamba UKIMWI ni ugonjwa utokanao na mambo machafu. Jamii hizo zimejeruhiwa kiroho.
- Watu kutoka katika jamii za kiimani ambazo zimeathirika au kuathiriwa na VVU pia wameumizwa kiroho, kutokana na kutakiwa kukabiliana na unyanyapaa na kukataliwa kutoka ndani ya jamii zao. Wapo baadhi yao ambao wamefika mahali hata wameamua kuacha imani zao kutokana na kupitia adha ya virusi na magonjwa. Watoto yatima na wazazi ambao ni wazee wameachana na jamii zao za kiimani kutokana na unyanyapaa na wao pia wamjeruhiwa kiroho.

Ukiangalia madhara yote hayo, utaona kuwa VVU na UKIMWI vimeathiri watu wengi katika hali mbalimbali kama vile kibiolojia, kisaikolojia, kijamii, kiuchumi, na kiroho. Hii inamaanisha kwamba wale wote walioathirika au kuathiriwa kwa namna mbalimbali wanahitaji uponyaji katika maeneo yote hayo.

Zoezi la 1

Madhumuni ya zoezi: Baada ya kumaliza zoezi hili, washiriki watakuwa wameelewa namna mbalimbali ambavyo VVU na UKIMWI vimeathiri jamii zao.

Njia za kufundishia: vikundi vidogovidogo, majadiliano ya pamoja

Vifaa vya kufundishia: bangokitita, kalamu za maka

Muda: dakika 20

Mwezeshaji atawagawa washiriki katika vikundi vya watu wasiozidi sita. Washiriki katika vikundi hivyo wachague mwendeshaji na katibu atakayerekodi hoja zote watakazokubaliana na kuziwasilisha mbele ya kundi zima. Maswali na mawazo yaliyoorodheshwa hapa chini yanaweza kutumika kama mwongozo wa majadiliano:

1. Tupe uzoefu wako kuhusu namna ambavyo VVU na UKIMWI vimeiathiri jamii yako mara tu baada ya upatikanaji mkubwa wa dawa za kupambana na virusi (Zingatia kuzungumzia makundi-rika yaliyoathirika zaidi, ambayo yameshuhudia idadi kubwa zaidi ya vifo, na namna ambavyo jambo hilo limeathiri idadi ya watu, pamoja na changamoto kubwa ambazo jamii yako inatakiwa kuzishughulikia).
2. Je, ni ujumbe gani ambao hapo awali watu katika jamii yako ya imani walikuwa nao kuhusu VVU na UKIMWI pamoja na wale wote ambao wameathirika au kuathiriwa nao? Je, kwa sasa unadhani ni ujumbe gani ambao jamii yako ya imani wanaweza kuutoa kwa watu wanaoishi au walioathiriwa na VVU na UKIMWI?

Zoezi la 2

Madhumuni ya zoezi: Hadi mwisho wazoezi hili, washiriki watakuwa wametambua madhara mbalimbali ya VVU na UKIMWI katika jamii zao.

Njia za kufundishia: vikundi vidogovidogo, majadiliano ya pamoja

Vifaa vya kufundishia: bangokitita, kalamu za maka

Muda: dakika 30

Mwezeshaji atawagawa washiriki katika vikundi vidogovidogo vya watu wasiozidi sita. Washiriki katika vikundi hivyo wachague mwendeshaji na katibu atakayerekodi hoja zote watakazokubaliana na kuziwasilisha mbele ya kundi zima. Maswali na mawazo yaliyoorodheshwa hapa chini yanaweza kusaidia kuongoza majadiliano. Kama tulivyoonesha hapo juu, VVU na UKIMWI vinawaathiri watu kibiolojia, kisaikolojia, kijamii, kiuchumi na kiroho. Katika zoezi hilii ni lazima athari hizi zielezwe na kufafanuliwa.

1. Orodhesha mifano ya madhara ya VVU na UKIMWI kibiolojia kwa watu walioathirika na kuathiriwa na virusi.
2. Orodhesha mifano ya madhara ya VVU na UKIMWI kisaikolojia kwa watu walioambukizwa na walioathiriwa na virusi.
3. Orodhesha mifano ya madhara ya VVU na UKIMWI kijamii kwa watu na jamii zilizoathiriwa na ugonjwa huu.
4. Orodhesha mifano ya madhara ya VVU na UKIMWI kiuchumi kwa mtu mmoja mmoja, familia na jumiya nzima ya watu alioathiriwa na gonjwa hili.
5. Orodhesha mifano ya madhara ya VVU na UKIMWI kiroho kwa mtu mmoja mmoja, familia na jumiya nzima ya jamii ya watu alioathiriwa na gonjwa hili.

Uponyaji Mkamilifu: Mbinu yaKukabiliana na Athari za VVU na UKIMWI

- Mara nyingi huwa tunawaza kuhusu uponyaji pale ambapo tunasikia hali ya ugonjwa kwa kuwa mara nyingi uponyaji hutafsiriwa kama ni suala linalohusisha kuondosha ugonjwa toka mwilini mwa mtu. Kwa maana hiyo, uponyaji unatafsiriwa kama njia ya kitabibu ya kurekebisha maumivu ya kibiolojia katika mwili wa mwanadamu. Hata hivyo, katika masomo yaliyopita na sehemu inayofuata ya mwongozo huu tumekosoa aina hiyo ya uelewa wa uponyaji, kwa kuwa ni mtazamo finyu sana wenye kusahau aina nyingine za uponyaji ambazo sote tungependa kuzipata.
- Uponyaji mkamilifu ni jitihada za kutaka kuondoa aina zote za maumivu ambayo wanadamu hupitia katika maisha yake, ambayo si tu kwamba husababisha wanadamu wawe wagonjwa, bali pia huwafanya wasiwe katika hali nzuri. Uponyaji mkamilifu unaweza kupatikana iwapo tu sisi sote tutania mamoja na kushirikiana na wengine katika kukabili mambo mbalimbali yanayowaathiri watu.
- Katika sehemu iliyopita, tumegundua kwamba tatizo la VVU na UKIMWI limesababisha magonjwa, umaskini, kuharibika kwa mahusiano katika jamii, na mateso ya kisaikolojia, kiroho na kiuchumi kwa watu. Kwa hiyo hii inamaanisha, iwapo tunataka uponyaji mkamilifu ufanikiwe, ni lazima tushughulikie masuala yote hayo.
- Kupitia maazimio tuliyofikia pale Kampala mwaka 2017, washiriki walishadidia umuhimu wa kutumia mbinu ya Uponyaji Mkamilifu – yaani mbinu inayoshughuliki uponyaji katikaa nyanja zote za kibiolojia, kisaikilojia, kijamii na kiroho kuwa ni mkakati bora zaidi wa kuufuata ili kufanikisha uponyaji mkamilifu na endelevu kwa watu wanaoishi na VVU pamoja na watu na jamii zote zilizoathiriwa na VVU na UKIMWI.

- Mbinu au mkakati huu unakataa madai ya uponyaji kwa imani pekee kutoka kwa viongozi wa kiimani na pia haukubaliani na kukataa kila kitu kuhusiana na kuponywa kwa imani kutoka kwa wasioamini. Kinyume chake mkakati huu unawaalika wadau na wataalamu mbalimbali ili waje na mkakati wa pamoja utakaofanikisha uponyaji mkamilifu.
- Je, mbinu ya uponyaji iitwayo ya kibiolojia, kisaikolojia, kijamii na kiroho ni nini? Kwa kifupi, mbinu hii ya uponyaji huhusisha ushirikiano na sekta mbalimbali katika kupambana na VVU na UKIMWI ili kufanikisha uponyaji.
    1. Neno **kibiolojia** humaanisha umuhimu au haja ya uwepo wa mchango wa masuala ya biolojia au dawa ili kufanikisha uponyaji mkamilifu. Wataalamu wa afya kama vile madaktari, manesi na wafamasia wana jukumu na mchango mkubwa sana katika kushughulikia matatizo ya kitabibu yanayowapata vijana walioathirika na virusi. Makundi mengine yote ya watu wana jukumu la kuunga mkono msaada huo wa kitabibu na kitaalamu. Jukumu kubwa kwa watu wengine wote waliobaki ni kuwahamasisha watu wanaotumia dawa kuzingatia matibabu. Hapa ndipo masuala ya dawa za kupinga virusi yanapoingia.
    2. Neno **kisaikolojia** linamaanisha kuwa kuna haja ya uwepo wa wanasaikolojia katika kuchangia uponyaji mkamilifu. Majeraha ya kiakili au kisaikolojia yanayotokana na watu kujua kuwa wanaishi na virusi ambavyo kamwe haviwezi kuondoka katika mifumo ya miili yao, ni tatizo kubwa linalohitaji utatuzi ili kufanikisha uponyaji ulio kamili. Maumivu ya kiakili yatokanayo na kuwaona wapendwa wako wakipata shida katika kukabiliana na kuukubali ukweli kwamba wanaishi na virusi au wanaugua magonjwa yanayohusiana na virusi na UKIMWI-vinaacha makovu ya kisaikolojia kwa watu na jamii. Hivyo basi wanasaikolojia wanatakiwa kuwa wadau wakubwa na muhimu katika kufanikisha uponyaji mkamilifu katika muktadha wa VVU na UKIMWI.
    3. Neno **kijamii** linawakilisha jamii, lakini lina maana pana zaidi katika matumizi yake. Neno hili linajumuisha mambo ya kijamii na kiuchumi katika maisha yetu. VVU na UKIMWI vimesababisha matatizo mengi ikiwa ni pamoja na kuingilia mahusiano kutokana na watu kukataliwa, kuachwa na kutengwa na familia na jamii zao. Changamoto hii pia imesababisha kuvurugika kwa shughuli za kiuchuni – watu wamepoteza kazi kutokana na kuwa wagonjwa kiasi cha kushindwa kufanya kazi. Uzalishaji kwenye mashirika umepungua kwa kuwa nguvu kazi imepungua. Kutokana na uwepo wa VVU na UKIMWI familia zimekuwa maskini. Idadi ya yatima imeongezeka na familia zinazoongozwa na watoto zimeongezeka. Uponyaji mkamilifu ni lazima ushughulikie changamoto zote hizi za kijamii na kiuchumi kwa kuwa zinasababisha mwanadamu asiwe na hali njema. Wataalamu walio katika maeneo hayo pamoja na watu wengine ni lazima waungane kutafuta namna ya kuimarisha ubia kati ya familia na jamii pamoja na kupambana na umasikini.

4. Neno **kiroho** linamaanisha hali ya binadamu katika masuala ya kiroho, na kiimani, ambayo ni maeneo ambayo pia hayajakwepa madhara yatokanayo na VVU na UKIMWI. Watu wengi walioambukizwa na kuathiriwa na UKIMWI, wamejikuta wakihoji hali zao za kiroho na imani pale wanapokabiliwa na ukweli kuhusu VVU na UKIMWI. Uwepo wa watu wengi walioathirika au kuathiriwa, umesababisha watu kugeukia mambo ya kiroho na kiimani pale wanapokabiliwa na shida ya VVU na UKIMWI. Katika nyakati wanapokuwa katika maumivu makali, watu wengi wamekuwa wakitaka kuwa na uhakika iwapo kama bado Mungu yu pamoja nao. Wachungaji na makasisi pamoja na wahudumu waliosimikwa wa dini na jamii nyingine za kiimani kwa ujumla, ni lazima wachukue nafasi zao katika kutimiza hamu ya kufikia uponyaji mkamilifu. Kwa baadhi yetu, dawa za kupambana na virusi hazitaweza kufanikiwa mpaka pale viongozi wa dini watakapokuwa wametuhakikishia kuwa dawa za kupambana na virusi zimevuviwa na Mungu na mpaka pale watakapokuwa wameweka mikono juu yetu na kutuombea.

- Uponyaji mkamilifu unaweza kufikiwa iwapo tu watu kutoka katika sekta mbalimbali wataungana na kuamua kushughulikia kwa pamoja matatizo mbalimbali yanayomsumbua mwanadamu katika muktadha wa VVU na UKIMWI.

Zoezi la 1

Madhumuni ya zoezi: Kufikia mwishoni mwa zoezi hili, washiriki watakuwa wameweza kujifunza na kuelewa mbinu zinazopendekezwa za uponyaji mkamilifu katika muktadha wa VVU na UKIMWI.

Njia za kufundishia: vikundi vidogovidogo, majadiliano ya pamoja

Vifaa vya kufundishia: bangokitita, kalamu za maka

Muda: dakika 30

Mwezeshaji atawagawa washiriki katika vikundi vya watu wasiozidi sita. Washiriki katika vikundi hivyo wachague msimamizi na katibu atakayerekodi hoja zote watakazokubaliana na kuziwasilisha mbele ya kundi zima. Maswali na mawazo yaliyoorodhesha hapa chini yanaweza kusaidia kuongoza majadiliano.

1. Kwa mujibu wa mwongozo huu, ni mkakati gani unaopendekezwa ili kufanikisha uponyaji mkamilifu katika muktadha wa VVU na UKIMWI?
2. Unadhani ni kwa nini ni muhimu kufanya kazi kwa pamoja ili kufanikisha uponyaji mkamilifu kwa watu wanaoishi na VVU au watu walioathiriwa na VVU na UKIMWI?

Zoezi la 2

Madhumuni ya zoezi: Mwishoni mwa zoezi hili, washiriki wataweza kuandaa mpango kazi wa namna ambavyo wataweza kushiriki kufanikisha uponyaji mkamilifu kwa kutumia njia ya uponyaji ya kibiolojia, kisaikolojia, kijamii na kiroho.

Njia za kufundishia: vikundi vidogovidogo, majadiliano ya kundi zima

Vifaa vya kufundishia: bangokitita, kalamu za maka

Muda: dakika 30

Mwezeshaji atawagawa washiriki katika vikundi vya watu wasiozidi sita. Washiriki katika vikundi hivyo watachagua msimamizi na katibu atakayerekodi hoja zote watakazokubaliana na kuziwasilisha mbele ya kundi zima. Maswali na mawazo yaliyoorodheshwa hapa chini yanaweza kusaidia kuongoza majadiliano:

1. Je, wewe unaangukia katika kipengele au vipengele vya gani vya mkakati huu? (Inawezekana mtu kuwa katika zaidi ya kipengele kimoja.)
2. Orodhesha mambo unayoweza kuyafanya katika kundi ulilopo ili kuchangia katika kuleta uponyaji wa mtu mmoja mmoja na jamii ama kwa kusaidiwa, au pasipo usaidizi wa watu kutoka nje.
3. Orodhesha mambo unayoweza kuyafanya ili kuwasaidia wengine katika nyanja mbalimbali ili kuwafanya wao wenyewe wachangie katika kuleta uponyaji wao binafsi au wa jamii zao.
4. Ni kwa nini unadhani oponyaji mkamilifu ni muhimu?

SEHEMU YA 3

Mbinu na Mikakati ya Kufanikisha Uponyaji Mkamilifu Katika Muktadha wa VVU na UKIMWI

SOMO LA 12

Kutambua Ubia na Ushirikiano

"Kwa kuwa walipo wawili watatu wamekusanyika kwa jina langu, nami nipo papo hapo katikati yao." (Mt. 18:20)

Madhumuni ya somo

Hadi mwisho wa somo hili, washiriki watakuwa wameelewa umuhimu wa kuwa na ubia na ushirikiano.

Usuli

Ili kuwa na matokeo mazuri zaidi katika jamii tunazozifanyia kazi, mara zote ni muhimu kuweka rasilimali zote pamoja, ikiwa ni pamoja na michango yetu ya mawazo pamoja na ufahamu wa mambo. Tunapoweka rasilimali pamoja, tunajiweka katika nafasi nzuri zaidi ya kufanikisha mambo mengi zaidi kuliko kama tutafanya kila mtu peke yake. Kihistoria, jamii zetu zilikuwa na mazoea ya "kukutanika pamoja" kwa malengo ya kila mtu kumsaidia mwenzake. Kwa kuwa VVU na UKIMWI vimeathiri jamii, si tu kwa mtu mmoja mmoja, basi itakuwa rahisi zaidi kushughulikia tatizo hilo kwa pamoja kwa kushirikiana na wengine wanaofanya kazi katika maeneo yanayohusiana na tatizo hilo. Uponyaji mkamilifu unamaanisha kushughulikia mambo yote yanayoweza kuzidisha madhara kwenye jamii za watu walioathiriwa na VVU na UKIMWI, mambo kama vile uzalishaji wa vyakula, upatikanaji wa dawa, mambo ya kiroho na mahusiano. Kwa kuwa si rahisi kwa kundi moja peke yake kutimiza mambo yote anayohitaji mtu ili apate uponyaji, ni muhimu kushirikiana na kufanya kazi pamoja ili kufanikisha uponyaji mkamilifu kwa mtu mmoja mmoja na hata kwa jamii.

- Takwimu za dunia zinaonesha hali halisi ilivyo kuhusiana na ugonjwa wa UKIMWI kwa mataifa ya Afrika na nchi zinazoendelea kwa ujumla. Hata hivyo madhara ya VVU na UKIMWI yanayoonekana sasa Afrika yataendelea kuwepo kwa miaka mingi ijayo.
- Baadhi ya mambo yenye kuonesha ukubwa wa tatizo tatizo la VVU na UKIMWI barani Afrika yanajulikana vizuri sasa, na hivyo kuhitaji kuchukua hatua zisizo za kawaida katika kukabiliana nayo. Hali ya VVU na UKIMWI inatoa changamoto za kipekee ambazo zinahitaji mbinu sizizo za kawaida kupitia ushirikiano na kuundwa kwa ubia na wadau kutoka ndani ya jamii na kwingineko.
- Janga la VVU na UKIMWI linatishia hali ya afya na maendeleo ya binadamu, linadhoofisha jamii na ukubwa wa janga unazidishwa zaidi na uwepo wa vita, migogoro ya kiraia na uhamaji wa watu. Aidha, vita dhidi ya VVU na UKIMWI huathiriwa na upungufu wa rasilimali, na hivyo kuifanya kila senti na shilingi inayopatikana kuwa muhimu na kulazimu kuhitaji busara kubwa katika kuipangia matumizi.
- Janga la VVU na UKIMWI linatofautiana na magonjwa mengine yanayoua kwa sababu lenyewe huangamiza watu wakati ambapo mchango wao unahitajika zaidi, na wakati ambapo wanatazamiwa kuwa wazazi wenye wategemezi. Kwa umahususi, janga la VVU na UKIMWI limerudisha nyuma maendeleo ya Afrika yaliyopatikana kwa miongo minne iliyopita na linatishia maendeleo ya Afrika kwa vizazi vijavyo.
- Hivyo basi ni muhimu sana kwamba ili kushughulikia janga hili vizuri, ni vema kutopoteza nguvu pasipo sababu kwa kurudia yale ambayo yameshafanywa au yanafanywa na wengine ili kutopoteza rasilimali chache tulizonazo katika kutekeleza malengo.

Je, Ubia ni Nini?

- Neno Ubia linamaanisha mpangilio fulani (rasmi au usio rasmi) ambapo wahusika wajulikanao kama wabia, hukubaliana kushirikiana ili kutekeleza kwa pamoja malengo yao. Wakati mwingine, ubia huu kati ya taasisi huhusisha watu wanaofanya mambo yasiyo fanana.
- Kwa mfano, ubia unaweza kuhuhusisha watoa huduma wa afya, taasisi za kiimani, mashirika ya misaada ya kilimo na mashirika wafadhili. Mashirika hayo ambayo hutofuatiana kwa kiasi fulani yanaweza kuunganisha juhudi zao ili kutimiza malengo ya pamoja.
- Mara nyingi shughuli za ubia hufanikiwa pale ambapo kuna ufanisi wa kazi na majukumu na iwapo majukumu hayo yameainishwa vizuri kwa kila mbia, na iwapo uwajibikaji kwa kila mmoja umewekwa wazi na kuainishwa vizuri.
- Katika shughuli za ubia, wabia hutakiwa kuwajibika kila mmoja na kujenga hali ya kila mmoja kumwamini mwenzake.

Je, Ushirikiano ni Nini?

- Neno ushirikiano lina uhusiano wa karibu na ubia, lakini pia maneno haya yanatofautiana. Wakati ubia kwa ujumla huzaa aina fulani ya ushirikiano, si kila ushirikiano unaweza kuwa ubia.
- Ushirikiano ni juhudi za pamoja za watu au kundi wanapoamua kufanya jambo au mradi fulani kwa pamoja. Mara nyingi ushirikiano huwa unatokea kwenye mashirika yenye mitazamo inayofanana, ambapo huchanganya rasilimali zao ili kufanikisha malengo yao ya pamoja.
- Hivyo basi, ushirikiano una maana inayokaribiana na ushirika kuliko ilivyo kwa ubia.
- Kwa mfano, Baraza la Makanisa Duniani kupitia mpango wa WCC-EHAIA-linalenga kukuza ujuzi kuhusu VVU katika makanisa na wanafanya kazi pamoja na taasisi za kiteolojia ili kulijumuisha suala la VVU katika mtaala wa teolojia pamoja na kukabiliana na visababishi vya ugonjwa huu. ARASA- ni ubia wa kikanda wa mashirika yasiyo ya kiserikali yanayofanya kazi pamoja ili kuimarisha ushughulikiaji wa suala la VVU, UKIMWI na Kifua Kikuu kupitia uwezeshaji na uhamasishaji na kwa kuzingatia mtazamo wa haki za binadamu katika nchi za kusini mwa Afrika. Ubia huu umeundwa kwa mtindo wa wakfu na mashirika wabia ambayo pia ni wajumbe wa wakfu huo. Kamati za uendeshaji, ambazo hujumuisha wajumbe wa wakfu hufanya kazi pia kama wajumbe wa bodi ya ushauri wa maeneo mawili ya programu ya ARASA: (i) mafunzo na kuongeza ufahamu; na (ii) uhamasishaji na ushawishi. Chombo kinachoitwa INERELA+ ni mtandao wa kimataifa unaojumuisha viongozi mbalimbali wa makanisa wa imani zote – mchanganyiko wa wafanyakazi wa kawaida na wale waliosimikwa, wanaume na wanawake – ambao ama wanaishi na waathirika au wao wenyewe wameathiriwa na VVU. Ubia huu unalenga katika kuwawezesha wanachama wake kutumia nafasi walizo nazo katika makundi yao ya kiimani kuvunja ukimya, kukosoa unyanyapaa na kusaidia kutoa kinga yenye kuzingatia hali halisi, kuwajali, pamoja na kushughulikia tiba. Kwa njia hii wanaweza kuunganisha nguvu na rasilimali ili kutoa mwongozo kuhusu uponyaji kwa imani na uzingatiaji wa matibabu. Kwa kuwa wakiwa kama shirika moja wanakuwa rasilimali chache ambazo zisingetosha kutoa miongozo, kwa kuweka nguvu pamoja wameweza kutoa mwongozo na kuusambaza kwa wengine.
- Mtazamo huu wa ushirikiano una unafuu mkubwa sana wa gharama katika mazingira ambapo kuna upungufu mkubwa wa rasilimali, na hivyo ni wa muhimu sana.

Sifa za Msingi na Kanuni za Kufanya Ubia na Ushirikiano

- **Malengo na maono yanayoelekeana** (mazoea mazuri): Shughuli za ubia ambazo zimejengwa katika maono na malengo yanayoelekeana husaidia kukuza hali ya kila mmoja kumsaidia mwenzake na mshikamano si tu katika utekelezaji wa miradi husika bali hata katika mambo mengine nje na hayo. Kufanya ubia na sekta tofauti inasaidia uwepo wa fursa mpya na kuongeza uwezo wa kufanya shughuli katika maeneo ya kijamii mengi zaidi.
- **Msukumo wa ujumuishaji** (mazoea mazuri): Shughuli za ubia na zile za ushirikiano ambazo huundwa kwa dhamira ya kujumuisha, zina nafasi nzuri zaidi ya kuheshimu na kuhamasisha maadili ya umajumui. Kufanya kazi na watu tofauti husaidia kufaidika na utofauti wa kitaasisi uliopo na ambao ni sehemu ya mazungumzo ya kila siku, na husaidia pia katika kuhakikisha kwamba shughuli za kijamii zinazoanzishwa zinaakisi sauti tofautitofauti, watekelezaji tofautitofauti na maoni yanayotofautiana.
- **Heshima, uaminifu, uwazi na utayari wa kuwajibika (**mazoea mazuri): Wadau bora ni wale ambao uhusiano wao una nguvu na umejengwa katika misingi ya kuheshimiana na kuaminiana, na ambamo wabia hufanya juhudi ya kuuelewa vizuri zaidi na kuuthamini upande wa pili. Wanahakikisha kwamba wabia wote wameweka wazi na kufafanua namna ambavyo fedha za mradi/shughuli zitashughulikiwa. Wanaujenga ubia katika michakato yenye kusisitiza na kuhakikisha kuwa kuna uwazi na uwajibikaji. Ni muhimu pia kuheshimu mchango na mawazo ya kila upande.
- **Heshima kwa hali ya kuwa huru** (mazoea mazuri): Kila mbia au mshiriki ni taasisi iliyo huru. Hali hiyo husababisha uwepo wa umuhimu wa wajibu na majukumu yanayohusiana na muundo, utawala, wajibu, nk. wa pande husika, ambayo yanaweza kutofautiana kati ya taasisi moja na nyingine. Ni muhimu kujadili na kuelewa wajibu na vikwazo vya kila upande mapema na kutilia maanani wajibu na vikwazo hivyo wakati unapofanya maamuzi mbalimbali.
- **Uwezeshaji wa usambazaji wa maarifa** (mazoea mazuri): Wakati ushirikiano hufanya kazi katika mazingira ambayo sio thabiti, kuwa na mpango mzuri wa mawasiliano wenye kuonesha tarehe za kukamilisha mawasiliano fulani miongoni mwa wabia ni muhimu ili kuhakikisha maarifa yanasambazwa ipasavyo kwa wahusika.
- **Makubaliano kuhusu madhumuni, matarajio, majukumu na wajibu** (mazoea mazuri): Kila mbia au mshirika atakuwa na orodha ya vipimo au maswali ya tathmini ili kubainisha madhumuni, matarajio, majukumu na wajibu wao ndani ya ubia husika, vilevile na wabia watarajiwa. Pia watahakikisha kwamba wabia wote wanayaelewa kikamilifu ili kuondoa uwezekano wa uwepo wa kutoelewana. Ni muhimu kuwepo kwa ushahidi wa kimaandishi kuhusu makubaliano hayo.

Faida/Manufaa ya Ubia na Ushirikiano

Mbinu za kutumia ubia katika kushughulikia changamoto zimekuwa ni maarufu sana miongoni mwa watunga sera. Zifuatazo ni miongoni mwa faida/manufaa ya kufanya ubia:

- **Kuwezesha ubunifu na tathmini:** Bila shaka ubia na ushirikiano ni maeneo yenye uwanja mpana wa kujaribu mawazo au mbinu mpya na ubunifu, pale wabia/wadau wanapoungana pamoja wakitokea katika nyanja na maeneo tofauti tofauti. Jambo hilo peke yake, linaweza kuleta mabadiliko makubwa sana kutokana na kubadilishana mawazo, utaalamu, na uzoefu, na ni rahisi kupunguza hatari zinazoweza kujitokeza.
- **Kushirikishana maarifa, utaalamu na rasilimali:** Moja kati ya sifa kubwa za shughuli za ubia/ushirikiano kati ya taasisi moja na nyingine ni namna ambavyo inakuwa rahisi kubadilishana ujuzi, maarifa, na utaalamu ili kuongeza kiwango cha usahihi, ubora na ufanisi katika uwezo wa kutatua matatizo.
- **Kuweka pamoja rasilimali na kuunganisha juhudi:** Katika ngazi ya chini kabisa, mbinu za ubia zinaweza kuongeza kiwango cha jumla cha rasilimali zilizopo kwa ajili ya kutatua matatizo au changamoto za kijamii, kiuchumi, kisiasa na matatizo ya kiafya. Ni rahisi pia kuwa na juhudi za pamoja kwa njia ya kuungana.
- **Kuongeza ufanisi na uwajibikaji:** Moja kati ya faida kubwa ambazo huhusishwa na uwepo wa ushirikiano/ushirika na ubia kati ya taasisi moja na nyingine ni kwamba kwa kiasi kikubwa inaweza ikasaidia katika kuongeza ufanisi, kwa kuondoa hali ya kurudia rudia ufanyaji wa kazi ile ile na kuboresha mawasiliano.
- **Uwezeshaji:** Ubia na ushirikiano wenye kujumuisha wadau wa ndani unaweza kusaidia kuwawezesha watu kutoka ndani ya jamii hiyo na kuwasaidia wanajamii hao kujiona kuwa ni wamiliki.
- **Husaidia kukubalika na "kupata mambo mapya":** Inaweza kusaidia uchotaji "maarifa toka kwa watu wa ndani" kupitia ushirikishwaji wa wabia/wadau kutoka katika ngazi ya jamii na matumizi yake yanaweza kuchangia sana katika kuendeleza matumizi ya mbinu zinazoweza kutatua matatizo ya ndani kwa ufanisi zaidi. Kuwahusisha wabia/wadau toka ngazi ya jamii kunaweza pia kuongeza hali ya kukubalika, na kuhamasisha misaada ya ndani, kwa ajili ya malengo mapya ya kisera.

Hasara/Matatizo/Mapungufu ya Kufanya Ubia

Kama ilivyo kwa aina nyingine zote za matokeo ya kuwaleta watu tofauti pamoja, kufanya ubia na ushirikiano kuna changamoto zake, ambazo zinaweza kuzuia ufanisi:

- **Migogoro kuhusiana na malengo na madhumuni:** Mara nyingi kukosekana kwa malengo ya wazi, na mahsusi hutajwa kwamba ndicho chanzo kikuu cha kushindwa kwa shughuli nyingi za ubia. Makubaliano mengi ya ubia huzingatia tu malengo ya jumla jumla, pasipo kuweka wazi malengo yao mahsusi, au mara nyingine wabia wanaweza kuwa na uelewa tofauti kuhusiana na maana halisi ya malengo yao. Jambo hili linaweza kutokea zaidi iwapo baadhi ya wabia watakuwa na ajenda zao za siri au "zilizofichika." Katika ngazi ya kimkakati, vipaumbele vinavyopingana na "vita vya kutaka kutawala" ambapo mashirika au taasisi tofauti hugombea kutawala jambo au huduma fulani, inaweza kuzuia juhudi za kuwa na malengo au mbinu za pamoja.
- **Gharama za Rasilimali:** Kufanya ubia kuna husisha kiasi kikubwa cha rasilimali na gharama, kama vile kugharimia muda wa wafanyakazi waliomo kwenye ubia na muda wao wa kufanya mikutano na majadiliano, na kuchelewa kufikia maamuzi kutokana na haja ya kufanya mashauriano na wabia wengi. Ni vigumu pia kusitisha shughuli za ubia ambazo hazitakuwa na mafanikio, au hata pale ambapo madhumuni yake yamefanikiwa; iwapo kutakuwa hakuna makubaliano kutoka pande zote kwa kuwa hili linaweza "kuharibu" mahusiano.
- **Uwajibikaji:** Kunaweza pia kutokea tatizo la uwajibikaji iwapo kutakuwa hakuna yeyote miongoni mwa wabia mwenye kujiona kuwa anawajibika kuhusu jambo au tendo fulani ndani ya ubia kutokana na mgawanyiko wa majukumu au mamlaka (kwa mfano, hakuna mbia anayewajibika kikamilifu kuhusiana na matatizo yanayoibuka au katika kuhakikisha sera inayofuatwa inaleta ufanisi au inatimiza malengo). Inaweza kuwa hakuna uwazi kuhusu "ni nani mwenye mamlaka."
- **Matatizo ya kitaasisi:** Baadhi ya vikwazo vikubwa vya shughuli za ubia au ushirikiano wenye ufanisi ni pamoja na mambo ya kitaasisi (hii ni pamoja na tofauti katika malengo, tofauti za mielekeo ya kitaalamu, tofauti za miundo na ufanyaji kazi ndani ya taasisi); mambo ya kisheria/utaalamu (sheria au kanuni zilizotungwa na mamlaka za juu, na tofauti katika uwezo wa kiteknolojia na utendaji ndani ya taasisi); na masuala ya siasa (siasa za nje zinazoizunguka taasisi lakini pia hata siasa za ndani na urasimu ndani ya taasisi).
- **Tofuti za kimtazamo miongoni mwa wabia:** Yapo mambo mengi yanayohusiana ambayo yanaweza kuathiri uanzishaji na uendelezaji wa shughuli za ubia kama vile tofauti za kanuni za tabia na mfumo wa kimadili miongoni mwa wabia.

- **Mahusiano ya kimamlaka:** Ushughulikiaji wa tofauti zilizopo za kimamlaka za vyombo au watu mbalimbali ndani ya ubia ni suala muhimu katika kufanikisha shughuli za ubia. Kunaweza kukajitokeza tofauti mbalimbali za kimamlaka miongoni mwa watendaji katika hatua mbalimbali za shughuli za ubia. Tofauti hizo zitahitaji kushughulikiwa kwa umakini kwa kuwa zinaweza kuharibu uwezekano wa kufanya ubia na ushirikiano.
- **Ushiriki wa jamii:** Katika kuufanya upya ubia, kukosekana kwa "uwezo wa jamii husika" kunaweza kuwa miongoni mwa vizuizi kwa wadau/washirika wa ndani kushiriki katika ubia husika. Si hivyo tu, bali pia ushiriki wa wale wanaojitolea kama watekelezaji "kunaweza kuhatarisha au kuhujumu majukumu halali" ya asasi za kijamii.

Zoezi

Njia za kufundishia: vikundi vidogovidogo, majadiliano ya pamoja
Vifaa vya kufundishia: bango kitita, kalamu za maka
Muda: dakika 40

Mwezeshaji atawagawa washiriki katika vikundi vidogovidogo vya watu wasiozidi sita na kuvisaidia vikundi hivyo kutafakari kuhusu shughuli za ubia na ushirikiano, namna gani ubia na ushirikiano hufanya kazi, na ni kwa nini ni jambo la msingi sana kutengeneza na kuimarisha shughuli za ubia na ushirikiano kwa ujumla na kwa umahususi katika muktadha wa VVU na UKIMWI. Aidha, washiriki watafakari kwa kina kuhusu sifa za ubia na ushirikiano, kanuni zake muhimu, pamoja na faida na hasara au mapungufu ya ubia na mashirikiano. Maswali na hoja zifuatazo hapa chini zinaweza kusaidia kutoa mwongozo wa majadiliano:

1. Je, ubia na ushirikiano, ni nini? Onesha tofauti zake na mambo yenye kushahibiana.
2. Je, ni kwa kiwango gani ubia na ushirikiano huchangia katika kufanikisha malengo ya jumla katika jamii yako katika muktadha wa VVU na UKIMWI?
3. Je, ni namna gani ubia na ushirikiano, hufanya kazi?
4. Kwa kuangalia wabia ambao hufanya kazi pamoja katika jamii yako, je, kuna nyakati ambapo umewahi kufikiria kwamba kanisa lisiruhusu ubia au ushirikiano? Je, kuna faida na hasara zipi za ushirikiano? Je, kuna faida na hasara zipi za kufanya ubia?
5. Fikiria kuhusu shughuli za ubia na ushirikiano, ambazo hazikuweza kufanikisha malengo yaliyotarajiwa na orodhesha mambo ambayo yamechangia hali hiyo. Onesha namna ambavyo mambo hayo yangeweza kuepukika?
6. Je, ni aina gani ya ubia na ushirikiano, itahitajika ili kushughulikia masuala ya uponyaji kwa imani?

SOMO LA 13

Utetezi na Mawasiliano

"Je! Saumu niliyoichagua, siyo ya namna hii? Kufungua vifungo vya uovu, kuzilegeza kamba za nira, kuwaacha huru walioonewa, na kwamba mvunje kila nira? na kama ukimkunjulia mtu mwenye njaa nafsi yako, na kuishibisha nafsi iliyoteswa; ndipo nuru yako itakapopambazuka gizani; na kiwi chako kitakuwa kama adhuhuri." (Isa 58:6-10)

Madhumuni ya somo

Mwisho wa somo hili washiriki watakuwa wameelewa:

- Dhana ya utetezi katika muktadha wa tiba ya dawa za kupambana na virusi na uponyaji kwa imani
- Umuhimu wa mawasiliano katika muktadha wa dawa za kupambana na virusi na uponyaji kwa imani
- Majukumu muhimu ya viongozi wa dini katika utetezi na mawasiliano kuhusiana na uzingatiaji wa matibabu.

Ni muhimu sana kwa viongozi wa dini kushirikishwa kikamilifu katika kuhamasisha uzingatiaji wa matibabu katika muktadha wa VVU na UKIMWI. Kwa kufanya hivyo wanahitaji kuongozwa na umaizi unaotokana na ufahamu wa utetezi na mawasiliano.

Je, Utetezi na Mawasiliano ni nini?

Ingawa zipo fasili nyingi (na mara nyingine zenye kukinzana) za utetezi na mawasiliano, katika somo hili tutatumia fasili ambazo zimerahisishwa kuhusiana na dhana hizo. Dhana ya **Utetezi** kwa viongozi wa dini inamaanisha, "kusimama kwa ajili na kusimama pamoja na" mtu mmoja mmoja, familia na jamii ambazo zina mahitaji maalumu yanayopaswa kutimizwa. Huko nyuma, ilidhaniwa kwamba mtetezi anapaswa "kuongea kwa niaba ya watu wasio na sauti." Lakini mara nyingi wanaharakati wamekuwa wakiwaambia viongozi wa dini, "Sisi si watu wasio na sauti. Tuna sauti isipokuwa tu hamtaki kutusikiliza."

Hivyo basi, kwa sasa utetezi unaeleweka kama ifuatavyo:

- Kuwa tayari kujifunza kutoka kwa wale ambao wameshuhudia jambo fulani wao binafsi au wameshiriki binafsi katika suala husika
- Kutoa fursa kwa wale ambao wao binafsi wameshuhudia suala fulani au wamelishiriki ili walifafanue suala hilo wao wenyewe

- Kuwaunga mkono wale ambao wameshuhudia suala fulani wao binafsi au wamelishiriki
- Kupinga sera au matendo yanayohusisha unyonyaji na ukandamizaji
- Kuungana na jamii zilizo katika mazingira magumu kwa ajili ya kufikia mageuzi ya kudumu ya kijamii.

Na mawasiliano yanaeleweka kama ifuatavyo:

- Utoaji au ubadilishanaji taarifa kwa njia za mazungumzo, maandishi, au kwa kutumia vyombo vingine.

Mawasiliano na utetezi ni dhana ambazo zina uhusiano wa karibu. Ili utetezi bora ufanyike ni lazima kuwa na mawasiliano yenye ufanisi. Kuhusiana na kushughulikia uzingatiaji wa matibabu katika muktadha wa VVU na UKIMWI, viongozi wa dini wanatakiwa kuwasiliana vizuri na kwa ufanisi.

Namna Bora ya Kufanya Utetezi na Mawasiliano kwa Viongozi wa Dini ili Kuboresha Uzingatiaji wa Matibabu

Viongozi wa dini wapo katika nafasi nzuri zaidi kimkakati ya kuweza kutekeleza vizuri zaidi jukumu la utetezi na mawasiliano kwa lengo la kuongeza kiwango cha uzingatiaji wa matibabu katika muktadha wa VVU na UKIMWI. Yaliyoorodheshwa hapa chini ni miongoni mwa mambo muhimu ya kuzingatia ili viongozi wa dini waweze kukosoa mafundisho potofu yenye kuwafanya baadhi ya watu waache matumizi ya dawa na kuanza kutegemea uponyaji kwa imani pekee:

- Kuwa makini kuhusiana na maandiko matakatifu yenye kuunga mkono utetezi na uharaka katika kuyakabili masuala yanayohatarisha afya na ustawi wa watu wa Mungu, kama vile uzingatiaji wa matibabu katika muktadha wa VVU na UKIMWI
- Pata maarifa na taarifa za kutosha kuhusiana na dawa za kupambana na virusi (ubora wake, madhara n.k)
- Tumia mimbari na wakati mtakatifu kuwasilisha ujumbe chanya unaotangaza dawa za kupambana na virusi kama mpango wa Mungu kuingilia kati katika utatuzi wa tatizo la VVU na UKIMWI
- Kuwa na utayari wa kuelezwa uzoefu kutoka kwa watu wanaoishi na VVU, wape heshima na fursa ya kuliongoza kanisa na washiriki juu ya umuhimu wa kuzingatia matibabu
- Tilia mkazo utumiaji wa dawa za kupambana na virusi kwa watu wanaoishi na VVU.
- Tangaza ujumbe ambao hauna utata wala mikanganyiko na wenye kuwahamasisha watu wanaoishi na VVU kuzingatia dawa za kupambana na virusi

- Tumia mikakati tofautitofauti ya mawasiliano ili kuboresha uzingatiaji wa matibabu katika muktadha wa VVU na UKIMWI
- Wakaribishe watu waliobobea kitaaluma katika masuala ya afya au utaalamu mwingine ili wawaelimishe washirika kuhusiana na dawa za kupambana na virusi
- Tumia aina mbalimbali za mawasiliano zilizopo (kama vile, ujumbe mfupi wa maandishi) ili kufikisha ujumbe chanya kuhusiana na dawa za kupambana na virusi.

Changamoto Ambazo Viongozi wa Dini Hukumbana nazo katika Kushughulikia Madai ya Uponyaji kwa Imani Pekee

Ipo haja kwa viongozi wa dini kufanya utetezi bora ili kuhakikisha kwamba wale wote wanaostahili kufaidika kutokana na dawa za kuokoa maisha wanafanikisha hilo. Ni aibu na inasikitisha sana kuona kwamba maisha ya watu yanapotea wakati Mungu ameshasaidia kufanikisha upatikanaji wa dawa zinazorefusha maisha. Ndugu Canon Gideon Byamugisha, ambaye ni mmoja kati ya wanaharakati ambao wako wazi na mwenye msimamo anayetoka miongoni mwa wanajumuiya ya waamini, mara nyingi amekuwa akieleza kuwa baadhi ya vifo vinaweza "kuahirishwa na vinazuilika." Hapa anamaanisha vile vifo ambavyo hutokea kwa sababu ya mtu kukosea jambo fulani au mahali fulani. Kwa hakika, vifo vitokanavyo na kushindwa kuzingatia dawa za kupambana na virusi vinaangukia katika kundi hilo. Hivyo basi, viongozi wa dini wanapaswa kujihusisha kikamilifu katika kushughulikia madai ya uponyaji kwa imani pekee katika muktadha wa VVU na UKIMWI. Byamugisha, pamoja na viongozi wengine wa dini kama vile Phumzile Mabizela na Rahab Kariuki, mara zote wamekuwa wakiwahamasisha viongozi wa dini kuhubiri ujumbe wenye kuleta uhai katikati ya uwepo wa VVU na UKIMWI.

Ili viongozi wa dini wafanye kazi vizuri katika kushughulikia madai ya uponyaji kwa imani pekee katika muktadha wa VVU na UKIMWI, wanatakiwa kuwekeza katika kufanikisha shughuli za ubia na ushirikiano. Wanapaswa kuunganisha nguvu pamoja na wadau wengine ili waweze kufikia malengo yao kwa kadri inavyowezekana. Moja kati ya changamoto kubwa inayozikumba jamii za kiimani imekuwa ni tabia ya kila mtu kufanya kazi peke yake. Ni kwa njia ya kuunganisha nguvu za wahusika pekee, ndipo tunaweza kushughulikia kikamilifu changamoto ya madai ya uponyaji kwa imani pekee katika suala la VVU na UKIMWI.

Zoezi

Madhumuni ya zoezi: Hadi kufikia mwisho wa zoezi hili, washiriki watakuwa wametafakari aina tofauti tofauti za wadau wanaoweza kufanya nao kazi katika kushughulikia changamoto ya madai ya uponyaji kwa imani pekee katika muktadha wa VVU na UKIMWI.

Njia za kufundishia: vikundi vidogovidogo, majadiliano ya pamoja

Vifaa vya kufundishia: bango kitita, kalamu za maka

Muda: dakika 30

Mwezeshaji awe na ufahamu wa ushirikiano wa kimkakati unaofaa unaoweza kufanywa na vyombo vya habari, idara na taasisi za serikali (Afya, Mambo ya Ndani, Usalama, nk.), Taasisi zisizo za kiserikali (wanasheria), kampuni za dawa na zile za famasia, nk. Mwezeshaji anatakiwa kuonesha mikakati ya kisasa ya mawasiliano iliyopo, kama vile matumizi ya simu za kiganjani katika kuinua kiwango cha uzingatiaji wa matibabu.

Mwezeshaji atawagawa washiriki katika vikundi vya watu wasiozidi sita na kuviruhusu vikundi hivyo kujadili na kutafakari umuhimu wa kuwa na ushirikiano na wengine katika kushughulikia suala la madai ya uponyaji wa VVU na UKIMWI kwa imani pekee kwa kujadili hoja na maswali yafuatayo:

1. Je, ni changamoto zipi ambazo mtu mmoja mmoja, familia, na wanajamii wamekumbana nazo kuhusiana na madai yauponyaji wa VVU na UKIMWI kwa imani pekee?
2. Je, unadhani ni wadau gani wengine muhimu kwako waliopo na wenye kuonesha utayari wa kushughulikia tatizo la madai ya uponyaji wa VVU na UKIMWI kwa imani pekee? Je, wanafanya nini kuhusiana na madai ya uponyaji wa VVU na UKIMWI kwa imani pekee?
3. Je, ni kwa namna gani (viongozi wa dini) tunaweza kushirikiana na wadau wengine ili kushughulikia madai ya uponyaji wa VVU na UKIMWI kwa imani pekee?
4. Ni kwa namna gani tunaweza kujenga na kufanikisha ushirikiano bora na imara zaidi kwa watu wenye imani zinazotofautiana ili kukabiliana na tatizo la madai ya uponyaji wa VVU na UKIMWI kwa imani pekee?
5. Fanya utambuzi wa fursa na changamoto zinazoweza kujitokeza pale tunapotaka kuhakikisha kunakuwa na ushirikiano na watu wengine katika kukabiliana na madai ya uponyaji wa VVU na UKIMWI kwa imani pekee.

SOMO LA 14

Uongozi wa Kimageuzi Katika Kuleta Uponyaji Mkamilifu: Kutekeleza Utetezi

"Haya ndiyo asemayo Bwana; Kwa makosa matatu ya Israeli, naam, kwa manne, sitaizuia adhabu yake isimpate; kwa sababu wamewauza wenye haki kwa fedha, na maskini kwa jozi ya viatu; nao hutwetea mavumbi yaliyo juu ya vichwa vya maskini, na kuipotosha njia ya mwenye upole; na mtu na baba yake humwendea mwanamke mmoja, hata kulitia unajisi jina langu takatifu."
(Amosi 2:6-7)

Madhumuni ya somo

Hadi mwisho wa somo hili, washiriki watakuwa wameweza kutambua na kutekeleza mbinu za uongozi katika kushughulikia changamoto za madai ya uponyaji kwa imani pekee katika muktadha wa VVU na UKIMWI.

Usuli

- Uongozi maana yake ni kuwa mbunifu katika kutatua na kufanya maamuzi mazuri unaposhughulikia changamoto zenye kutishia afya na ustawi wa watu, familia, jamii, na mataifa.
- Uongozi wenye ufanisi unataka mtu mwenye uwezo wa kusikiliza na kushirikiana na wengine kutafuta utatuzi.
- Uongozi maana yake ni kusimama kwa ajili ya na kusimama pamoja na watu, familia, jamii na mataifa yanayoishi au kuathiriwa na virusi vya VVU na UKIMWI.
- Mashirika kama vile INERELA+ yamekuwa mstari wa mbele katika kukabiliana na suala la VVU na UKIMWI. Wameshiriki katika kuzihamasisha jamii zao kutumia rasilimali zao katika ubunifu wa kushughulikia janga hili na kwa hali uendelevu.

Je, Uongozi wa Kimageuzi Maana Yake ni Nini?

Dhana ya uongozi ina fasili nyingi. Hata hivyo maana iliyotawala zaidi ya uongozi **wa kimageuzi** ni aina ya uongozi yenye kujumuisha wahusika kujitolea na kuchukua hatua za kivitendo. Katika muktadha wa kukabiliana na changamoto za madai ya uponyaji wa VVU na UKIMWI kwa imani pekee, uongozi wa kim-

ageuzi unamaanisha kuwa na viongozi wa dini ambao wamekubali kuzibeba changamoto zitokanazo na VVU kama sehemu ya majukumu yao na kuwa mstari wa mbele katika kuzishughulikia.

Uongozi wenye mtazamo mpya una sifa hizi:

- Ni jumuishi
- Huzuia tatizo kabla halijatoke

Uongozi jumuishi unamaanisha kwamba viongozi hawatumii mtindo wa "jeshi la mtu mmoja" ambapo wao peke yao ndio wanakuwa chanzo kikuu cha suluhisho la shida zote. Katika kushughulikia changamoto za madai ya uponyaji wa VVU na UKIMWI kwa imani pekee, uongozi jumuishi humaanisha kwamba viongozi huaanzisha na kuimarisha ubia na ushirikiano na wadau wengine wanaofaa. Viongozi hawa wa dini hawawachukulii wadau wengine kama maadui au washindani, bali wanawachukulia kama "wafanyakazi wenza katika shamba la Mungu."

Kuwa jumuishi kuna maanisha kufanya kazi na watu kutoka fani mbalimbali na kuruhusu uwepo wa mitazamo tofautitofauti kuhusu masuala mbalimbali. Kuwa jumuishi kuna maanisha kumkubali kila mtu pasipo kulaumu au kuhukumu "wengine." Katika suala la kukabiliana na changamoto zinazotokana na wale wanaopinga matumizi ya dawa za kupambana na virusi na kusisitiza uponyaji kwa imani pekee, ni lazima viongozi wa dini wawe na utayari wa kuwashirikisha na kukabiliana na wale wote wanaoeneza teolojia za aina hiyo. Neno kuwashirikisha lilivyotumika hapa halimanishi kuungana nao katika mitazamo yao. Hata hivyo, katika hali ya kawaida hakuna suluhisho lolote lile la kudumu linaloweza kufikiwa katika kukabiliana na changamoto hii isipokuwa uwepo wa majukwaa ya majadiliano. Ni jambo la kutia moyo sana kuona kwamba katika maeneo mengine, viongozi wa dini ambao wakati fulani walikuwa wanahubiri na kutoa ujumbe unaohusu uponyaji kwa imani pekee wamebadili ujumbe wao na kuanza kuwahamasisha washirika wao kuzingatia dawa za kupambana na virusi.

Kutatua tatizo kabla halijatokea kunamaanisha kutosubiri mtu fulani aje kushughulikia tatizo. Kuna maanisha pia mhusika kuanza kutafuta ufumbuzi wa tatizo au changamoto kabla changamoto hiyo haijafikia mahali pa kushindikana. Kuhusiana na jambo tunalojadili hapa, hii inamaanisha ya kuanzisha jambo unalodhani linafaa au lina uwezekano wa kuwa suluhisho la madai ya uponyaji wa VVU na UKIMWI kwa njia ya imani pekee mara moja na kwa ujasiri au pasipo kusita.

Uongozi unaweza ukatafsiriwa pia kuwa ni uwezo wa kuwahamasisha wengine kuchukua hatua. Uongozi kwa maana hii ni jambo muhimu sana kwa maendeleo ya mtu mmoja mmoja, mashirika, na jamii. Uongozi wenye mtazamo mpya ni namna ya uongozi ambapo kiongozi ni mwanafunzi, mshauri, na mwalimu. Yeye ni mwanzilishi na mchora ramani. Hahusiki tu na uboreshaji wa mambo kwa kutumia njia, mifumo, misingi na mitazamo iliyopo, lakini anakwenda mbele zaidi kwa kubuni na kuongoza michakato yenye kuibadili miongozo na mitazamo yenyewe.[5]

Uongozi wa Kimageuzi, Uponyaji Mkamilifu na Utetezi katika Kukabiliana na Uponyaji kwa Imani na Uzingatiaji wa Matibabu

Viongozi wa dini wanaweza kufanya utetezi na kusaidia kuleta uponyaji mkamilifu katika muktadha wa VVU na UKIMWI. Masomo yaliyotangulia yametoa maana ya neno utetezi, ambalo kimsingi linamaanisha, "kusimama kwa ajili ya au pamoja na" wahitaji. Uponyaji mkamilifu unamaanisha kuyafanya maisha ya watu wanaoishi na VVU yawe mazuri na yenye ukamilifu/yenye kujitosheleza, maisha huru dhidi ya unyanyapaa na kubaguliwa. Na pia kuwafanya wasiingie kwenye mkumbo wa madai kuhusu uponyaji wa VVU na UKIMWI kimiujiza au kulazimishwa kuachana na matibabu yao. Kufanya utetezi ni kusisitiza uponyaji mkamilifu katika muktadha wa madai ya uponyaji wa VVU na UKIMWI kwa imani pekee kunamaanisha pia yafuatayo:

- Kukubali kuitumia mitazamo ya haki za binadamu ambapo haki za watu wanaoishi na VVU hulindwa na kuheshimiwa. (hii inamaanisha uanzishwaji wa shughuli za ubia na ushirikiano na watu kutoka katika mashirika ya kijamii na wale wenye kushughulikia masuala ya kisheria)
- Kuwahamasisha vijana (makundi yote, wavulana na wasichana) wanaoishi na VVU katika jamii za kidini kuongoza mapambano ya kukabiliana na madai ya uponyaji wa VVU na UKIMWI kwa imani pekee
- Kuwapa wanawake fursa ya kuongoza mapambano dhidi ya changamoto ya baadhi ya viongozi wa dini kusababisha watu wasitishe matumizi ya dawa katika muktadha wa VVU na UKIMWI
- Kuwa kichocheo cha mabadiliko kwa kuwashirikisha viongozi wenzetu wa dini wanaosisitiza uponyaji kwa imani pekee katika mazungumzo yanayoendelea na kuwashawishi kupenda matibabu ya VVU na UKIMWI kwa kutumia dawa za hospitali

5. UNDP, *Leadership Development Strategy Program: The Answer Lies Within* (New York: UNDP, nd), 7. Bold in original.

- Kuunda mahusiano imara na mitandao ya watu wanaoishi na VVU na kuwa na utayari wa kuongozwa, kupewa taarifa na kufundishwa kutokana na uzoefu wao na matarajio yao
- Kutengeneza na kugawa vifaa vya kujifunzia (vya aina tofautitofauti) vyenye kutoa maelezo muhimu kuhusiana na dawa za kupambana na virusi.

Zoezi

Madhumuni ya zoezi: Hadi mwisho wa zoezi hili, washiriki watakuwa wameweza kutambua namna ambavyo wanaweza kuwa viongozi wa kimageuzi ambao wana uwezo mzuri katika kuhamasisha uzingatiaji wa dawa za kupambana na virusi.

Njia za kufundishia: vikundi vidogovidogo, majadiliano ya pamoja

Vifaa vya kufundishia: bangokitita, kalamu za maka

Muda: dakika 30

Mwezeshaji atawagawa washiriki katika vikundi vidogovidogo vya watu wasiozidi sita na kuvisaidia vikundi hivyo kutafakari kuhusu umuhimu wa kutilia mkazo uzingatiaji wa dawa za kupambana na virusi kwa kujadili hoja na maswali yafuatayo:

1. Je, uongozi unafasiliwaje katika lugha yako? Uongozi wa kimageuzi hufasiliwaje?
2. Je, ni mambo gani ambayo wewe unayachukulia kuwa ni sifa za msingi za uongozi zinazohitajika katika kukabiliana na changamoto ya baadhi ya viongozi wa dini ambao wanawavunja moyo baadhi ya watu wanaoishi na VVU ili ama wasianze au wasiendelee na matumizi ya dawa za kupambna na virusi?
3. Je, ni mambo gani ambayo wewe binafsi utayafanya, ili kukabiliana na changamoto za baadhi ya viongozi wa dini ambao ni kikwazo kwa matumizi ya dawa za kupambana na virusi?
4. Onesha hatua utakazozichukua ili kuhakikisha kwamba mfumo wa uongozi/majibu ya changamoto unayoyaamua yanakuwa endelevu?

Viambatisho

Kiambatisho cha 1

Kuwabainisha Wadau na Washirika wa kufanya nao kazi ili Kufanikisha Uponyaji Mkamilifu katika Muktadha wa Madai ya Uponyaji wa Imani Pekee

"Yohana akamjibu, akamwambia 'Mwalimu, tulimwona mtu akitoa pepo kwa jina lako, ambaye hafuatani nasi; tukamkataza, kwa sababu hafuatani nasi. Yesu akasema, Msimkataze, kwa kuwa hakuna mtu atakayefanya mwujiza kwa jina langu akaweza mara kuninenea mabaya; kwa sababu asiye kinyume chetu, yu upande wetu.'" (Marko 9:38-40)

Kuwabainisha wadau na washirika wa kufanya nao kazi ni hatua muhimu ili kuelewa wadau na wabia muhimu wanaoweza kupatikana kwa ajili ya kukabiliana na VVU na UKIMWI, na kujua ni nini wanachohitaji au ambacho tayari wanakifanya chenye uhusiano na jukumu lako la kupambana na VVU na UKIMWI. Ili kufanikisha vizuri zaidi, mchakato huu unapaswa kuongozwa na mkakati jumuishi.

Je, Kuwabaianisha Wadau na Washirika wa kufanya nao kazi ni Nini?

Kupangilia wadau na washirika wa kufanya nao kazi ni mchakato shirikishi unaojumuisha kutafiti, kufanya mazungumzo, na majadiliano yenye kutumia mitazamo na njia mbalimbali ili kupata orodha ya wadau na watu wenye uwezekano wa kufanya nao ubia kutoka katika idadi ya wadau wote waliopo. Kubainisha wadau na washirika wa kufanya nao kazi kunaweza kugawanyika katika hatua kubwa nne:

1. **Utambuzi**: hii hujumuisha uorodheshaji wa makundi yote yanayofaa, taasisi, na watu wanaohusika moja kwa moja na masuala ya VVU na UKIMWI, hata wale ambao hawana uhusiano wa moja kwa moja
2. **Uchambuzi:** ili kuelewa mitazamo ya wadau, na mambo wanayoyapendelea katika kukabiliana na VVU na UKIMWI

3. **Kupangilia ufanyaji kazi:** kupata taswira ya aina ya mahusiano na madhumuni ya wadau wengine
4. **Kuweka vipaumbele**: kuainisha, kutambua kazi zao na kuwapanga wadau kutokana na umuhimu wao kwako.

Zoezi hili la kupangilia wadau na washirika wa kufanya nao kazi ni la muhimu kama vile ilivyo kwa matokeo yake, na ubora wa hatua zake unategemeana sana na maarifa waliyonayo watu wanaofanya zoezi hilo. Kwa kuwa mbinu tuliyoichagua ni mbinu jumuifu yenye kuangalia masuala ya kibiolojia, kisaikolojia, kijamii na kirohokimwili na ya kiroho, ni vema kutafuta wabia kutoka katika makundi mbalimbali. Tunahitaji kuwa na wabia kutoka:

- Fani ya **dawa** na **ufamasia** ili kusaidia katika eneo la matibabu
- Mambo ya **saikolojia** ili kusaidia katika masuala ya ushauri nasaha wa kitaalamu kwa walioathirika na kuathiriwa
- Mambo ya **kijamii** na **kiuchumi** kwa ajili ya kusaidia kutambua na kutatua mahitaji ya kijamii na kiuchumi kwa wale walioathirika au kuathiriwa
- Watu wa **kiroho** ili kusaidia mahitaji ya kiroho ya watu walioathirika au kuathiriwa.

Kutegemeana na madhumuni yako, wadau au wabia wanaofaa kufanya kazi nao wanaweza wasifanye majukumu yao ya kawaida ya kusaidia mambo kuwa endelevu lakini wakasaidia katika mambo mengine muhimu.

- **Kuwa na mchanganyiko**: Hakikisha kuwa kuna mchanganyiko wa wadau wenye utaalamu mbalimbali, kutoka mahali tofauti tofauti, na wenye mbinu tofautitofauti kutoka fani zote. Hii itatoa fursa ya kuwafikia watu wapya na wa zamani, na wadau kutoka makundi kama vile: washawishi, washiriki, watetezi na wabia wa utekelezaji.
- **Jishirikishe katika mambo ya kijamii**: Mitandao ya kijamii husaidia sana kwa kutoa fursa ya kipekee ya kuyatambua na kuyafikia makundi ambayo yalikuwa hayajulikani sana. Tovuti za blogu, majukwaa, mitandao, uchambuzi, na taarifa zinaweza kusaidia kutambua wadau wanaofaa kwa ajili ya kazi yako na kujifunza kuhusu mambo wanayopendelea na yale yenye uhusiano na ya kwako.
- **Kuwa na ufahamu**: Katika zoezi hili la kupangilia ufanyaji kazi, watu wengi wana tabia ya kujikita katika kuangalia mamlaka rasmi pekee, lakini ni vema kukumbuka kwamba si mara zote ambapo watu wanaopaza sauti sana wakawa ndio wadau muhimu. Tafakari na uwaongeze katika orodha yako wadau wasioongeaongea kwa sababu wanaweza wakawa na utajiri wa utaalamu uliofichika.

Uchambuzi wa wanaoweza Kuwa Wabia

Baada ya kuwa umeshaandaa orodha ya wadau, ni vizuri kufanya uchambuzi zaidi ili kuelewa umuhimu wao na michango wanayoweza kutoa, pia ni

muhimu kuelewa namna watakavyoweza kuhusika katika kusaidia uzingatiaji wa matibabu na kufanikisha uponyaji mkamilifu katika muktadha wa VVU na UKIMWI, na kupanga vipaumbele kulingana na umuhimu wao katika kufanya nao kazi.

Orodha ifuatayo ni baadhi ya vigezo vinavyoweza kusaidia kufanya uchambuzi wa wadau wote:

- **Mchango (thamani):** Je, Mdau huyo ana taarifa, ushauri, au utaalamu gani kwenye masuala ya VVU na UKIMWI ambao unaweza kuwasaidia viongozi wa dini?
- **Uhalali:** Je, ni kwa kiasi gani madai ya mdau kutaka kufanya kazi na wewe yana uhalali?
- **Utayari wa kushirikiana:** Je, ni kwa kiwango gani mdau ana utayari wa kushirikiana?
- **Ushawishi:** Je, mdau huyo ana kiwango gani cha ushawishi? (Itabidi ufafanue "ni nani" wanaomshawishi, mfano, kampuni nyingine, Shirika Lisilo la Kiserikali, wateja wao, wafadhili, nk.)
- **Ulazima wa kushirikishwa:** Je, mdau husika anaweza kuharibu au kufanya kazi yako isiwe halali iwapo hatashirikishwa?

Mambo ya kufanya: Tumia vigezo hivyo vitano kuunda na kuijaza chati yenye maelezo mafupi kuhusu namna wadau wanavyoweza kuvifikia au kuvifaulu. Tofautisha viwango vya wadau hao kwa kadri ya kufaa kwao (mdogo, wa kati, au wa hali ya juu). Hizi ni taarifa za awali ambazo zitasaidia kufanya maamuzi kuhusu aina ya wadau wanaofaa kushirikiana nao.

Kupanga Kwa Kuzingatia Vipaumbele Kwa Wale Wanaoweza kuwa Wabia

Kuwapanga wadau kwa kuzingatia vipaumbele ni zoezi lingine muhimu ambalo litasaidia kupunguza hatari ya kuwafuata wadau hali ukijua kwamba kuna uwezekano mdogo wa kufanikisha kufanya ubia nao au kuna uwezekano wa kuwapoteza wale ambao wangefaa zaidi kuwafuata. Baada ya kuwa umeshawatambua wadau, umefanya uchambuzi, na umepangilia namna ya kufanya nao kazi, hatua inayofuata ni kuwapanga kutegemeana na mambo muhimu wanayojishughulisha nayo ukioanisha na mambo ya kipaumbele kwako. Zoezi hili litakufanya uelewe ni mdau gani anafaa kuanza naye kabla ya wengine, au pengine ni nani ambaye hastahili kabisa kufuatwa.

Mambo ya kufanya: Wapange wadau wanaofanya kazi mbalimbali katika jamii yako kwa vipaumbele vyao na umuhimu wao. Namba moja ikionesha chaguo bora zaidi la ubia, na namba tano ikionesha chaguo la ubia lisiofaa kabisa. Maelezo yafuatayo yanaweza kusaidia katika kufanya maamuzi na kuwapanga wadau kulingana na vipaumbele:

1. Je, ni nani kati ya wadau katika jamii yangu anafanya kazi katika eneo la ukatili wa kingono na kijinsia (SGBV)? (upo mtazamo kwamba baadhi ya wanawake wanaweza kuwa ni wahanga au manusura wa ukatili wa kingono na kijinsia kwa kuwa wamekuwa wakitumia dawa za kupambana na virusi na hivyo wanaweza kuwa na uwezekano mkubwa wa kushawishiwa na watu wanaoponya kwa imani ili waachane na mtumizi ya dawa za kupambana na virusi na kufuata uponyaji kwa imani pekee.)
2. Ni nani katika jamii husika hufanya kazi katika eneo la miradi ya uwezeshaji wa akina mama? (Wanawake wengi wameathirika na VVU kwa kuwa hawana namna ya kujikimu na wamejikuta wanaishia kwenye mahusiano yenye kuwaelemea, ambapo wameshindwa kuwa na maamuzi katika masuala ya ngono.)
3. Ni mdau gani katika jamii yangu anafanya kazi katika miradi ya maendeleo? (Umaskini ni jambo mojawapo linalowafanya watu wengi – wanawake kwa wanaume kuwa katika hali hatarishi, vikundi vinavyoshughulika na masuala ya maendeleo vinaweza kuwa ni wabia muhimu katika kuboresha maisha ya watu pamoja na uwezo wao wa kupambana na VVU na UKIMWI.)
4. Je, ni nani anafanya kazi zinazohusiana na masuala ya uzingatiaji wa matibabu kwa watu wanaoishi na VVU?
5. Je, ni nani anafanya kazi katika masuala ya haki za kiuchumi na za kijamii? (Haki za kijamii na kiuchumi ni suala muhimu katika kufanikisha uponyaji mkamilifu katika jamii, makundi ya aina hiyo yanaweza kuwa ni wabia muhimu).

Kwa kutumia maswali hayo makuu, ni rahisi kutambua na kuwapanga wadau kulingana na umuhimu ili kutambua chaguo bora la wale wanaoweza kuwa wadau wa kundi au taasisi yako.

Shughuli: Kuwabaianisha Wadau kwa kuzingatia Muktadha Wako

Madhumuni: Ifikapo mwisho wa shughuli hii, washiriki watakuwa wamefanya zoezi la wadau wanaofaa kufanyaji kazi nao katika mazingira ya jamii zao.

Njia za kufundishia: bangua bongo, vikundi vidogovidogo, majadiliano ya pamoja

Vifaa vya kufundishia: bango kitita, kalamu za maka

Muda: dakika 45

Mwezeshaji atawagawa washiriki katika makundi kwa kuzingatia aina za kazi au fani zao. Makundi hayo yafanye zoezi la kuwabainisha wadau wa kufanya nao kazi katika suala la “Kufanyia kazi suala la Ukatili wa Kijinsia kwa Mtazamo wa Kikristo.” Makundi hayo yafanye ubunifu katika kufanya zoezi hilo katika maeneo yao kama ilivoelekezwa hapo juu.

Kiambatisho cha 2

Je, Teolojia ya Kufuatana Nao ni Nini?[6] Tafakari Fupi

Kwa kutumia mfano Yesu alisema, "Amin, nawaambia, kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi." (Mt. 25:40). Mstari huu una ujumbe mzito sana na unaweza ukawa ni mahali pazuri pa kuanzia kuielewa teolojia ya kufuatana nao. Kwanza, tunaambiwa kwamba walio maskini, wale wasio nacho na waliosahaulika kwenye jamii, na wale waliotengwa au kukataliwa na jamii, wote hao wapo katika familia ya Yesu. Mstari huo unaeleza zaidi na kufafanua kwamba kama vile tunavyoitendea familia hii ya Yesu ndicho kipimo hicho hicho ambacho Yesu anakitumia kujua kama kweli tunamtumikia yeye. Mstari huu pia unanisisitiza kwamba familia nzima ya binadamu ni familia ya Yesu na kwamba ninawajibika kwa mujibu wa ubatizo wangu katika Mwili wa Kristo kuwapenda na kuwatumikia watu wote wanaotokana na uumbaji wa Mungu. Kuwatumikia watu wa Mungu kunaweza kuja katika namna mbalimbali ambapo pengine moja kati ya njia muhimu za kumtumikia ni kufuatana nao. Kwa kufanya hivi tunakuwa tumeunganishwa na Mungu wetu, na Baba yetu, ambaye hutembea pamoja nasi katika mambo yote tunayoyapitia. Mungu hutembea nasi siku zote, na sisi kama Wakristo, tumeitwa kutembea pamoja na wale wote wanaoweza kuwa wanahitaji uwepo wetu.

Kutembea Pamoja

"Kutembea pamoja" ni kauli picha muhimu kuhusu umuhimu wa usawa na kupendana, na ni uthibitisho wa agano la Kiaskofu la ubatizo wa Kanisa. Linamtaka kila mmoja wetu "kumtafuta na kumtumikia Kristo ndani ya watu wote, na kumpenda jirani yako kama unavyojipenda mwenyewe" na "kujitahidi kuwa na amani na haki na watu wote, pamoja na kuheshimu utu wa kila binadamu" (*Kitabu cha "Common Prayer*," uk. 305). Dhana inayojitokeza hapa kwamba Mungu Baba ambaye ni mkamilifu anaamua kutembea hatua kwa hatua na watoto wasio wakamilifu na ambao hawajapevuka katika jamii inanifanya nione ni dhana muhimu katika teolojia hii ya kufuatana nao. Hii inamaanisha kwamba ni lazima tuchague "kufuatana na" watu ambao pengine

6. Imechukuliwa toka kwa Lelanda Lee, *The Theology of Accompaniment and Asset Based Community Development*, inapatikana kwenye mtandaokupitia http://faith.episcopal.co/wp-content/uploads/2016/02/Theology-of-Accompaniment-and-ABCD-Essay.pdf (ilisomwa tarehe 11 July 2018).

hata hawaelewi umuhimu wa kufuata amri ya Yesu ya kuwapenda jirani zao kama wanavyojipenda wao wenyewe. Wakati mwingine, watu hudhani wanahitaji kuwa peke yao, pale ambapo katika hali halisi wanafikiri kwamba hakuna mtu ambaye angependa kuwa nao, hata hivyo, tunapochagua kuwa na watu wa aina hii, tunachangia katika kuwaletea furaha na utoshelevu katika maisha yao. "kutembea pamoja na" watu wa aina hiyo huwafanya watambue na kujiona kwamba wao pia ni sehemu ya jamii. Si kwamba "tunatembea kwa ajili" yao isipokuwa inamaanisha "kutembea pamoja" nao.

"Kutembea pamoja" ina maanisha kuwatendea wengine vile ambavyo sisi tungependa tutendewe, kwa sababu Kristo anatarajia tuwe hivyo. Katika dini duniani kote, falsafa au mtazamo huu hujulikana kama Amri Kuu: "Watendee wengine kama vile ambavyo wewe ungependa kutendewa." "kutembea pamoja" kunaanza na kila mmoja kuwa pamoja na mwenzake, kuwa na muda wa kukaa pamoja, kubadilishana uzoefu wa kwenye jamii, na kushirikishana simulizi za kila upande. Uwepo wa kila mmoja kwa mwenzake husaidia kuanza kwa mazungumzo ambapo tunaweza kuzungumzia na kupeana matumaini na kushirikishana ndoto zetu, pia kushirikishana mashaka na hofu zetu, na kusikiliza yale ambayo kaka na dada zetu wanasema. Kwa maneno mengine mtu anaweza kusema "kutembea pamoja na" inatuelekeza kwenye teolojia ya ukarimu yenye kumuona mgeni ni – "mtu asiyetuhusu"– kuwa ni kama mtu anayejaza nyumba au nafasi. Wao ni sisi na sisi ni wao. Hakuna tofauti yoyote kati ya wao na sisi; wote tunapendwa katika hali ya usawa machoni pa Muumba. "Kutembea pamoja" kunajumuisha aina fulani ya kusafiri pamoja, kupitia hali ngumu au nyepesi, katika furaha au matukio ya kusherehekea, na katika hali ya maumivu ya moyo na huzuni. Suala muhimu ni kung'ang'ania kuwa pamoja na kushikamana, kwa kuwa wale ambao wako pamoja wanaipenda jumuiya moja na ni watu ambao wana mambo wanayoyapenda na pia wana matatizo yao.

Uelewa huu wa teolojia ya Kufuatana nao unaonesha kwamba katika historia nzima ya biblia, suala hilo limejitokeza kama sehemu muhimu ya dini na maisha ya wana wa Isreli pamoja na maisha ya watu wa kanisa el kwanza. Mungu alitembea na Abrahamu pale alipokuwa akisafiri kuelekea nchi ya ahadi. Ingawaje Musa alikuwa akiishi kwa amani katika jumba lake la kifalme, yeye alichagua "kutembea pamoja na wana wa Israeli wakiwa watumwa" Katika safari yao kuelekea kupata uhuru. Manabii, akina Eliya, Elisha, Amosi, Mika, Hosea and Isaya na wengine wengi walifuatana pamoja na watu maskini na watu wa Israel walioonewa. Hata misafara ya Yesu kama inavyoelezwa na Yesu mwenyewe ilikuwa ni misafara ya kufuatana nao, Yesu "anatembea na" wale watu ambao walikuwa ni wahanga wa utawala wa Kirumi. Hata Paulo anatembea pamoja na mataifa huku akipanda na kufungua kanisa moja baada ya jingine. Uimara wa kanisa hutokana na kuitumia nafasi yake kama wanaharakati na kama taasisi yenye kutembea pamoja na watu wote. Kanisa hufuatana na mtu tangu pale anapozaliwa mpaka pale anapoingia kaburini. Teolojia ya kufuatana nao imeletwa kwetu na watangulizi wetu katika Biblia na Mungu anatufanya sisi tutambue umuhimu wa kufuatana nao. Kufuatana nao kutatufanya sisi tuwe

sehemu ya jamii na pale inapotokea hakuna yeyoye anayefuatana na sisi, tutajiona kama ni watu ambao tumekataliwa na jamii. Watu wanaoishi na VVU na wale ambao wameathiriwa na VVU na UKIMWI, kwa muda sasa wamefanywa kuwa ni watu wasio na watu wa kufuatana nao, na hivyo kuwafanya wao kuwa si wanafamilia ya Mungu. Kutokuwa na yeyote wa kufuatana naye yaweza pia hata kusababisha msongo wa mawazo na huzuni kwa kujiona kuwa hawakubaliki.

Uwepo, na Namna ya Kuzuia Misaada ya Hatari

Teolojia ya kufuatana nao – "kutembea pamoja"– pia inajumuisha huduma ya uwepo, ambapo, tunapokuwa mahali ili tu tuwe pamoja na mtu mwingine au kuwa pamoja na jamii fulani, kuwepo mahali, kusikiliza, kuwa wasikivu, na "kutofanya chochote." Hilo ni jambo gumu kidogo kwa walio wengi, ambao wanajiona kuwa tayari wao wanatoa misaada na tayari wanasaidia. Ni jambo gumu zaidi kwa mashirika ya huduma za kijamii ambayo yameundwa kwa kanuni kwamba wao ni "mashirika ya kusaidia." Hata kama "tunafanya jambo fulani" kwa ajili ya wengine, ni muhimu kujizuia kuchukua "misaada ya hatari," yaani, kumfanyia kazi mtu mwingine ambaye yeye ndiye hubeba sifa kuhusu zawadi zao na uwezo wa kufanya mambo wao wenyewe. Jambo hili lina ukweli zaidi kwa watu wanaoishi na VVU au wale ambao wameathiriwa. Kuwa katika hali hizo za kiafya hakumaanishi kwamba hawana uwezo wa kujihudumia. Hali walizonazo zinaweza kumaanisha kwamba wanakosa marafiki au watu ambao wana utayari hata tu wa kukaa au kushinda nao, watu ambao wako tayari kuwasikiliza. Sisi kama viongozi wa dini, tunayo fursa nzuri zaidi kimkakati kwa kuwa tuna wahudumia kwa njia rahisi ya uwepo wetu, au kuwepo tu pale.

Binafsi, nikiwa kama mtu aliyesomea mambo ya uchumi na masuala ya benki, ninatambua tofauti zilizopo kati ya uchumi wa Mungu na ule wa wanadamu. Katika uchumi wa Mungu, mara zote kuna utoshelevu; kile ambacho hutolewa mara zote huwa kinajitosheleza. Hii inatofautiana kabisa na uchumi wa kibinadamu ambapo mara nyingi huwa tunashuhudia tukio moja baada ya jingine yanayoashiria kutokuwa navyo, inakuwa kama hatuna vitu vyote tunavyovihitaji, na wakati mwingine tunahisi kuogopa kuwa wahanga wa hali ya kutokuwa navyo au mambo ambayo tunaamini kwamba tunayakosa. Maandiko, yanatufumbua macho yetu kuuona utajiri ambao Mungu ameuumba na kumpa mwanadamu, na tunaalikwa kujenga tabia ya kushukuru na kuwashirikisha wengine utajiri na utoshelevu wa Mungu. Mungu anatualika katika uchumi ambamo shukrani ndio mahali pa kuanzia na fadhila ni sawa na fedha inayotuweka huru dhidi ya hali ya woga. Katika namna inayofanana na hiyo, mbinu ya kutumia rasilimali zilizopo kwenye jamii kwa ajili ya maendeleo inatutaka kuwa watu wenye shukrani kwa ajili ya rasilimali tulizonazo kwenye jamii zetu na kuziinua na kuwashirikisha wengine katika kuzitumia rasilimali hizo pamoja na wengine kwa manufaa ya jamii nzima. Shukrani ndio mahali pa kuanzia – kutambua pamoja na wanajamii wengine kwamba tuna kila kitu tunachokihitaji kwa ajili ya kujiimarisha sisi wenyewe kama jamii.

Katika kitabu chake, kiitwacho *Toxic Charity* (HarperOne, 2011,), Robert D. Lupton ameandika kuhusu umuhimu wa kufanya ubia na kutambua uwezo wa watu na jamii ili kujifunza kutumia kazi zao wenyewe kuboresha jamii zao. Hii ni tofauti na iwapo kama tungetegemea mashirika ya misaada kuja kusaidia na rasilimali zao pasipo hata kutambua uwepo wa rasilimali na vipaji vilivyo ndani ya jamii hizo. Katika sura ya tano ya Injili ya Yohana, Yesu anafanya jambo ambalo ni kama kinyume cha utoaji wa hatari kwa kumponya mtu mmoja ambaye alikuwa mgonjwa kwa muda wa miaka 38 akimwamuru "inuka, jitwike godoro lako na uende." Angalia pia namna ambavyo Yesu alivyoanzisha mazungumzo kwa kumuuliza mgonjwa, "Je, unataka kuwa mzima?" Yesu anajihusisha na usikivu mtakatifu na hakuna jambo ambalo analichukulia kwamba litatokea tu kuhusiana na matamanio ya mwanadamu. Yule mtu akamjibu Yesu, "Bwana, mimi sina mtu wa kunitia birikani, maji yanapotibuliwa; ila wakati ninapokuja mimi, mtu mwingine hushuka mbele yangu." Kanuni za kutumia raslimali zilizopo kwenye jamii kwa ajili ya maendeleo zinatufundisha kuhusu umuhimu wa kushughulikia mahitaji ya jamii. Kuwa na utayari wa kufuatana nao katika safari yao kuelekea kujitambua wenyewe kuhusu vipawa walivyonavyo na vile vilivyoko katika jamii zao ni njia nzuri kuelekea kuweka katika vitendo vipawa hivyo na kujiwezesha. Katika muktadha wa VVU na UKIMWI, kufuatana nao kunajumuisha uelewa kwamba kuishi na VVU hakubadili ukweli kwamba watu wote wameumbwa kwa mfano wa Mungu na kwamba tumeitwa ili wakati wote tuwe tayari kuwasaidia watu wote, hasa wale ambao wanasumbuka kutokana na unyanyapaa na ubaguzi. Jambo ambalo wengi kati ya watu hawa wanahitaji zaidi, ni kwa wao kuendelea kuwa sehemu ya jamii na kuwa na jamii fulani na marafiki ambao wanaweza kufuatana nao katika safari yao.

Simulizi Hutuunganisha

Kama vile ambavyo Yesu alivyotumia mifano kuwafundisha wanafunzi wake na watu wengine waliokuja kumsikiliza, usimuliaji wa mambo yetu binafsi na yale ya kifamilia au jamii zetu kwa watu wengine ni njia ya msingi sana na ni kama utambulisho wa Ukristo wetu na wa kanuni zinazoongoza mbinu ya kutumia rasilimali zilizopo katika jamii kwa ajili ya maendeleo. Utamaduni wetu ambao ni mchanganyiko wa Uyahudi na Ukristo (Judeo-Christian) umejaa usimuliaji wa mambo kama njia ya kufundisha jamii, ukiangalia Biblia kuanzia kwenye mifano ya mafumbo ya Yesu kwa Wayahudi mpaka sikukuu ya Wayahudi kabla ya Pasaka na hata kufikia ekaristi kwa Wakristo kukumbuka karamu ya mwisho. Kanuni za kutumia rasilimali zilizopo katika jamii kwa ajili ya maendeleo pia huhusisha matumizi ya simulizi za mambo au matukio kwa njia ya kuwaalika watu kutoka kwenye jamii ili kutoa simulizi zao kupitia mazungumzo ya ana-kwa-ana (usaili). Simulizi hizi – simulizi zetu – zinatuunganisha na wanadamu wengine na kutuonesha namna ambavyo mambo yetu yanavyofanana na ambavyo tuna vipawa vingi ambavyo kila mtu anaweza kutoa kwa jirani yake. Hatua zilizopo kwenye mbinu ya kutumia rasilimali zilizopo katika

jamii kwa ajili ya maendeleo pia zinatuonesha namna tunavyoweza kujiungamanisha na vipawa vyetu kila mtu kwa mwenzake kwa ajili ya mafanikio yetu wote. Tukiwa kama viongozi wa kiimani, tutakuwa tumefanya vema sana iwapo tutajitoa na kusikiliza kutoka kwa watu ambao maisha yao yameathiriwa na VVU na UKIMWI na katika hilo tukawa tumeanza kufuatana nao, tunaweza tukawashirikisha simulizi zetu binafsi namna ambavyo wakati fulani tulitamani kufuatana nao pale ambapo tulijisikia kutengwa na kukataliwa. Kuwashirikisha uzoefu unaoshahibiana na ule wa kwao na namna ambavyo sisi tulifutana au kuandamana na watu fulani inaweza kuleta matokeo makubwa kwa kuwafanya wale ambao tunafuatana nao waone kwamba wapo katika njia sahihi ambayo wengi wameipitia.

Kuanzia mtoto mdogo kabisa mpaka mtu mzima kabisa, kuanzia mbumbumbu hadi mwenye elimu ya juu kabisa, bila kujali lugha yake; kusimulia mambo au matukio ni kitu ambacho kila mmoja anao uwezo wa ndani wa kukifanya. Wanaweza wakasimulia kwamba wao ni akina nani, wanatokea wapi, ni nani aliyechangia kuwafanya wawe hivyo walivyo, na ni nini wanachokitamani au kuwa na ndoto nacho wao binafsi na pamoja na jamii zao. Masimulizi ni suala la kila siku katika maisha ya watu wanaoishi katika falsafa ya kibantu ya *ubuntu*, ambayo mara nyingi hueleza kwamba "Mimi niko ndani yako, na wewe upo ndani yangu," au "mimi nipo, kwa sababu wewe upo." Simulizi zetu zinaelezea sisi ni akina nani hutengeneza vitu vinavyotuunganisha ambavyo tunaweza kuvichukua na kujenga uelewa wa pamoja na wa kila mtu na mwenzake. Tunafanyika kila mmoja kuwa simulizi ya mwenzake pale tunaposikia simulizi zao na sisi tunapoanza kujiona katika simulizi zao kwa sababu ya ubinadamu ambao unatuhusu sote–pale ambapo tunavutwa na mambo tunayoyasikia, tunashiriki hisia za mtu anayesimulia na wahusika wengine kwenye simulizi, na tunaanza kutamani kufanya jambo fulani ili kumsaidia msimuliaji na watu wengine wenye mambo yanayofanana na ya msimuliaji. Kwa kadri tunavyosikia simulizi nyingi na kuwashirikisha wengine, ndivyo kadri tunavyozidi kutambua kwamba sisi sote tu sehemu ya simulizi moja tumeumbwa na Mungu muumbaji, Mungu mwandani wetu, na Mungu mpatanishi wetu.

Kiambatisho cha 3

Ukurasa Kuhusiana na Ukweli kuhusu Wenza Wenye Hali Mchanganyiko[7]

Je, Nini Maana ya "Wenza Wenye Hadhi Mchanganyiko"?

Hii hutokea pale ambapo mwenza mmoja hana VVU na wakati mwenzake amethirika.

Kupima VVU na Ushauri Nasaha kwa Wanandoa

Kupima VVU pamoja na kupata ushauri kwa pamoja na mwenza wako inaweza kusaidia yafuatayo:

- Kuwarahisishia wenza kuweka wazi majibu yao ya vipimo vya VVU kila mmoja kwa mwenzake
- Inakusaidia kuchukuliana na hali halisi iwapo mmoja kati yenu au wote wawili mmeambiwa mmeathirika
- Inasaidia katika kuweka mipango ya baadaye na kuchukua jukumu la pamoja.

Vidokezo Kuhusu Ngono Salama

Wenza wenye hali mchanganyiko wana uwezo wa kuwa na mahusiano salama ya kimapenzi iwapo watafuata ushauri ufuatao:

- kuzungumza kuhusu kuzuia VVU na uzazi wa mpango kwa pamoja kama wenza, pamoja na mtaalamu wa afya.
- kutumia kondom kila mara unapofanya ngono.
- kuamua aina ya matibabu ya VVU wanayoona yanafaa.

Matibabu ya VVU kwa Mwenza Aliyeathirika na VVU

- Dawa za kupambana na virusi zinaweza kupunguza kiwango cha VVU mwilini mwako.
- Dawa hizi zinaweza kupunguza kiwango cha virusi kufikia kiwango cha chini sana (hadi kutoonekana), na hivyo kupunguza uwezekano wa kumuambukiza VVU mtu mwingine.
- Unatakiwa uanze matibabu ya VVU mara tu baada ya vipimo. Hii itasaidia kupunguza virusi mwilini mwako na kuzuia maambukizi kwa mwenza wako.
- Omba ushauri kutoka kwa mhudumu wa afya kuhusiana na kuanza matibabu.

---

7. Kipeperushi cha AVERT, *HIV and Mixed-Status Couples*, Kipeperushi, Kinapatikana kwenye mtandaoni kupitia; www.avert.org/learn-share/VVU-fact-sheets/serodiscordant-couples kilinukuliwa tarehe 11 Julaik 2018.

Matibabu ya VVU kwa mwenza ambaye hajaathirika na VVU

- Matibabu anayopata mwenza ambaye hajaathirika na VVU huitwa "pre-exposure prophylaxis (PrEP)." Dawa hii inashauriwa kutumiwa na wenza wenye hali mchanganyiko.
- Humsaidia mtu ambaye yupo katika mazingira ya kupata VVU kuzuia asipate maambukizi.
- Dawa za PrEP hazipatikani kwa urahisi, hivyo inawezekana zikawa hazipatikani mahali ulipo.

Mpango wa uzazi

- Ni muhimu kwako kupanga kuhusiana na ujauzito ili kumlinda mwenza wako pamoja na mtoto dhidi ya VVU.
- Mshauri wako wa afya anaweza kukupa maelekezo kuhusiana na huduma hizo.

Chaguzi za mimba

Inawezekana ukapata mtoto ambaye hana maambukizi ya VVU kwa kuweka mipango makini. Njia ya kupata ujauzito itatofautiana kwa kutegemeana na kwamba ni mwenza yupi ambaye ameathirika VVU.

Njia ya upandikizaji

- Upandikizaji humkinga mwenza wa kiume ili asiathirike kutokana na majimaji ya mwili yanayotoka kwa mtu mwenye maambukizi ya VVU. Katika njia hii, shahawa za mwanaume huingizwa katika uke wa mwanamke kwa njia ya sindano. Unaweza ukafanya hii nyumbani kwako wewe mwenyewe, lakini ni muhimu kuzingatia ushauri wa daktari.
- Upandikizaji hufanya kazi vizuri zaidi wakati ambapo mwanamke yupo katika kipindi ambacho yai moja au zaidi limeachiwa kutoka kwenye moja ya ovari (yai kupevuka). Upevukaji wa yai hutokea takribani siku 14 baada ya mwanamke kuingia katika mzunguko wake wa hedhi.
- Upevukaji wa yai hutofautiana kati ya mwanamke mmoja na mwingine, ni vizuri ukapata ushauri wa daktari wako.

Njia ya Kutenganisha Mbegu za Kiume

Majimaji yaitwayo "Shahawa" ni ute unaotoka katika uume wa mwanaume pale anapopizi. Ute huu ni mchanganyiko wa mbegu za kiume na majimaji mengine yanayoitwa shahawa.

- Shahawa ambayo imeathirika na VVU haiwezi kusababisha maambukizi kwa mtoto wako bali unaweza kumuambukiza mwenza wako.

- Utenganishaji wa mbegu za kiume ni utaratibu ambao hutumika kwa namna ambayo mbegu za kiume zisizo na VVU hutenganishwa kutoka katika shahawa' kutoka kwa mtu mwenye maambukizi ya VVU.
- Mbegu za kiume ambazo hazina VVU zinaweza kuwekwa katika uke mwa mwanamke kwa njia ya kupandikiza ili kuondoa hatari ya kuambukizwa VVU.
- Mbegu za kiume zilizotenganishwa zinaweza pia zikatumika katika kurutubisha yai la mwanamke kupitia njia iitwayo "in vitro fertilization (IVF)."
- Njia nyingine ya kuzuia maambukizi ni kwa kutumia mbegu za kiume kutoka kwa mtu asiye na maambukizi ya VVU ambaye hujitolea mbegu zake.
- Upatikanaji wa huduma za kutenganisha shahawa na IVF unaweza ukawa ni mdogo katika baadhi ya maeneo.

Vinginevyo, ngono ya bila kutumia kinga kwa kufanya mahesabu ya muda inaweza pia isisambaze VVU kwa mwenza wa kike, iwapo kama mwenza wa kiume atakuwa na:

- Uwingi wa virusi vya UKIMWI ambao haujagundulika kwa miezi sita
- Uzingatiaji mzuri wa matibabu
- Hana maambukizi ya magonjwa ya zinaa.

Ni vizuri pia kupata ushauri wa daktari kabla hujachukua maamuzi yoyote.

Matibabu ya VVU na Ngono ya Bila Kutumia Kinga kwa Kufanya Mahesabu ya Muda

Aina zote mbili za wenza ambao wapo kwenye kundi la "serodiscordant" wanaweza kutumia matibabu ya VVU na kupata ujauzito kwa njia za asili.

- Mwenza mwenye maambukizi ya VVU anaweza kutumia matibabu ya VVU na kuendelea nayo ili kupunguza kasi ya nguvu au kiwango cha virusi alichonacho.
- Mwenza ambaye hana maambukizi ya VVU anaweza akatumia PrEP kabla ya kufanya ngono bila kinga katika mazingira fulani (hapa kutakuwa na hatari ya kuambukizwa VVU).
- Wenza wote wawili wanapaswa kupima afya na kupata matibabu ya magonjwa ya zinaa ili kupunguza hatari ya kuambukiza VVU.
- Wenza wanapaswa kufuatilia viwango vya virusi walivyonavyo kwa umakini iwapo wataamua kufanya ngono pasipo kinga.
- Wenza wafanye ngono bila kinga pale tu mwenza wa kike atakapokuwa kwenye kipindi ambacho yai limepevuka.
- Ngono isiyo na kinga bado ina hatari ya kuambukiza VVU kwa mtu asiyeathirika.

Fahamu Haki Zako

Una haki ya:

- Kuomba au kukataa kufanyiwa kipimo cha VVU
- Kukataa matibabu ya VVU
- Kuchagua iwapo unahitaji, namna gani, na wakati gani upate ujauzito.

Ukurasa Unaoelezea Ukweli kuhusu Kifua Kikuu na VVU

World Health Organization

Taarifa za 2009, Ukweli kuhusu KIFUA KIKUU

- Kifua Kikuu ni ugonjwa wa kuambukiza na **huenezwa kwa njia ya hewa**. Ikiwa hautatibiwa, kila mtu mwenye ugonjwa wa Kifua Kikuu huwaambukiza kwa wastani watu 10 hadi 15 kila siku.
- Ziadi ya **watu bilioni 2**, sawa na theluthi moja ya watu wote duniani, wameambukizwa kirusi cha Kifua Kikuu, kimelea ambacho kinasababisha Kifua Kikuu. 1 kati ya watu 10 ambaye ameambukizwa kirusi cha Kifua Kikuu ataugua ugonjwa wa Kifua Kikuu wakati fulani katika maisha yake.
- Kifua Kikuu ni **ugonjwa wa umasikini** unaowaathiri zaidi vijana katika umri wao wa uzalishaji. Vifo vingi vya Kifua Kikuu vipo kati nchi zinazoendelea, na zaidi ya nusu ya vifo hutokea Asia
- Kulikuwa na **kesi mpya za Kifua Kikuu milioni 9.4** mwaka 2008 (milioni 3.6 kati yao ni wanawake) ikiwa ni pamoja na kesi milioni 1.4 miongoni mwa watu wanaoishi na VVU.
- Watu **milioni 1.8** walikufa kwa Kifua Kikuu mwaka 2008, ikiwa ni pamoja na watu 500,000 wenye VVU – sawa na vifo 4500 kwa siku
- Kiwango cha matokeo ya athari ya ugonjwa kimataifa kilishuka hadi kufikia **kesi 139 kwa watu 100,000** mwaka 2008 baada ya kuongezeka mwaka 2004 kwenye kesi 143 kwa watu 100,000. Viwango **vinashuka taratibu sana** katika kanda 5 za WHO (kiwango hiki kinaimarika Ulaya). Idadi kamili ya kesi bado inapanda kwa sababu ya ongezeko la watu.
- Kulikuwa kuna **taarifa milioni 5.7 za kesi za Kifua Kikuu** mwaka 2008. **Watu milioni 36 walitibiwa** katika programu za DOTS (kati ya mwaka 1995 – 2008), na vifo takribani milioni 8 vilizuiwa
- **Kiwango cha mafanikio ya kutibu cha 87%** kilivuka lengo la 85% kwa mara ya kwanza tangu lengo hilo kuwekwa mwaka 1991. Nchi 53 zilivuka lengo hili la kutibu wagonjwa kwa 85%.
- **Kifua Kikuu ni ugonjwa unaoongoza kuua watu wenye VVU.** Watu ambao wana maambukizi ya VVU na wameambukizwa Kifua Kikuu wana uwezekano wa kuugua Kifua Kikuu kwa zaidi ya mara 20 hadi 40 kuliko watu ambao hawana maambukizi ya VVU wanaoishi katika nchi hiyo hiyo
- Suala muhimu katika kuokoa maisha ni kutekeleza kwa haraka **mambo makuu matatu** (kutafuta kesi kulikoimarishwa zaidi, matibabu ya kuzuia ya Isoniazid, na udhibiti wa maambukizi) – ya hatua ambazo zinapunguza mzigo wa Kifua Kikuu kwa watu wanaoishi na VVU
- **Kifua Kikuu Kinachopinga Dawa Nyingi** (MDR-TB) ni aina ya Kifua Kikuu ambacho ni vigumu na aghali sana kukitibu na hushindwa kuitikia dawa za awamu ya kwanza. Kifua Kikuu kinachokataa dawa kabisa (XDR-TB) hutokea ambapo upinzani kwa dawa za awamu ya pili unaongezeka na kuwa juu ya MDR-TB
- **5% ya kesi zote za Kifua Kikuu zina MDR-TB,** kutokana na data zilizokusanywa katika zaidi ya nchi 100 katika muongo uliopita
- Kulikadiriwa kuwa na **kesi mpya 500,000 za MDR-TB** mwaka 2007. Zaidi ya 1% ya kesi zilikuwa zinapokea matibabu mwaka 2008 yaliyozingatia viwango vilivyopendekezwa na WHO.
- Mwaka 2018, WHO iliripoti kwamba **viwango vya juu kabisa vya MDR-TB vilivyowahi kurekodiwa**, kwa kiwango cha juu cha hadi 22% ya kesi mpya za Kifua Kikuu, vilikuwa katika baadhi ya maeneo ya Umoja wa Soviet. Katika ukanda huo huo, 1 kati ya kesi 10 za MDR-TB ni XDR-TB
- **Nchi 27 zinafanya jumla ya 85% ya kesi zote za MDR-TB**. Nchi tano zenye idadi kubwa ya kesi hizi ni India, China, Shirikisho la Urusi, Afrika Kusini na Bangladesh. Hadi sasa XDR-TB imegundulika katika nchi 57.
- Waka 2009, **maazimio ya Mkutano Mkuu wa Kimataifa wa Afya kuhusu MDR-TB na XDR-TB** yaliungwa mkono na Mataifa Wanachama wa WHO 192 na yalijumuisha hatua za kipaumbele zilizopendekezwa ili kushughulikia Kifua Kikuu kinachokataa dawa

MALENGO YA KIFUA KIKUU KWA MWAKA 2015

Malengo ya Maendeleo ya Milenia ya Umoja wa Mataifa:
kuzuia na kuanza kuuhafifisha ugonjwa huu

Tathmini ya sasa
Malengo yametimia katika kanda zote za WHO ingwa ugonjwa bado unafifia taratibu

Malengo ya Stop TB Partinership:
kupunguza kuenea kwa ugonjwa huu na vifo hadi nusu yake kufikia mwaka 2015 kwa kulinganisha na mwaka 1990

Tathmini ya sasa
WHO Afrika hawajafikia lengo

Ikiwa mpango wa Kimataifa wa Kuzuia Kifua Kikuu 2006 – 2015 utafadhiliwa kikamilifu na kutekelezwa maisha ya watu milioni 14 yataokolewa na watu milioni 50 watatibiwa

Idara ya Kuzuia TB ya WHO pamoja na ofisi za kikanda na za nchi: hutengeneza sera, mikakati na viwango; husaidia jitihada za Nchi Wanachama wa WHO; hupima maendeleo ya kufikia malengo ya Kifua Kikuu na hutathimini utendaji wa programu ya kitaifa, hufadhili na kuwezesha; huhimiza utafiti; na huwezesha ushirikiano, uenezi na mawasiliano

Stop TB Partnership (ikiwa na sekretarieti yake inayofadhiliwa na WHO) ni mtandao wa zaidi ya washirika 1000; una Bodi ya Uratibu na makundi 7 yanayofanya kazi: DOTS Upanuzi; Mradi wa Maabara ya Kimataifa; MDR-TB; Kifua Kikuu/VVU; Dawa Mpya; Upimaji Mpya wa Magonjwa; Chanjo Mpya

Kiambatisho cha 5

Tiba ya Dawa za Kupambana na Virusi (ART)

Dawa za Kupambana na Virusi ni Nini?

Dawa za Kupambana na Virusi ni aina ya dawa zinazotibu VVU. Dawa hizo haziui wala kutibu virusi. Hata hivyo pale zinapotumika kwa kuzichanganya zinaweza kuzuia ukuaji wa virusi. Pale virusi vinapopunguzwa nguvu, ndivyo hivyo pia VVU inapunguzwa nguvu. Dawa za kupambana na virusi zinajulikana kama ARV. Mchanganyiko wa tiba ya ARV (ART) inachukuliwa kuwa ni dawa ya kupambana na virusi yanye ufanisi sana (HAART).

Je, Mzunguko wa Uhai wa VVU ni Nini?

1. Virusi huru huzunguka katika mfumo wa damu.
2. VVU vinajiambatanisha kwenye seli.
3. VVU vinatoa vinasaba vyake na kuingia kwenye seli.
4. Vinasaba vya VVU (RNA) hutumika kurejesha aina nyingine ya kimeng'enya ili kujenga vinasaba vya VVU.
5. Vinasaba vya VVU huingizwa kwenye kromosomu za seli kupitia vimeng'enya vipyaa vyenye VVU vilivyozalishwa. Hali hii husababisha maambukizi ya VVU kwenye seli.
6. Wakati seli zenye maambukizi zinapojizalisha, huhuisha Vinasaba vya VVU, ambavyo hutengeneza vitu vingine ghafi kwa ajili ya kutengeneza virusi vipya vya VVU.
7. Mrundikano wa vinasaba hukusanyika pamoja na kutengeza virusi vipya.
8. Virusi ambavyo havijapevuka hujitoa nje ya seli zenye maambukizi kupitia mchakato unaoitwa "kuotea."
9. Virusi ambavyo havijapevuka hutoka na kuwa huru nje ya seli zilizoathirika.
10. Virusi vipya vinapevuka: mali ghafi hukatwa kwa kimeng'enya cha protease na vinajikusanya na kutengeneza virusi vingine vyenye nguvu.

Je, Dawa Zilizoidhinishwa ni zipi?

Kila aina, au "kundi," la dawa za ARV zinashambulia VVU kwa namna tofauti. Kundi la kwanza la dawa za kuzuia VVU lilikuwa ni lile linaloitwa "nucleoside reverse transcriptase inhibitors" (zinajulikana pia kama NRTIs au "nukes"). Dawa hizi huzuia hatua ya 4 katika mzunguko wa uhai wa VVU, ambapo vinasaba vya VVU hutumika kutengeneza DNA kutoka katika RNA.

Dawa ya "Non-nucleoside reverse transcriptase inhibitors," pia huitwa "non-nukes" au qqNNRTIs pia huzuia hatua ya nne lakini katika namna tofauti.

Dawa ya "Protease inhibitors" au PIs, huzuia hatua ya kumi, ambapo mali ghafi kwa ajili ya virusi vipya vya VVU hukatwa katwa katika vipande.

Dawa ya Entry inhibitors huzuia VVU visiingie kwenye seli kwa kuzuia hatua ya 2 katika mzunguko wa maisha ya VVU.

Dawa ya VVU ya "integrase inhibitors" huzuia VVU ili visingize "genetic code" zake katika mfumo wa binadamu wa "cell's code" katika hatua ya tano ya mzunguko wa uhai wa VVU.

Ni kwa Namna Gani Dawa Hizi Zinatumika?

Mara nyingi Dawa za Kupambana na Virusi hutumika kwa kuchanganywa na dawa nyingine tatu au zaidi kutoka katika makundi zaidi ya moja. Hii huitwa "Tiba Mchanganyiko." Tiba Mchanganyiko husaidia kuzuia upinzani.

Watengenezaji wa ARV wanaendelea kuziboresha dawa zao ili ziwe rahisi kuzimeza, na wamezichanganya baadhi kuwa katika matibabu ya kidonge kimoja.

Je, ni Nini Maana ya Dawa Kutofanya Kazi?

Pale VVU vinapokuwa vingi, nakala na aina mpya za virusi huzaliwa: hivi vinakuwa tofauti kidogo na vile virusi vya awali. Baadhi ya virusi vipya vinavyozaliwa huendelea kuongezeka hata pale unapotumia dawa za ARV. Suala hili linapotokea, virusi vinakuwa na uwezo wa kuwa na nguvu ya kutosikia dawa na dawa za kupambana na virusi zinaweza kuacha kufanya kazi. Angalia ukurasa wa maelezo namba 126 ulioambatanishwa kwa maelezo zaidi.

Iwapo kama dawa ya ARV moja au mbili pekee zitatumika, itakuwa rahisi kwa virusi kutengeneza nguvu ya kujilinda na kutosikia dawa. Ni kwa sababu hii, hatushauri kutumia dawa ya aina moja au mbili tu. Lakini iwapo utatumia dawa tatu, virusi vipya vitakavyofanikiwa vitatakiwa "kukumbana na" dawa zote kwa wakati mmoja. Matumizi ya tiba mchanganyiko yanamaanisha kwamba itachukua muda zaidi kwa virusi kutengeneza mfumo wa upinzani.

Kuzingatia ARV ni muhimu sana ili matibabu yaweze kufanya kazi. Kipimo cha kuangalia idadi ya virusi hutumika katika kuangalia iwapo dawa za ARV zinafanya kazi

Je, ni hatua gani inayofuata?

Dawa mpya bado zinaendelea kufanyiwa utafiti katika madaraja au makundi yote yaliyopo. Watafiti pia bado wanaendelea kutengeneza dawa mpya, ambazo zitazuia baadhi ya hatua katika mzunguko wa maisha ya VVU, pamoja na dawa ambazo zitaimarisha mfumo wa mwili wa kujilinda.

Kiambatisho cha 6

Ratiba ya Mafunzo Inayopendekezwa kwa Wawezeshaji

Muda	Siku ya Kwanza	Siku ya Pili	Siku ya Tatu	Siku ya Nne
0800 – 0830	Maombi ya asubuhi	Maombi ya asubuhi	Maombi ya asubuhi	Maombi ya asubuhi
0830 – 1030	Kuwasili na usajili	Simulizi na shuhuda – simulizi mbili (Somo la 5)	Teolojia ya kufuatana nao (Somo la 8)	Ubia na ushirikiano kwa ajili ya uponyaji mkamilifu (Somo la 12)
1030 – 1100	Kuwasili na usajili	MAPUMZIKO MAFUPI	MAPUMZIKO MAFUPI	MAPUMZIKO MAFUPI
1100 – 1300	Kuwasili na usajili	Simulizi na shuhuda – simulizi mbili (Somo la 5)	Watoto, vijana na wanaolekea utu uzima na uponyaji kwa imani katika muktadha wa VVU (Somo la 9)	Utetezi na mawasiliano kwa ajili ya uponyaji mkamilifu (Somo la 13)
1300 – 1400	MAPUMZIKO YA CHAKULA CHA MCHANA	MAPUMZIKO YA CHAKULA CHA MCHANA	MAPUMZIKO YA CHAKULA CHA MCHANA	MAPUMZIKO YA CHAKULA CHA MCHANA
1400 – 1530	Kusudi na usuli wa mwongozo (Somo la 1 & 2)	Je, uponyaji kwa imani na matibabu/ tiba kwa imani ni nini? (Somo la 6)	Fasili mpya ya uponyaji kwa imani kwa jumuiya za kiimani zenye mtazamo wa kimageuzi (Somo la 10)	Uongozi wa kimageuzi kwa ajili ya uponyaji mkamilifu (Somo la 14)
1530 – 1600	MAPUMZIKO MAFUPI	MAPUMZIKO MAFUPI	MAPUMZIKO MAFUPI	MAPUMZIKO MAFUPI
1600 – 1800	Namna ya kutumia mwongozo na namna ya kuanza (Somo la 3 & 4)	Dawa za Kupambana na Virusi ni muujiza wa Mungu (Somo la 7)	Mikakati kwa ya uponyaji ajili mkamilifu (Somo la 11)	Majadiliano ya pamoja na matangazo
1800	MAPUMZIKO NA CHAKULA CHA USIKU	MAPUMZIKO NA CHAKULA CHA USIKU	MAPUMZIKO NA CHAKULA CHA USIKU	MAPUMZIKO NA CHAKULA CHA USIKU

ANGALIZO: Iwapo manusura kutokana na madhara ya madai ya uponyaji kwa njia ya imani pekee watakuwa ni miongoni mwa washiriki na iwapo watakuwa tayari kusimulia shuhuda za maisha yao wenyewe, shuhuda hizo zinaweza kuwa badala ya shuhuda zilizo kwenye Somo la 5.

Kiambatisho cha 7

Ratiba ya Mafunzo Inayopendekezwa kwa Viongozi wa Dini

Muda	Siku ya K	Siku ya pili	Siku ya tatu
0800 – 0830	MAOMBI YA ASUBUHI	MAOMBI YA ASUBUHI	MAOMBI YA ASUBUHI
0830 – 1030	Simulizi na shuhuda: simulizi mbili (Somo la 5)	Teolojia ya kufuatana nao (Somo la 8)	Ubia na ushirikiano kwa ajili ya uponyaji mkamilifu (Somo la 12)
1030 – 1100	MAPUMZIKO MAFUPI	MAPUMZIKO MAFUPI	MAPUMZIKO MAFUPI
1100 – 1300	Simulizi na shuhuda: simulizi mbili (Somo la 5)	Watoto, vijana, na wanaolekea utu uzima – uponyaji kwa imani katika muktadha wa VVU (Somo la 9)	Utetezi na mawasiliano kwa ajili ya uponyaji mkamilifu (Somo la 13)
1300 – 1400	MAPUMZIKO YA CHAKULA CHA MCHANA	MAPUMZIKO YA CHAKULA CHA MCHANA	MAPUMZIKO YA CHAKULA CHA MCHANA
1400 – 1530	Je, uponyaji wa kiimani au matibabu kwa imani/tiba ni nini? (Somo la 6)	Fasili mpya ya uponyaji kwa imani kwa jumuiya za kiimani zenye mtazamo wa kimageuzi (Somo la 10)	Uongozi wa kimageuzi kwa ajili ya uponyaji mkamilifu (Somo la 14)
1530 – 1600	MAPUMZIKO MAFUPI	MAPUMZIKO MAFUPI	MAPUMZIKO MAFUPI
1600 – 1800	Dawa za Kupambana na Virusi ni muujiza wa Mungu (Somo la 7)	Mikakati kwa ajili ya uponyaji mkamilifu (Somo la 11)	Majadiliano ya pamoja na matangazo
1800	MAPUMZIKO NA CHAKULA CHA USIKU	MAPUMZIKO NA CHAKULA CHA USIKU	MAPUMZIKO NA CHAKULA CHA USIKU

ANGALIZO: Iwapo manusura kutokana na madhara ya madai ya uponyaji kwa njia ya imani pekee watakuwa ni miongoni mwa washiriki na iwapo watakuwa tayari kusimulia shuhuda za maisha yao, shuhuda hizo zin-aweza kuwa badala ya shuhuda zilizo kwenye somo la 5.

Kiambaticho cha 8

Fomu za Tathmini ya Kabla ya Kuanza Mafunzo na Tathmini ya Baada ya Kumaliza Mafunzo

Fomu za Tathmini ya Kabla ya Kuanza Mafunzo

1. Jinsia _____ Kundi la Umri ☐ 15–24 ☐ 25–34 ☐ 35–49 ☐ 50–65 ☐ 65+

2. Je, unaelewa nini kuhusiana na suala la imani na uponyaji? _____

_____

_____

_____

_____

_____

3. Je, unadhani mtu yeyote anayeishi na VVU na ambaye ana UKIMWI anaweza akaponywa? Eleza kwa ufupi.

_____

_____

_____

_____

_____

4. Je, kwa kufika kwako kwenye mafunzo haya, una matarajio gani? _____

_____

_____

_____

_____

_____

5. Je, una hofu gani kuhusiana na mafunzo haya? _____

_____

_____

_____

_____

_____

Fomu za Tathmini ya Baada ya Kumaliza Mafunzo

1. Jinsia _____ Kundi la Umri ☐ 15–24 ☐ 25–34 ☐ 35–49 ☐ 50–65 ☐ 65+

2. Toa maoni yako kuhusu ubora wa vipengele vya mafunzo vifuatavyo
(5 = Ni ya Kiwango cha Kipekee, 4 = Nzuri sana, 3 = Nzuri 2 = Mbaya, 1 = Mbaya sana)

Uwezeshaji
☐ 1 ☐ 2 ☐ 3 ☐ 4 ☐ 5

Vifaa (Usafiri, Malazi, Chakula)
☐ 1 ☐ 2 ☐ 3 ☐ 4 ☐ 5

Mpangilio (Muda, Shughuli)
☐ 1 ☐ 2 ☐ 3 ☐ 4 ☐ 5

3. Orodhesha mambo matatu ambayo yameleta changamoto kwako katika mafunzo kuhusu uponyaji kwa imani na Dawa za Kupambana na Virusi

_____

_____

_____

_____

_____

Mafunzo haya yamenipa changamoto zenye kuleta msukumo chanya (5 = Ninakubaliana kabisa, 1 = sikubaliani kabisa)
☐ 1 ☐ 2 ☐ 3 ☐ 4 ☐ 5

Mafunzo haya yamenipa mahali pa kuanzia ili niweze kuwa mtetezi wa uponyaji mkamilifu katika jamii yangu (5 = Ninakubaliana kabisa, 1 = sikubaliani kabisa)
☐ 1 ☐ 2 ☐ 3 ☐ 4 ☐ 5

Nitawashawishi na kupendekeza kwa viongozi wenzangu mafunzo haya ili washiriki
(5 = Nakubaliana kabisa, 1 = sikubaliani kabisa)
☐ 1 ☐ 2 ☐ 3 ☐ 4 ☐ 5

Orodhesha maoni mengine yoyote unayoweza kuyatoa kuhusiana na mafunzo haya _____

_____

_____

_____

_____

_____

Mwongozo huu unasaidia kutupa mafunzo kuhusu ujuzi wa maisha ambao utazisaidia jamii zetu kuwa na afya na kuwa jumuishi kwa watu wote.

– Mchungaji Dk Olav Fykse Tveit, Katibu Mkuu wa WCC

Madai kuhusu upekee wa uponyaji kwa imani katika mazingira ya uwepo wa VVU na UKIMWI barani Afrika - kusini mwa jangwa la sahara huwashawishi watu wanaoishi na VVU kuachana na matumizi ya matibabu kama wanavyoshauriwa na madaktari wao. Mwongozo huu unakuja kama jibu la changamoto hiyo kwa kutoa mbinu zitakazowawezesha viongozi wa dini katika maeneo yote kwenye makanisa kuhamasisha uzingatiaji wa matibabu. Masomo yaliyomo yapo katika uhalisia, yamerahisishwa kwa msomaji na yameandaliwa kwa kufanyiwa majaribio katika mazingira halisi na pia yanaweza kutumika katika hali na mzingira tofauti tofauti.

Mwongozo huu ni miongoni mwa miongozo minne inayohusiana na VVU na UKIMWI ambayo imeandaliwa na Baraza la Makanisa Duniani, Mpango wa kiumini wa utetezi na kushughulikia VVU na UKIMWI (World Council of Churches' Ecumenical HIV and AIDS Initiatives and Advocacy, WCC-EHAIA) chini ya ufadhili wa Mpango wa pamoja kati ya Shirika la UKIMWI Duniani (Joint United Nations Programme on HIV and AIDS, UNAIDS) na Mpango wa Dharura wa Rais wa Marekani wa Kusaidia Masuala ya UKIMWI (the American President's Emergency Plan for AIDS Relief, PEPFAR).

World Council of Churches

Postal address:
P.O. Box 2100
CH-1211 Geneva 2
Switzerland

Visiting address:
150 Route de Ferney
Grand-Saconnex (Geneva)
Switzerland

Tel: (+41 22) 791 6111
Fax: (+41 22) 791 0361

www.oikoumene.org

worldcouncilofchurches @oikoumene @worldcouncilofchurches wccworld

Religion / Health

ISBN 978-2-8254-1717-1

9 782825 417171